Yametekelezwa	Endapo Taasisi imetekeleza mapendekezo kama inavyotakiwa na kuwasilisha ushahidi wa unaoonesha utekelezaji wa vipengele vyote vya mapendekezo
Hayajatekelezwa	Endapo taasisi imewasilisha ushahidi wa utekelezaji wa mapendekezo ambao hata hivyo haujitoshelezi katika kuthibitisha utekelezaji wa mapendekezo , au kushindwa kabisa kutoa ushahidi wa utekelezaji
Yamepitwa na wakati	Endapo mapendekezo yaliyotolewa yamepoteza uhalali kwasababu moja au nyingine.

Jedwali 2: Tathmini ya Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Miaka Iliyopita

Mwenendo wa Mapendekezo	2017/18		2018/19	
	Idadi	Asilimia	Idadi	Asilimia
Yametekelezwa	16	21	72	38.3
Hayajatekelezwa	60	78	112	59.6
Yamepitwa wakati	1	1	4	2.1

SURA YA TATU

3.0 UTHIBITI KATIKA MIFUMO YA TEHAMA

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nimekagua umadhubuti wa udhibiti katika mifumo ya TEHAMA ambayo husaidia uendeshaji wa shughuli katika baadhi ya taasisi na idara za Serikali. Ukaguzi niliofanya ulikijikita katika mawanda ya mifumo ya fedha, bajeti, manunuzi, na mifumo ya ukusanyaji mapato. Katika ukaguzi huu nilibaini mapungufu ya udhibiti katika mifumo hiyo. Mapungufu niliyobaini yanahusiana na kutofuatwa kwa sheria, taratibu, miongozi ya kitaifa na kimatifa na taratibu za kiutendaji. Mapungufu niliyobaini yanaweza kusababisha umepotevu wa mapato na kuwathiri taarifa za kifedha katika taasisi husika.

3.1 UDHAIFU WA UDHIBITI KATIKA MIFUMO YA TEHAMA

3.1.1 Udhaifu wa Uthibiti katika Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE)

Katika mwaka wa fedha 2019/20 nimekagua umadhubuti wa Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE), unaotumiwa na taasisi za serikali kama mbadala wa mfumo uliokuwa wa fedha uliokuwa ukitumika awali (IFMS Epicor). Katika ukaguzi wangu nimebaini mapungufu yafuatayo:

a) Usanidi usio sahihi katika usimamizi wa masurufu.

Katika ukaguzi wangu nimebaini kuwa mfumo umesanidiwa katika namna isiyojitosheleza katika usimamizi wa masurufu. Nimebaini kuwa utoaji wa masufuru na urudishwaji wa masufuru hurekodiwa na kuripotiwa kabla ya kurekodiwa kwenye hati ya malipo na kukamilika kwa hatua za malipo. Hii inaweza kusababisha madeni hewa, kupotosha taarifa za fedha au vyote. Pia nimebaini kuwa mfumo hauna leja zote zinazohitajika wakati wa utoaji wa masurufu, utoaji hati za malipo, malipo ya mwisho, na marejesho. Mfumo hauoneshi kwa uwazi ni akaunti/leja zipi zinazohusika katika kila hatua ya kulipa masurufu.

Nina mashaka kuwa mfumo unaweza ukawa na taarifa za madeni ilhali hakuna malipo halisi yaliyofanyika kwa mdaiwa. Hii huweza kusababisha upotoshaji wa taarifa za fedha.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuuboresha Mfumo wa Malipo Serikalini, ili masufuru yatambulike na kurekodiwa pale tu mchakato wa malipo utakapokamilika.

b) Mapungufu katika kurekodi miamala ya karadha (Prepayments)

Ukaguzi wangu umebaini kuwa Mfumo wa Malipo Serikalini haurekodi taarifa za karadha (prepayment) kwenye baadhi ya leja ndogo (sub ledgers). Nimebaini kuwa wakati wa mchakato wa karadha, mfumo unarekodi miamala katika hatua za mwisho, ambapo katika hatua hizo kiachofanyika ni kupunguza kifungu cha matumizi na kuongeza kitabu cha fedha au akaunti ya benki, na kutoweka kumbukumbu kwenye leja za madai. Aidha, mapitio yangu ya taarifa za mfumo yamebaini kuwapo kwa taarifa za mali ilhali hakuna malipo ya awali kabla ya kupata huduma yaliyofanyika. Hii husababisha ugumu wa kutambua ni madai ya huduma gani iliyotolewa.

Maoni yangu ni kuwa, ukosefu wa taarifa sahihi za miamala katika mfumo kunaweza kusababisha upotoshaji wa taarifa za fedha.

Ninapendekeza kwa Wizara ya Fedha na Mipango:

- Kuchunguza kama bakaa za akaunti na leja zinazohusika zimerekodi kwa usahihi taarifa za malipo ya awali kabla ya kupata huduma.
- Kusanidi mfumo ili uwezeshe kurekodi leja zote wakati wa mchakato wa malipo ya awali kabla ya huduma.

c) Miamala ya matumizi kufanyika katika namna inayokinzana na Mwongozo wa IPSAS

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inatumia mfumo wa kimataifa wa kanuni za hesabu za fedha katika sekta ya umma (IPSAS) toka tarehe 1 Julai 2004, kwa mamlaka ya serikali za mitaa, serikali kuu, na mashirika ya umma. Hatua hii ilishajihishwa na hatua ya kuanza kufuatwa Mwongozo wa kimataifa katika ukaguzi na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA). Hii ilipelekea taasisi zote za umma kutumia mwongozo wa IPSAS - isiyu taslim (accrual basis) katika uandaaji hesabu za fedha.

Nimebaini kuwa mfumo umesanidiwa ili kuzuia miamala kufanyika na kurekodiwa endapo hakuna bakaa katika kifungu husika cha matumizi. Usanidi unazuia kutambua na kurekodi matumizi kinyume na mwongozo wa IPSAS unaoelekeza Taasis kutambua matumizi pale yanapofanyika na sio fedha zinapolipwa.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuuboresha mfumo ili uwezeshe usahihi katika kurekodi na kuripoti taarifa za fedha kwa mujibu wa mwongozo wa IPSAS.

d) Mapungufu katika udhibiti wa Akaunti za Udhibiti

Akaunti za Udhibiti ni muhtasari wa akaunti za leja kuu. Kazi ya control account ni kuhifadhi taarifa za kina za leja kuu. Taarifa hizi hujumuisha jumla ya miamala inayohifadhiwa katika leja ndogondogo. Kwa kawaida akaunti hizi huwa na muhtasari wa madai na madeni kwa sababu akaunti hizi huwa na taarifa nyingi.

Ukaguzi wangu umebaini kuwapo kwa bakaa kwenye Akaunti za Udhibiti (suspense accounts na control accounts) ambazo hazikuwainishwa kwenye taarifa ya fedha. Hii inaashiria kuwa, mfumo unaruhusu watumiaji kupitisha miamala ikiwemo marekebisho ya miamala katika Akaunti za Udhibiti nje ya utaratibu wa kawaida. Kihisibu, Akaunti za Udhibiti hazitakiwi kuwa na bakaa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha, na endapo kutakuwa na bakaa katika akaunti hizo italazimu uainishwaji wa bakaa hizo kwenye taarifa ya fedha na uainishwaji huo uambatane na vielelezo vya sababu zilizopelekea kuwapo kwa bakaa hizo.

Nina shaka kuwa miamala isiyoidhinishwa inaweza kupitishwa katika Akaunti za Udhibiti na leja kuu na kusababisha upotoshaji wa taarifa za fedha.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango

- **Kuchunguza bakaa zilizopo kwenye Akaunti za Udhibiti ili kuhakikisha kuwa hakukuwa na miamala isiyoidhinishwa iliyopitishwa katika kipindi husika.**
- **Taasisi ziweke udhibiti katika control accounts na leja kuu katika mfumo ikiwemo kudhibiti upitishaji wa miamala.**

e) Mfumo kushindwa kuandaa taarifa za fedha

Mapitio ya mfumo yamebaini kuwa, taasisi zinazotumia mfumo zinashindwa kuandaa taarifa za fedha ndani ya mfumo, kinyume na matakwa ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 inayoelekeza taarifa za fedha kuandaliwa ndani ya mfumo.

Kwa muktadha wa wingi wa miamala inayofanywa na taasisi kwa kutumia mfumo wa MUSE, ni wazi kwamba ubora wa taarifa za fedha ungeboreshwa kwa kiasi kikubwa endapo mfumo ungewezesha uandaaji wa taarifa za fedha na hesabu.

Nina shaka kuwa bila kutumia mfumo katika kuandaa taarifa za fedha na hesabu, taarifa na hesabu zitakabiliwa na makosa, upungufu, na kuchezewa kwa makusudi. Mambo hayo yatasababisha upotoshaji wa taarifa za fedha.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kuwa mfumo unaboreshwa ili taasisi za serikali ziweze kuandaa taarifa za fedha zenye taarifa sahihi.

f) Wahasibu kushindwa kuhakiki taarifa za akaunti za leja kuu zinazohusika wakati wa kuandaa miamala.

Katika ukaguzi wangu nimebaini kuwa ingawa mfumo umesanidiwa kuhakikisha kuwa miamala inaakisiwa katika leja stahiki, watumiaji wa mfumo (wahasibu) hawawezi kuhakiki miamala wanayofanya kabla ya kurekodi miamala (posting transactions).

Ni maoni yangu kuwa, kitendo cha watumiaji wa mfumo (wahasibu) kushindwa kuhakiki miamala na kuona leja zinazowina na miamala hiyo pindi wanapoituma kwenye vitabu vya fedha vinavyotumika katika uandaaji wa taarifa za fedha kunaweza kusababisha kuwapa kwa taarifa ambazo sio sahihi na kusababisha urekebishaji wa miamala ambao ungeweza kuepukika endapo tu wahasibu wangukuwa na uwezo wa kuhakiki miamala wakati wa kuituma.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuuboresha mfumo iwawezeshe wahasibu kuhakiki miamala wanayoituma kwenye vitabu vya fedha, kwa kuwapa fursa ya kuona leja zinavyowiana na miamala hiyo.

3.1.2 Udhhibiti dhaifu katika mifumo ya Votebook, Sage Pastel Evolution, Quickbooks, Sage AccPac, Advance na Front

Katika mwaka wa fedha 2019/20, nimekagua mifumo ya uhasibu ya Chuo Kikuu Cha Soikoine (SUA), Shirika la Nyumba (NHC), Baraza la Mitihani (NACTE), Chuo cha kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), CDTF, na ARUWASA kuangalia umadhubuti wa udhibiti kwenye mifumo ya fedha katika taasisi husika, ili nipate uhakika na usahihi wa taarifa za fedha

zitokazo kwenye mifumo husika. Ukaguzi wangu umebaini mapungufu yatokanayo na kutokuwapo kwa uwezo wa kiutendaji (Functionality) wa kutengeneza taarifa za fedha (Financial Statements), tofauti kati ya 'General ledger' na 'Trail Balance', usimamizi usioridhisha wa mali, kutokuwapo kwa mgawanyo wa majukumu, watumiaji wa mfumo kuwa na haki za utumiaji mfumo zaidi ya majukumu waliyopangiwa, na kushindwa kutumia mfumo katika baadhi ya maeneo kutokana na masharti ya leseni.

Ukaguzi wangu wa mfumo wa Votebook unaotumiwa na Shirika la Nyumba (NHC), umebaini kutokuwapo kwa ripoti ya 'Account Payable Aging Analysis'. Uchambuzi huu ni muhimu katika kuandaa na kutoa taarifa ya fedha kwani huelezea kwa kina usahihi na utimilifu wa bakaa za madeni yaliyoripotiwa katika taarifa ya fedha. Nilipotaka ufafanuzi, niliarifiwa na uongozi wa Shirika la Nyumba la Taifa kuwa mfumo wa fedha yaani Votebook hauna uwezo wa kufanya 'Payable Aging Analysis' hivyo hulilazimu shirika kufanya 'aging analysis' bila kutumia mfumo jambo linalosababisha makosa ya kibinadamu kimakusudi au kibahati mbaya.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa ripoti ya 'Payable aging analysis' kutasababisha Shirika kushidwa kutambua na kuripoti madeni ya muda mrefu ambayo bado hayajalipwa.

Ninashauri uongozi wa Shirika la Nyumba kuhakikisha kwamba ripoti ya 'Aging analysis' inaandaliwa kwa kutumia mfumo wa uhasibu kwa ajili ya usahihi na utimilifu wa bakaa za madeni zinazoripotiwa katika taarifa za fedha.

Pia nilikagua mfumo wa uhasibu wa Sage ACCPac unaotumiwa na Chuo cha kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), ambapo nilibaini kwamba mfumo hauna uwezo wa kutoa mchanganuo wa madeni ya wanafunzi kwa kuzingatia muda 'student debtors aging schedule', mchanganuo ambao husaidia ufuatiliaji wa makusanyo ya madeni ya wanafunzi. Kukosekana kwa mchanganuo huo kulisababisha nishindwe kupima uwezo wa chuo katika kurejesha madeni.

Vilevile, kutokana na sampuli za miamala kutoka kwenye leja kuu (General Ledger) na urari (Trial Balance) nimebaini kuwa mfumo hutoa muhtasari wa taarifa za leja kuu 'general ledger' za bakaa za akaunti, ambapo miamala ya kipindi cha mwezi mmoja hujumlishwa na kuripotiwa kama muamala mmoja ndani ya mwezi husika, badala ya kuwa na taarifa za muamala

mmoja mmoja. Jambo hili limesababisha kutofautiana kwa taarifa za kwenye leja kuu (General Ledger) na taarifa za kwenye urari (Trail Balance) kama ilivyoainishwa kwenye safu G katika jedwali nambari moja. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa kina kwenye taarifa za madeni ya wanafunzi katika mfumo wa taarifa za wanafunzi (OISM) nimebaini kuwa bakaa za wanafunzi wanaodaiwa kwa mujibu wa mfumo zinalingana na taarifa za madeni kwenye urari (Trail Balance).

Jedwali Na. 1: Tofauti kati ya Leja kuu na Urari

Code & name of the general ledger	Salio Anzia (Sh.)	Muhtasari wa Madeni (Sh)	Muhtasari wa Mapato (Sh.)	Bakaa ya Jumla ya Miamala	Bakaa ya Mwisho kutoka ACCPACC	Tofauti (Sh.)
	A	B	C	D	E	G (D - E)
655-Students debtors	1,681,468,903	10,255,227,400	7,056,678,403	4,880,017,900	1,961,754,875	2,918,263,025
322-Advertisement	-	74,380,660	-	74,380,660	96,857,600	22,477,000
418-Personnel emolument	-	8,597,173,348	-	8,597,173,348	8,644,708,905	47,535,357

Chanzo: Taarifa ya leja kuu na urari kutoka mfumo wa Sage AccPac

Maoni yangu ni kuwa, mapungufu niliyoyabaini yanasababisha kukosekana kwa taarifa zitazosaidia usimamizi na udhibiti wa madeni ya wanafunzi, vilevile bakaa za leja kuu hazitoi taarifa sahihi kwa wafanya maamuzi.

Ninashauri uongozi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kuhakikisha kuwa mfumo wa fedha unatoa 'ageing report' kwa madeni ya wanafunzi na taarifa za kina kwa kila muamala katika leja kuu.

Pia, nilifanya ukaguzi wa mfumo wa 'Sage Pastel Evolution' unaotumiwa na Baraza la Mitihani ambapo nilibaini kutounganishwa kwa moduli ya uhasibu na moduli ya mali zisizohamishika, jambo hili linasababisha uhamishaji wa taarifa za thamani za mali zisizohamishika kutoka kwenye moduli ya mali, kwenda kwenye moduli ya uhasibu, kutozingatiwa kwa miongozo ya usalama wa nywila, uwezo wa akaunti ya mtumiaji kujifunga ikikaa bila kutumiwa, na ukomo nywila kutumika. Vilevile nimebaini toleo la mfumo linalotumika, yaani toleo namba 7.20.2.000 la mwaka 2016 limepitwa na wakati na pia mkandarasi wa mfumo ameacha kutoa msaada wa kiufundi katika toleo hilo.

Maoni yangu ni kuwa, kutounganishwa kati ya moduli ya uhasibu na moduli ya mali zisizohamishika, kunaweza kusababisha makosa ya kibinadamu wakati wa uhamishaji wa taarifa za thamani za mali, kutoka moduli ya mali kwenda kwenye moduli ya uhasibu, na hii itasababisha makosa katika taarifa za fedha. Pia kutumia toleo la mfumo lililopitwa na muda kunaweza kusababisha kutopatikana kwa utatuzi wa matatizo ya kiufundi pindi hitilafu

ikitokea. Na zaidi kutozingatiwa kwa miongozo ya usalama wa nywila na akaunti za watumiaji wa mfumo kunaweza kusababisha uvujaji taarifa za mfumo na hivyo kuhatarisha usalama wake.

Ninapendekeza uongozi wa Baraza la Mitihani la Taifa kurekebisha mapungufu yaliyobainika katika mfumo wa uhasibu ikiwemo kuunganisha moduli ya uhasibu na moduli ya mali zisizohamishika. Pia ninashauri kuhakikisha baraza linafuata miongozo ya usalama wa nywila na akaunti za watumiaji wa mfumo, na kuboresha toleo la mfumo kwenda kwenye toleo linalopata msaada wa kiufundi kutoka kwa mkandarasi wa mfumo.

Ukaguzi wangu wa mfumo wa uhasibu, pia ulitathmini kuzingatiwa kwa mgawanyo wa majukumu katika mfumo hiyo, nikiwa na malengo ya kujiridhisha kuwa majukumu ya kihasibu yanayokinzana yametenganishwa. Ukaguzi wangu wa mfumo wa Votebook unaotumiwa na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) ulibaini kuwa watunza fedha wamepewa haki kwenye mfumo ya kufanya usuluhishi wa kibenki. Kulingana na miongozo ya kihasibu watunza fedha hawapaswi kuhusika na usuluhishi wa kibenki.

Pia, nilibaini kuwa maafisa TEHAMA wamepewa majukumu ya kiutendaji kwenye mfumo kama vile haki za usimamizi wa madeni, usimamizi wa hati za manunuzi (LPO) kinyume na majukumu yao kama maafisa TEHAMA. Vilevile nilipitia miamala ya mapato katika Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Shajara za hati ya malipo (Journal Vouchers), kwa kuchukua sampuli ya miamala ya mapato yatokanayo na uuzaji wa nyumba na viwanja, ambapo nilibaini miamala 9(31%) kati ya miamala 29 yenye thamani ya Tsh milioni 796.69 Tsh iliandaliwa, kuhakikiwa, na kuidhinishwa na mtu mmoja katika mfumo wa uhasibu wa Votebook.

Mapitio ya mfumo wa uhasibu wa Quickbooks unaotumiwa na Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (SOUWASA), yalibaini kuwa mfumo huo hauna udhibiti wa ngazi za matumizi kwa maana ya uanzishaji, kuhakiki, na uidhinishaji wa miamala. Hii husababisha taarifa za miamala zinazoingizwa na wahasibu, kwenda moja kwa moja kwenye leja kuu bila kuhakikiwa na kuidhinishwa na maafisa katika ngazi za juu. Pia mapitio yangu yamebaini kuwa uingizwaji wa taarifa za vifaa vilivyopokelewa katika mfumo upo wazi kwa kila mtumiaji badala ya uwezo huo kuwa nao mtunza vifaa peke yake. Hii ina maana kuwa afisa yeyote anaweza kuingiza taarifa ya kupokea vifaa bila mtunza vifaa kufahamu, wala kuhusishwa.

Udhaifu huu ulisababisha matukio ambayo mtunzaji kubaini kurekodiwa kwenye mfumo kwa baadhi ya taarifa za vifaa vilivyopo stoo pasi na kuona vifaa husika. Hali kadhalika nimefanya mapitio ya mfumo wa uhasibu katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha (ARUWASA) na kubaini kuwa afisa mmoja ana ruhusa ya kuanzisha na kufuta (Reverse transactions) miamala. Mfumo haujasimikwa kumzuia mtumiaji kufanya na kufuta muamala bila kuidhinishwa na afisa wa ngazi ya juu.

Maoni yangu ni kwamba, udhibiti usiotosheleza katika kuhakikisha mgawanyo wa majukumu kwenye mfumo wa uhasibu huchangia hatari ya kukosewa kwa taarifa za fedha, zinazoweza kusababishwa na vitendo vya ubadhirifu au/na makosa ya kibinaadamu kukiwa na uwezekano wa udanganyifu katika mchakato wa kuandaa taarifa za fedha.

Ninapendekeza:

- (a) Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Kilimo (SUA) kuondoa hali za utumiaji mfumo (access rights) kwa watumiaji ambao imebainika kuwa haki walizopewa zinakinzana na miongozo ya mgawanyo wa majukumu. Pia menejimenti ihakikishe inafanya mapitio ya mara kwa mara katika haki za utumiaji wa mfumo ili kuhakikisha kuwa hazi za utumiaji mfumo zinalingana na majukumu ya watumiaji.**
- (b) Menejimenti ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kuhakikisha mgawanyo wa majukumu katika mchakato wa kuanzisha na kuidhinisha shajara za hati za malipo (Journal vouchers) kunazingatiwa.**
- (c) Menejimenti ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Songea (SOUWASA) ihakikishe kuwa ngazi za udhibiti zinakuwepo katika mfumo wake wa fedha (QuickBooks) ili kuepusha makosa wakati wa matumizi ya mfumo.**
- (d) Menejimenti ya Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha (ARUWASA) iweke na kudhibiti mgawanyo wa majukumu katika mfumo wake wa fedha.**

Pia nimepitia mfumo wa uhasibu wa Front unaotumiwa na Mfuko wa Maendelo ya Pamba (CDTF) umebaini kuwa mfumo hauruhusu watumiaji tofauti kuingia kwenye mfumo kwa wakati mmoja, mtumiaji mmoja tu ndio anaruhusiwa kuingia kwenye mfumo jambo linalosababisha watumiaji wa

mfumo kutumia akaunti ya meneja wa fedha ambaye hayupo kazini kwa sasa. Hii imetokana na ufinyu wa idadi ya watumiaji kwa mujibu wa masharti ya leseni ya utumiaji.

Maoni yangu ni kuwa, hali hii huathiri utendaji kwani ni mtumiaji mmoja tu anaweza kuingia kwenye mfumo kwa wakati mmoja, pia huondoa uwajibikaji kwani watumiaji wa mfumo wanatumia akaunti moja.

Ninapendekeza uongozi wa Mfuko wa Maendeleo ya Pamba kufanya mawasiliano na Mkandarasi wa mfumo ili uweze kupata leseni itakazokidhi mathitaji ya mfuko.

3.1.3 Udhaifu wa udhibiti katika mfumo wa uhasibu wa Advance

Nimefanya ukaguzi wa mifumo katika Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), ambapo nimebaini kuwa Mamlaka inatumia mfumo wa uhasibu wa Advance ambao umeunganishwa na mfumo wa bajeti unaoitwa Budget Portal. Malipo kwa ajili na watumishi wa Mamlaka na wazabuni huanzishwa na kuidhinishwa katika mfumo wa Budget Portal, kisha hutumwa katika mfumo wa uhasibu kwa ajili ya malipo na kuhifadhiwa katika leja kuu.

Mapitio yangu ya mfumo wa uhasibu na namna ulivyounganishwa na mfumo wa Budget Portal umebaini mapungufu ya kiudhibiti yafuatayo:

- Mfumo unaruhusu maombi ya malipo ya masurufu kufanywa kwa njia ya maombi ya malipo ya kawaida. Hali hii inaondoa ulazima kwa mlipwaji kufanya 'retirement'. Hii inatokana na mfumo kutumia fomu moja katika uanzishaji wa maombi ya aina zote ambapo muombaji huchagua aina ya malipo ili kutofautisha baina ya maombi ya masurufu na maombi ya kawaida. Hata hivyo mfumo haumzuii muombaji kuendelea na utengenezaji wa hati ya malipo hata kama ombi la kuomba malipo ya masurufu litatumika katika kufanya maombi ya safari.
- Upungufu mwingine ni katika ununuzi wa tiketi za ndege, mfumo unaruhusu maafisa manunuzi kubadilisha kiasi kilichopo kwenye gharama za tiketi za ndege katika mfumo wa uhasibu wa Advance, hii hubatilisha uidhinishaji wa kiasi cha gharama za tiketi husika ambao unafanyika katika mfumo wa kibajeti.
- Katika kutengeneza hati za malipo (LPO) mtumiaji wa mfumo anatakiwa kuingiza nambari ya maombi ya malipo inayolandana na nambari ya

kasma iliyopo katika mfumo wa bajeti. Hata hivyo mfumo haumzii mtumiaji endapo atatumia nambari tofauti ya kasma isiyohusiana na malipo husika, bali huruhusu mtumiaji kufanya malipo kwa kutumia kasma yoyote ile ili mradi iwe imeidhinishwa.

- Mtumiaji anaweza kubadili msimbo wa akaunti na kiwango cha malipo kwenye mfumo wa uhasibu katika kufanya malipo yanayohusiana na posho ya kujikimu (perdiem) wakati wa kutengeneza hati ya malipo. Hali hii hubatilisha udhibiti wa uidhinishaji uliowekwa kwenye mfumo wa budget portal.
- Mfumo unashindwa kurejesha kasma zilizotengwa kwa miamala iliyofutwa (transaction reversals), hii hulazimisha urejeshaji wa kasma za miamala hiyo kufanywa na mhasibu badala ya mfumo kufanya wenyewe bila juhudi za kibinadamu.
- Uhakiki na uidhinishaji wa kutoa vifaa vilivyopo stoo unafanyika nje ya mfumo, jambo linalopelekea matumizi mabaya ya mfumo, kwani mtumiaji anaweza kutoa vifaa bila ya idhini na mtunzaji wa vifaa. Pia utoaji wa vifaa katika mfumo hufanywa na mtu mmoja baada ya fomu ya kuchukua vifaa (requisition form) kujazwa na kuidhinishwa nje ya mfumo. Hii hupelekea utolewaji wa vifaa bila kuidhinishwa.
- Malipo huanzishwa katika mfumo wa budget portal, na baada ya kuidhinishwa hutumwa kwenye mfumo wa uhasibu kwa ajili ya malipo. Hata hivyo nimebaini kuwa hakuna usahihishaji wa taarifa za miamala, ambapo mfumo wa uhasibu haurudishi taarifa za miamala iliyofutwa kwenye mfumo wa budget portal, hii husababisha miamala hiyo kuendelea kuonekana kuwa imelipwa katika mfumo wa budget portal.

Ninadhani kuwa mapungufu yaliyobainika yanasababishwa na usimikaji mfumo usio sawia na kutokuwekwa kwa udhibiti unaostahili wakati wa usimikaji wa mfumo.

Ninaamini kuwa mapungufu yaliyobainika kama yalivyooredheshwa hapo juu yanaweza kusababisha taarifa zisizo sahihi za miamala pia kusababisha makosa katika uandaaji wa taarifa za fedha.

Ninapendekeza menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro kuchukua hatua zifuatazo;

- (a) Kuimarisha udhibiti katika mfumo wa uhasibu wa Advance ili kuzuia utengenezaji wa hati za malipo (Payment vouchers) kwa ajili ya malipo ya masurufu, kufanyika kwa kutumia nambari za malipo ya kawaida, na kinyume chake.
- (b) Mfumo wa uhasibu uboreshwe ili kuzuia kuhariri au kubadilisha kiwango kilichoidhinishwa kwenye mfumo wa budget portal kwa maombi ya kufanya manunuzi wakati wa utengenezaji wa hati ya manunuzi (LPO). Sambamba na hili kiwango halisi wakati wa kufanya manunuzi, kiingizwe kwenye mfumo wa budget portal na kiidhinishwe endapo kutakuwa na tofauti kati ya kiwango kilichoidhinishwa wakati wa maombi na kiwango halisi wakati wa kufanya manunuzi.
- (c) Kuhakikisha mfumo wa uhasibu unazuia ubadilishaji wa kiwango na msimbo wa malipo kwenye malipo ya fedha za kujikimu wakati wa utengenezaji wa hati za malipo ili kuzuia ubadilishaji wa uidhinishwaji wa malipo hayo uliofanyika kwenye mfumo wa budget portal.
- (d) Kuboresha mfumo wa uhasibu, ili uweze kurejesha kasma katika vifungu husika endapo miamala itarejeshwa au kufutwa.
- (e) Kuboresha mfumo wa Budget Portal, ili ujazaji na uidhinishaji wa fomu za kuchukulia vifaa stoo (requisition form) ufanyike kwenye mfumo kabla kutambuliwa na mfumo wa uhasibu.
- (f) Mfumo wa uhasibu ujengewe uwezo wa kupeleka mrejesho kwenye mfumo wa budget portal. Hii itatokea pale miamala imerejeshwa au kufutwa katika hatua za malipo kwenye mfumo wa uhasibu.

3.1.4 Udhaifu wa kiudhibiti katika mfumo wa FFARS

FFARS ni mfumo wa kifedha uliotengenezwa na kusimamiwa na Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa malengo ya kuzisaidia Serikali za Mitaa katika usimamizi wa mapato na matumizi kwenye vituo vya afya na shule.

Mapitio yangu ya mfumo wa FFARS yamebaini kuwa mfumo hautunzi taarifa za vitendo au matukio yanayofanywa na watumiaji kwenye mfumo 'audit trail', kumbukumbu za vitendo vya mtumiaji wa mfumo pale mtumiaji

anapotumia mfumo husika kwa ajili ya kuweka uwajibikaji endapo mtumiaji atatumia mfumo kinyume na taratibu zilizowekwa. Pia nimebaini kuwa mfumo hauna utaratibu wa kuidhinisha marekebisho au ufutwaji wa miamala jambo linalopelekea uidhinishaji wa marekebisho ya miamala kufanyika nje ya mfumo na hivyo kutozuia watumiaji kufanya marekebisho ya miamala ndani ya mfumo bila kuidhinishwa. Zaidi, nimebaini kuwa mfumo hauna taarifa inayoonesha miamala iliyofanyiwa marekebisho au kufutwa.

Ni matumaini yangu kuwa mapungufu yaliyobainishwa yatasababisha urekebishaji wa miamala isiyoidhinishwa na Serikali za Mitaa kushindwa kuwawajibisha watumiaji wa mfumo endapo watafanya vitendo ambavyo ni kinyume na taratibu za matumizi ya mfumo.

Ninapendekeza uongozi wa TAMISEMI kuuboresha mfumo wa FFARS ili uwezeshe uidhinishaji wa marekebisho ya miamala kufanyika ndani ya mfumo, pia mfumo uwe na uwezo wa kutunza taarifa za vitendo vya mtumiaji wa mfumo.

3.2 UDHIBITI DHAIFU KATIKA MFUMO WA MANUNUZI

Mwaka 2016, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) iliingia mkataba na European Dynamics kwa ajili ya kubuni, kutengeneza, kusambaza, kusanikisha, kusanidi, na kujenga uwezo wa vifaa na kimfumo kwa ajili ya mfumo wa manunuzi unganifu wa kieletroniki (TANePS). Mfumo huo umekuwa ukitumiwa na taasisi inayofanya manunuzi (Taasisi na idara za Serikali) chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) tangu mwaka 2018.

Nimeukagua mfumo wa TANePS na namna unavyofanya kazi, na kubaini mapungufu katika maneo yafuatayo: utekelezaji wa mkataba, kuwapo kwa taarifa kwa ajili ya kusaidia wafanya maamuzi, baadhi ya michakato ya kimanunuzi kuhitaji jitihada za kibinadamu, kutokuwepo na uthibitisho wa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo, kutokuwepo uwiano kati ya aina ya zabuni na hatua za zabuni, na haki za kutumia mfumo kwa wasimamizi wa mfumo.

a) Utekelezaji wa mkataba usioridhisha

Nimepitia taratibu za upatikanaji, na utengenezaji wa mfumo nikiangazia uwezo wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) katika Nyanja za kiufundi, kutoa msaada kwa watumiaji na usimamizi wa mfumo ambapo nimebaini mambo yafuatayo: -

- Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) haina uwezo wa kitaalamu wa kusimamia na kuuendesha mfumo kwani mpaka wakati ukaguzi unafanyika mnamo Septemba, 2020 bado Mamlaka ya Manunuzi ya Umma ilikuwa ikimtegemea mkandarasi katika kufanya maboresho ya mfumo. Pia nimebaini ushirikishwaji hafifu wa wataalamu wa TEHAMA wa Mamlaka katika kubuni na kutengeneza mfumo kama ilivyohitajika katika mkataba.
- Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) haijapokea hatimiliki ya mfumo (Intellectual Property), na pia nimebaini kuwa PPRA haijapatiwa umiliki wa 'source code' za mfumo ingawa muda wa udhamini (warranty period) umeisha miaka miwili iliyopita kinyume na kifungu GCC 15.4 cha mkataba. Hii imesababisha PPRA kushindwa kufanya maboresho ya mfumo bila kumshirikisha mkandarasi.
- Kukosekana kwa maelezo ya kina juu ya mafunzo waliyopewa wataalamu wa PPRA kama ilivyoielezwa katika mpango wa usimamizi wa mabadiliko (Change Management Plan - D13), ibara ya 2.4 kuwa "Kutakuwa na mafunzo ya kina kwa wataalamu wa PPRA na wafanyakazi wengine watakaosaidia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) kutekeleza majukumu ya kusimamia uendeshaji wa mfumo wa TANEPS".
- Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (TANEPS) haina mpango unaoonesha mkakati wa kuchukua umiliki na uendeshaji wa mfumo kutoka kwa mkandarasi.

Maoni yangu ni kuwa, mapungufu yaliyobainishwa yanaweza kutishia uendelevu wa mfumo kutokana na utegemezi uliopitiliza kwa mkandarasi wa mfumo. Pia wasiwasi kuwa gharama za kutunza mfumo zinaweza zisiwe himilivu kwa serikali kwani kwa sasa ada ya mwaka ya kutunza mfumo ni Dola za Kimarekani 129,381.10 ikijumuisha kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

Ninapendekeza Menejimenti ya Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) kuhakikisha: -

- (a) ‘Source code’ za mfumo zinakabidhiwa kwa PPRA haraka iwezekanavyo, ikiwa ni pamoja na kuundwa kwa timu ya wataalamu ili kuanzisha mchakato wa kuhamisha maarifa (Kuhusu mfumo) kabla ya ukomo wa muda wa waranti ambao ni mwezi Desemba 2021.**
- (b) Mkandarasi atoe mafunzo kwa timu ya wataalamu wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) ili kuwawezesha kutimiza majukumu ya kutoa msaada wa kiufundi na kuendesha mfumo wa TANEPS.**
- (c) Mamlaka iandae Mpango wa kina kuhusu mkakati wa kuchukuwa usimamizi na uendeshaji wa mfumo, unaoelezea kwa kina vitu vinavyohitajika ili kuwezesha zoezi hilo.**
- (d) Mkandarasi asipewe haki ya kuingia kwenye ‘server’ na kanzidata ya mfumo bila udhibiti**

Ukaguzi wangu wa mfumo wa TANEPS umebaini kuwa mkandarasi ana ruhusa ya kuingia kwenye mfumo na kanzidata ‘database’ ya mfumo pasi na udhibiti mbali na mfumo kuwa umeshakabidhiwa kwa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma (PPRA) na muda wa waranti kupita. Kwa kawaida mkandarasi anatakiwa apewe ruhusa ya kuingia kwenye mfumo panapokuwa na uhitaji hata hivyo mpaka mwezi Septemba, 2020 wakati wa ukaguzi unafanyika mkandarasi pekee ndiye alikuwa na haki za kuingia na kusimamia kanzidata ya mfumo bila usimamizi wa mamlaka.

Usimamizi wa ‘server’ na kanzidata ya mfumo kufanywa na mkandarasi, kunamaanisha kwamba PPRA haiwezi kufanya jambo lolote kwenye ‘server’ na kanzi data ya mfumo bila kumshirikisha mkandarasi. Pia nilibaini kuwa wataalamu wa PPRA hawana uwezo wa kuingia kwenye ‘server’ na kanzidata ya mfumo, jambo linalopelekea kushindwa kufuatilia na kutambua vitendo visivyoruhusiwa vinavyoweza kufanywa na mkandarasi.

Ninapendekeza Menejimenti ya Mamlaka ya manunuzi (PPRA) kuchuhukua hatua zifuatazo

- (a) Kuhakikisha ruhusa aliyopewa mkandarasi kuingia katika 'server' na kanzidata ya mfumo inaondolewa, na PPRA ihakikishe kuna uhabibiti wa kuingia na kutumia 'server' na kanzidataya mfumo.
- (b) Kuwepo na utaratibu ambao utahakikisha mkandarasi anapewa haki ya kuingia kwenye 'server' na kanzidata ya mfumo pale tu inapohitajika, na
- (c) Kuhakikisha kuwa akaunti za watumiaji ambao wana uwezo wa kuingia kwenye 'server' na kanzidata ya mfumo ziwe zinafuatiliwa na kupitiwa mara kwa mara ili kuhakikisha kwamba hawafanyi vitendo visivyoruhusiwa katika kuuathiri mfumo huo.
- (d) Mfumo kukosa taarifa muhimu kwa ajili ya kufanya maamuzi

Moja kati ya majukumu ya PPRA kama ilivyoielezwa katika kifungu cha 9(b) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya mwaka 2011, ni kufuatilia na kuripoti utendaji wa mfumo wa manunuzi ya umma na kuishauri serikali kufanya mabadiliko yanayohitajika katika mfumo wa manunuzi. Katika kutekeleza majukumu yake kifungu cha 36(l) cha sheria hiyo hiyo kinaelekeza maafisa wa taasisi za umma kuwasilisha orodha ya mikataba ya manunuzi ilizotolewa, mpango wa manunuzi, na orodha ya taasisi zisizotakiwa kupewa zabuni.

Ukaguzi wangu wa mfumo wa manunuzi (TANePS) umebaini kuwa, mfumo hauna uwezo wa kutambua idadi ya taasisi za serikali ambazo zimetuma mpango wa manunuzi wa mwaka. Pia nimebaini mfumo hauna uwezo wa kutoa taarifa kuhusu jumla ya taasisi zinazofanya manunuzi zilizopo, idadi ya taasisi zilizowasilisha mpango wa mwaka wa manunuzi, idadi ya taasisi ambazo hazikuwasilisha mpango wa manunuzi wa mwaka, na idadi ya mikataba ya manunuzi iliyotekelezwa katika kiwango cha nchi na kitaasisi.

Ni maaoni yangu kuwa kukosekana kwa taarifa ambazo zitaosadia PPRA katika kufanya maamuzi, zikiwemo taarifa zilizoosodheshwa hapo juu, kunadhoofisha malengo ya mfumo katika kuisadia Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

Ninapendekeza uongozi wa Mamlaka ya manunuzi

- (a) Kuuboresha mfumo ili uweze kutoa taarifa zifuatazo kwa muhtasari: Jumla ya idadi ya taasisi zinazofanya manunuzi, taasisi ambazo zimewasilisha mpango wa mwaka wa manunuzi, na idadi ya mikataba ya manunuzi iliyotekelezwa katika ngazi ya kitaifa na kitaasisi.
- (b) Pia ipitie na kubainisha taarifa zote muhimu ambazo zitasadia uongozi katika kufanya maamuzi na kutekeleza majukumu ili mfumo uweze kuwa na taarifa hizo.
- (c) Baadhi ya hatua za mchakato wa manunuzi kufanyika nje ya mfumo

Nimepitia kiwango cha shughuli na hatua za manunuzi zinazofanyika kwa kutumia mfumo bila kuhitaji utashi wa watendaji, ambapo nimebaini kuwapo kwa baadhi ya hatua za manunuzi ambazo zinafanyika nje ya mfumo ambazo ni: Manunuzi yenye thamani isiyozidi 10,000,000 Tsh kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa, na yasiyozidi 20,000,000 Tsh kwa zabuni za ujenzi (Minor Procurement), Manunuzi yote yasiyozidi 5,000,000 Tsh kwa matumizi ya kawaida (Micro Procurement). Pia nilibaini kuwa uhakiki wa kuzingatiwa vigezo vya zabuni, uidhinishaji wa zabuni unaofanywa na bodi ya zabuni, na uanzishaji wa maombi ya vifaa, huduma, au ujenzi ili mchakato wa manunuzi ufanyike (user requisition) havifanyiki kwenye mfumo.

Maoni yangu ni kuwa, endapo shughuli nilizozibainisha zitafanywa katika mfumo bila kuhitaji utashi wa watendaji, zitaongeza ufanisi wa mfumo na kupunguza makosa ya kibinadamu katika mchakato wa zabuni.

Ingawa sheria inaruhusu zabuni zenye vigezo vilivyotajwa kufanyika nje ya mfumo, Maoni yangu ni kuwa, zabuni hizi zikifanyika ndani ya mfumo zitaongeza uwezo wa PPRA katika kufuatilia na kupima kiwango cha uzingatiaji wa masharti ya manunuzi katika taasisi za serikali.

Ninapendekeza PPRA kuchukuwa hatua zifuatazo:

- (a) Kuboresha mfumo ili Manunuzi yenye thamani isiyozidi 10,000,000 Tsh kwa ajili ya manunuzi ya bidhaa , na yasiyozidi 20,000,000 Tsh kwa zabuni za ujenzi (Minor Procurement), Manunuzi yote yasiyozidi 5,000,000 Tsh kwa matumizi ya kawaida (Micro Procurement) yanafanyika ndani ya mfumo.

(b) Kuchambua na kuuboresha mfumo ili uhakiki wa kuzingatiwa vigezo vya zabuni, uidhinishaji wa zabuni unaofanywa na bodi ya zabuni, na uanzishaji wa maombi ya vifaa, huduma, au ujenzi ili mchakato wa manunuzi ufanyike (user requisition) vifanyike kwenye mfumo.

b) Udhibiti dhaifu katika kuhakiki taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo

Msimbo wa bidhaa na huduma unaotambuliwa na Umoja wa Mataifa (UNSPSC) ni utaratibu unaotofautisha bidhaa katika mpango wa manunuzi wa mwaka. Vilevile bei ya zabuni ni moja ya taarifa muhimu katika uchambuzi wa zabuni.

Nimefanya mapitio ya udhibiti katika uhakiki wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo na kubaini yafuatayo: -

- Mfumo hauna udhibiti wa kutosha katika kuhakiki msimbo wa bidhaa na huduma (UNSPSC)
- Mfumo hauzuii taarifa ambazo si tarakimu au sifuri kuingizwa katika uwanja wa kuingiza gharama ya zabuni.
- Mfumo hauhakiki ulinganifu wa kiwango cha fedha kilichowekwa wakati wa kutengeneza zabuni, dhidi ya kiwango cha fedha kadiriwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka.

Maoni yangu ni kuwa, ukosefu wa uhakiki wa kutosha kwenye taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo hususani msimbo wa bidhaa na huduma (UNSPSC) na gharama ya zabuni kunaweza kusababisha taarifa kutokamilika na kutokuwa sahihi.

Ninapendekeza uongozi wa PPRA

(a) kuweka uhakiki wa kutosha na sahihi wa taarifa zinazolingizwa kwenye mfumo ikiwemo msimbo wa bidhaa na huduma na gharama za zabuni wakati wa mchakato wa maombi ya zabuni.

(b) Pia mfumo uboreshwe ili kuhakikisha kuwa unahakiki ulinganifu wa kiwango cha fedha kilichowekwa wakati wa kutengeneza

zabuni, dhidi ya kiwango cha fedha kadiriwa kwenye mpango wa manunuzi wa mwaka.

c) Kutokuwapo kwa mlandano baina ya mbinu za kizabuni na hatua za mchakato wa zabuni

Mfumo wa Manunuzi (TANePS) unaruhusu mbinu mbili za kizabuni ambazo ni: Tathmini ya awali, na mwaliko wa zabuni. Katika tathmini ya awali, taasisi inayotaka kufanya manunuzi inachagua na kuorodhesha wazabuni katika hatua ya kwanza, na kisha kutoa mwaliko kwa wazabuni waliochaguliwa. Kwa upande mwingine, katika mwaliko wa zabuni, taasisi inayotaka kufanya manunuzi huandaa tangazo la zabuni ili wazabuni waweze kuwasilisha bei za huduma kulingana na matakwa ya zabuni. Hii ina maana mbinu ya tathmini ya awali inahitaji hatua mbili ili kukamilika na mbinu ya mwaliko wa zabuni inahitaji hatua moja ili ikamilike.

Nimefanya mapitio ya namna ya kutengeneza zabuni na kubaini kuwa mfumo haumzuii mtumiaji anayetengeneza zabuni kwa kuchagua mbinu ya tathmini ya awali kuweka hatua moja kwenye sahemu inayohitaji taarifa ya hatua za zabuni, na vilevile mfumo haumzuii mtumiaji anayechagua mbinu ya mwaliko wa zabuni kuweka hatua mbili katika sahemu ya kuweka taarifa ya hatua za zabuni.

Maoni yangu ni kuwa, mapungufu niliyobaini yanaweza kudhoofisha ufanisi wa mfumo kwani inapotokea kutolandana kati ya mbinu ya kizabuni na hatua za zabuni, mchakato wa zabuni hauwezi kuendelea mpaka ukwamuliwe.

Ninapendekeza uongozi wa PPRA kuuboresha mfumo ili mfumo wenyewe uweze kutambua hatua za zabuni zitakazohitajika kulingana na mbinu ya kizabuni iliyochaguliwa.

d) Udhaifu wa udhibiti katika mtiririko wa kuandaa zabuni kwenye mfumo

Katika mtiririko wa kuandaa zabuni, taasisi inayofanya manunuzi inaweza kufanya baadhi ya hatua nje au ndani ya mfumo. Hiari ya kufanya baadhi ya hatua za zabuni nje ya mfumo iliwekwa ili kuwezesha kufanya manunuzi ya dharura au manunuzi ambayo taarifa zake ni siri.

Hata hivyo, pia ukaguzi wangu umebaini kuwa mfumo hauna udhibiti wa kuzuia manunuzi ya kawaida kufanyika nje ya mfumo, kwa manunuzi ambayo si ya dharura na hayana usiri yanaweza kuamuliwa baadhi ya hatua kufanyika na mfumo hauna utaratibu wa kuzuia hili.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa udhibiti wa manunuzi yasiyokidhi vigezo vya kidharura, au taarifa zake kuwa siri, kutofanyika nje ya mfumo kunaweza kutumika vibaya kwa taasisi inayofanya manunuzi kuamua kufanya baadhi ya hatua za zabuni nje ya mfumo ili kukwepa udhibiti uliowekwa.

Ninapendekeza uongozi wa Mamlaka ya Manunuzi ya Umma kuboresha mfumo ili kutenganisha uandaaji wa zabuni kwa manunuzi ya kawaida na manunuzi ambayo yana mahitaji ya usiri au dharura. Pia kuweka udhibiti kuzuia kuandaa zabuni za kawaida kwa njia ya dharura

e) Maafisa TEHAMA kufanya majukumu ya kiuendeshaji

Aya ya 11.2 ya Mwongozo wa Kimataifa wa Shirika la Viwango la Kimataifa kuhusu usalama na udhibiti wa mfumo ya taarifa ISO 27002:2013 inaelekeza haki za matumizi ya mfumo zitolewe kwa kuzingatia majukumu ya mtumiaji: Yaani mtumiaji wa mfumo apewe haki za utumiaji ambazo zitamwezesha kutimiza majukumu yake ya msingi tu.

Nimepitia haki walizopewa watumiaji wa mfumo na kubaini kuwa wasimamizi wa mfumo (System Administrators) wana haki za utumiaji zinazowawezesha kuidhinisha usajili wa wazabuni, usajili wa taasisi zinazofanya manunuzi, na kufanya usuluhishi wa malipo.

Maoni yangu ni kuwa, kuidhinisha usajili wa wazabuni, kusajili taasisi zinazofanya manunuzi, na kufanya usuluhishi wa malipo ni kinyume na majukumu na wajibu wa wasimamizi wa mfumo kwa mujibu wa Ikama ya wafanyakazi kwa watumishi wa PPRA. Pia Maoni yangu ni kuwa, kitendo cha wasimamizi wa mfumo kufanya majukumu ya watumishi wa idara tendaji ni kiyume na utaratibu wa mgawanyo wa majukumu na pia huenda ikasababisha Mamlaka ikashindwa kuwawajibisha watumishi watakaofanya makosa kwa bahati mbaya au kwa kukusudia.

Ninapendekeza uongozi wa Mamlaka ya manunuzi (PPRA) kuwaondolea haki za kuidhinisha kusajili wazabuni, usajili wa taasisi zinazofanya manunuzi, na kufanya usuluhishi wa malipo walizopewa

wasimamizi wa mfumo, Aidha Menejimenti ihakikishe kuwa haki wanazopewa watumiaji wa mfumo zinazingatia mgawanyo wa majukumu na kuzingatia majukumu ya watumishi.

3.3 UDHAIFU KATIKA MIFUMO YA BAJETI

Katika mwaka wa fedha 2019/20 nimekagua ufanisi wa udhibiti katika mifumo miwili ya bajeti ambayo ni; 'Budget Portal' unaotumiwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, na 'Central Budget Management System' (CBMS) unaotumiwa na Wizara, Idara, na Mamlaka za Serikali unaosimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango. Ukaguzi wangu umebaini mapungufu ya udhibiti katika uidhinishaji wa ukomo wa bajeti, maafisa masuuli kushindwa kuidhinisha bajeti ndani ya mfumo, mfumo kushindwa kuwezesha uidhinishaji wa kuhamisha vifungu vya bajeti kufanyika ndani ya mfumo, na kufeli kwa taratibu za udhibiti wa bajeti.

3.3.1 Udhaifu wa udhibiti katika mfumo wa CBMS

- a) **Kukosekana kwa udhibiti katika kuzuia uwasilishaji wa bajeti zilizozidi ukomo wa bajeti.**

Kifungu cha 5 cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, kinataka Mpango na Bajeti ubainishe malengo ya bajeti kwa kuzingatia vigezo ikiwemo kuwepo ukomo wa kibajeti, utakaozuia mapungufu katika masuala ya fedha ikiwemo mikopo. Vilevile mwongozo wa uandaaji wa mpango na bajeti unaitaka Wizara ya Fedha na Mipango, itoe ukomo wa bajeti kwa kila kifungu ili kutoa mwongozo katika kuandaa makadirio ya bajeti. Maafisa masuuli wanatakiwa kufuata kiwango cha ukomo kilichoidhinishwa kwa ajili ya kupanga matumizi ya rasilimali kwa mujibu wa vipaumbele vya taasisi.

Nilifanya majaribio katika mfumo wa CBMS ili kuhakiki ufanisi wa udhibiti wa ukomo wa bajeti, niliweka ukomo katika fungu la 45 kisha nikatuma kiwango cha bajeti ambacho kilizidi ukomo nilioweke. Katika jaribio hili nilibaini kuwa mfumo ulikubali kupokea kiwango cha bajeti kilichotumwa. Vilevile niliangalia taarifa za bajeti zilizoidhinishwa kutoka kwenye mfumo, nikabaini bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam, ni kubwa kuliko kiwango cha ukomo wa bajeti kilichowekwa.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa udhibiti katika kuhakiki kiwango cha bajeti kilichowasilishwa dhidi ya ukomo wa bajeti kunasababisha taasisi kufanya matumizi zaidi ya kiwango kilichoidhinishwa na Bunge.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuboresha mfumo wa Bajeti ili kuhakikisha kiwango cha bajeti zinazowasilishwa na taasisi na idara za serikali zinahakikiwa dhidi ya ukomo wa bajeti uliowekwa.

b) Kukosekana kwa uidhinishaji wa bajeti ndani ya mfumo.

Kifungu cha 21-(1) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, kinazitaka taasisi za Umma kuandaa makadirio ya bajeti na kuyawasilisha kwa Katibu Mkuu kwa ajili ya uchambuzi na idhini kwa mujibu wa Sheria hii, pia kwa ajili ya kupokea fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kuzingatia bajeti iliyoidhinishwa. Pia kifungu 17-(1)(a) cha Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, kinawataka maafisa masuuli kuhakikisha kuwa mafungu ya bajeti na taasisi za umma zinaandaliwa kwa mujibu wa miongozo yake, na Miongozo ya Bajeti.

Kinyume na matakwa na sheria, mapitio yangu ya mfumo wa CBMS yamebaini kuwa mfumo haumuwezeshi afisa masuuli kupitia na kuidhinisha bajeti ndani ya mfumo kabla ya kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Hazina. Kwa hali ilivyo sasa afisa bajeti ndiye huwasilisha bajeti bila uhakiki na uidhinishaji wa afisa masuuli ndani ya mfumo.

Maoni yangu ni kuwa, mfumo kushindwa kuwezesha maafisa masuuli kupitia na kuidhinisha bajeti kabla ya kuziwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Hazina kunatokana na udhaifu katika wakati wa kuandaa mahitaji ya mfumo.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa uhakiki na uidhinishwaji wa bajeti ndani ya mfumo kunaweza kusababisha makosa ya makusudi au bahati mbaya. Pia mapungufu haya yanaweza kusababisha uwajibishwaji kwa afisa masuuli endapo kutatokea makosa katika mfumo.

Ninapendekeza Wizara ya Fedha na Mipango kuboresha mfumo wa Bajeti ili kuwawezesha Maafisa Masuuli kuhakiki na kuidhinisha bajeti ndani ya mfumo kabla ya kuwasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango.

3.3.2 Mapungufu ya udhibiti katika mfumo wa budget portal

Nimekagua mfumo wa bajeti wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro ili kupima ufanisi katika udhibiti wa bajeti kwenye mfumo na kubaini mapungufu yafuatayo:

- Kukosekana kwa uhakiki wa idara husika katika uhamishaji wa vifungu vya bajeti, ambapo idara ya mipango inafanya uhamishaji huo kulingana na uidhinishwaji ambao hufanyika nje ya mfumo. Uhamishaji wa vifungu vya bajeti ndani ya mfumo unafanyika bila kuhusisha idara ambayo vifungu vyake vinahamishwa, hii inaweza kusababisha kuhamisha vifungu vya idara husika kimakosa.
- Kutokuwapo kwa udhibiti wa bajeti, nilipitia taarifa ya mchanganuo wa vifungu na kubaini kuwapo kwa bakaa hasi kwenye baadhi ya vifungu vya bajeti. Hii inaashiria kuwa matumizi katika vifungu husika yalikuwa makubwa kuliko bajeti na fedha zilizopangwa.
- Mfumo haukokotoi kwa usahihi fedha na bakaa za bajeti, kitendo kinachoweza kuwapotosha watumiaji wa taarifa za bajeti.

Ninahusisha mapungufu niliyobaini na kutofanyika kwa uchambuzi wa kina katika kutambua mahitaji wa udhibiti wakati wa kutengeneza mfumo.

Maoni yangu ni kuwa, mapungufu yaliyobainishwa yanaweza kusababisha upotoshaji wa taarifa ambao utasababisha makosa katika taarifa za fedha.

Ninapendekeza Menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, ifanye mambo yafuatayo; -

- (a) Iboreshe mfumo wa Budget Portal ili idara ziweze kuhakiki na kuidhinisha uhamishaji wa vifungu vya bajeti ndani ya mfumo.**
- (b) Ichunguze sababu za mfumo kushindwa kuwa na udhibiti madhubuti wa kuzuia matumizi kuwa makubwa kuliko fedha zilizotengwa.**
- (c) Iboreshe mfumo ili uweze kutoa taarifa sahihi za bakaa za fedha.**

3.4 UDHAIFU WA UDHIBITI KATIKA MIFUMO YA MAPATO NA KODI

Ukaguzi wangu wa mwaka wa fedha 2019/2020, nilifanya tathimini ya umadhubuti wa udhibiti katika mifumo ya kukusanya kodi na mapato. Tathimini yangu ililenga katika kuhakikisha ufanisi wa makusanyo na taarifa za mapato. Tathimini yangu ilibaini yafuatayo;

3.4.1 Mfumo wa makusanyo ya mapato ya serikali za mitaa (LGRCIS)

LGRCIS ni mfumo ambao hutumiwa kukusanya mapato ya vyanzo vya ndani vya Serikali za Mitaa. Mapato hukusanywa kupitia vifaa vya Point of Sale (POS) walivyopewa wakusanya mapato wa vyanzo husika vya mapato. Vifaa hivi vimeunganishwa na Mfumo wa Ukusanyaji Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) na vimesanidiwa ili kusawazisha miamala ya mapato na mfumo wa LGRCIS kwa wakati halisi. Watoza ushuru wanatakiwa mara kwa mara kuomba bili kutoka kwa wahasibu wa mapato kulingana na pesa zilizokusanywa na kupelekwa benki.

Ukaguzi wangu wa mfumo huu wa LGRCIS uliotathmini ufanisi wa matumizi na udhibiti wa usalama ili kupata uhakika kuhusu ukamilifu na usahihi wa mapato ya Serikali za Mitaa ulibaini udhaifu ufuatao;

a) Mfumo kutokokotoa ushuru wa huduma, ada za vibali vya ujenzi na adhabu za kuchelewa kulipa ada

Ukaguzi wangu wa mfumo wa LGRCIS uliofanyika ili kukagua ufanisi wa ukusanyaji wa ushuru, malipo ya ada za vibali vya ujenzi na adhabu iliyotokana na kuchelewa kulipia upya leseni za biashara, uligundua kuwa tathimini ya ushuru, hesabu ya ada za vibali vya ujenzi na uamuzi wa adhabu hufanywa kwa mikono nje ya mfumo. LGRCIS hauna uwezo wa kufanya hesabu kiatomati kulingana na vigezo vinavyohitajika kwa vyanzo vya mapato vilivyotajwa.

Maoni yangu ni kuwa, udhaifu niliougundua umesababishwa na kushindwa kutambua vidhibiti muhimu, na kushindwa kutambua mahitaji muhimu ya mtumiaji wa mfumo.

Jambo hili limesababishwa na ukokotozi unaofanyika nje ya mfumo, jambo ambalo linakabiliwa na makosa yaliyokusudiwa na yasiyokusudiwa ambayo yanaweza kusababisha upotevu wa mapato.

Ninapendekeza PO-RALG kukokotoa hesabu za ushuru (service levy), ada za vibali vya ujenzi na adhabu za kuchelewesha leseni za biashara kiotomatiki kwenye mfumo wa LGRCIS.

b) Mfumo kuwa na kumbukumbu zisizo sahihi za kiwango cha fedha zilizopelekwa benki na wakusanya mapato

Wakati wa ukaguzi wangu wa udhibiti wa matumizi ya mfumo wa LGRCIS, nilifanya mapitio kwenye mfumo ili kupima ufanisi wa mfumo wakati wa kuwamua kiwango ambacho hakijapelekwa benki. Katika ukaguzi wangu nilitumia historia ya mpito ya mkusanya mapato katika Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa. Nilitoa ripoti za mkusanyaji mapato mwenye kitambulisho cha mlipaji 308600000330: Mapato yaliyokusanywa kutoka kwenye vyanzo mbalimbali, historia ya malipo na orodha ya wanaokiuka (defaulters). Kutoka kwenye ripoti hizo ilibainika kuwa kufikia tarehe 7 Agosti, 2020 wakati nilipotoa ripoti kwenye mfumo mkusanyaji wa mapato alikusanya jumla ya Sh. 186,342,100.00 na kuweka benki jumla ya Sh. 111,727,353.00 na kusababisha kiasi kisichokuwa benki (unbanked figure) cha Sh. 74,614,747.00. Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti ya wanaokiuka (defaulter) kutoka kwenye mfumo, mkusanyaji huyu wa mapato alikuwa na kiasi kisicho benki (unbanked amount) cha Sh. 78,982,847.00 ambacho ni Sh. 4,368,100.00 zaidi ya kiwango halisi kisicho benki.

Nina maoni kwamba, hii inasababishwa na upimaji duni wa mfumo wakati wa muundo na wakati wa kutengeneza mfumo.

Nina wasiwasi kwamba, udhaifu huu unasababisha kupatikana kwa wakiukaji wasio sahihi (unrealistic defaulters) na ripoti za mapato zisizo sahihi.

Ninapendekeza TAMISEMI kuimarisha mfumo huu ili uripoti takwimu halisi za kiwango cha fedha ambazo hazijapelekwa benki.

c) Kutolingana kwa muda wa leseni ya biashara ilivyo kwenye mfumo wa LGRCIS na kanuni za leseni ya biashara

Mapitio yangu ya mchakato wa kusajili na kusasisha leseni ya biashara kwenye mfumo wa LGRCIS ulibaini kuwa mfumo umesanidiwa kama vile leseni za biashara zinamalizika mwishoni mwa mwaka wa fedha 30 Juni. Hata hivyo, kanuni za leseni ya biashara zinahitaji leseni ya biashara

kuisha mwaka mmoja tangu tarehe ya usajili bila kufuata mwaka wa kifedha. Ada ya leseni ya biashara hulipwa kila mwaka kwa hivyo kila Juni 30 mfumo hutambua mapato kutoka kwenye ada itakayolipwa baada ya kumalizika kwa leseni na kusababisha mapato yasiyo sahihi.

Maoni yangu ni kuwa, jambo hili limesababishwa na kucheleweshwa kwa uboreshaji wa mfumo ili kuendana na kanuni mpya za leseni ya biashara.

Nina wasiwasi kwamba, jambo hili linasababisha kutambuliwa kwa mapato kamili kwa leseni zote, badala ya sehemu ya mapato kwa leseni ambazo muda wake utaisha tarehe 30 Juni pekee.

Ninapendekeza kwa Manajimenti ya TAMISEMI kuhakikisha mfumo wa LGRCIS umeimarishwa ili kuendana na kanuni mpya za leseni ya biashara.

d) Vifaa vya POS vilivyosajiliwa bila kuwa na miamala tangu usajili wake

Kifaa cha POS hutolewa na kusanidiwa kwa ombi maalumu wakati kikiwa kinahitajika tu, Hivyo basi, vifaa vyote vya POS vilivyotolewa na vilivyosanidiwa havipaswi kukaa bila kutumika. Badala yake vinapaswa kutumika kufanya miamala, na kisha kutuma miamala hiyo katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS).

Mapitio yangu ya orodha ya vifaa vya POS vilivyosajiliwa katika manispaa ya Ilala yalibainisha kuwapo kwa vifaa 14 vya POS ambavyo havikuwa na miamala (havikufanya miamala) yoyote tangu usajili wake. Hata hivyo, vifaa hivi vya POS havikuwepo katika orodha ya vifaa vilivyopotea na wala vifaa vyenye kasoro, kwa hivyo, vilikuwa vikifanya kazi na vinatumika.

Ni maoni yangu kwamba, vifaa hivi vya POS vinaweza kutumiwa kukusanya mapato bila miamala kupelekwa/kuunganishwa na mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS) na kusababisha upotezaji wa mapato. Jedwali 4 ni orodha ya vifaa vya POS vilivyosajiliwa bila kuwa na miamala tangu usajili wake.

Jedwali Na. 2: Vifaa vya POS vilivyosajiliwa bila kuwa na miamala tangu usajili wake.

S/N	Nambari ya Kifaa	IMEA	Nambari ya Kifaa chanzo
1	269	352482033267497	Soko la Ilala
2	272	352482033267588	Soko la Ilala
3	603	355554100090700	AIFOLA PRIME TRADERS LTD
4	680	355554100579389	SATEK TRADING CO. ILALA
5	142	355615077262877	Soko la Ilala
6	258	357213087892145	Anatoglo
7	81	357784041278977	Taka Buguruni
8	136	357784041279678	SHERIA
9	691	357903100279961	GREEN WASTE PRO LTD
10	688	357903100741424	GREEN WASTE PRO LTD
11	159	358264072982127	Gerezani Ward Ilala
12	433	358765080708783	M.P. ENVIRONMENT CO.LTD
13	678	865709040143844	Mazingira
14	161	869661020224563	Gerezani Ward Ilala

Chanzo: Orodha ya POS zilizosajiliwa na ripoti za miamala ya POS

Mtazamo wangu NI kwamba kukosekana kwa mapato ya vifaa hivyo kunasababishwa na ukosefu wa ufuatiliaji wa mara kwa mara wa vifaa vya POS.

Maoni yangu ni kuwa, kuna uwezekano kwamba vifaa hivi vya POS hutumiwa kukusanya mapato bila halmashauri kujua kwa kuwa POS hizo hazitumi miamala kwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRSIS) hivyo kusababisha upotezaji wa mapato.

Ninapendekeza OR - TAMISEMI:

- (a) Itambue vifaa vya POS vilivyosajiliwa ambavyo vimekuwa havifanyi kazi (havifanyi miamala) kwa Halmashauri zote.
- (b) Iulize maelezo kutoka kwa Halmashauri ambazo zina vifaa hivyo vya POS na kuchunguza ili kuhakikisha kuwa hakuna upotezaji wa mapato.
- e) Mapungufu ya kiutendaji ya mfumo (“System bugs”) ambayo hupelekea watumiaji kuingizwa kwenye halmashauri tofauti na ile iliyopo wakati wa kuingia katika mfumo

Katika mahojiano yangu na wahasibu wa mapato nilibaini kuwa mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS) unaelekeza/hamisha/peleka watumiaji wa mfumo huo kwa halmashauri tofauti na ile iliyokusudiwa mara baada ya kuingia kwenye mfumo. Wakati wa ukaguzi wa halmashauri ya Bariadi mhasibu wa mapato alielezea kuwa hii ilitokea mara mbili kwake, mara ya kwanza hakugundua kuwa alikuwa ameingia katika halmashauri nyingine tofauti na Bariadi, matokeo yake alitengeneza muamala wa malipo kwa Halmashauri tofauti na ile aliyoikusudia na baadaye hakuweza kuuona muamala huo, hii inamaanisha kuwa muamala uliotengenezwa uliingizwa na kuhifadhiwa katika halmashauri tofauti, halmashauri ambayo alielekezwa/pelekwa.

Kuhusu uchunguzi na PO-TAMISEMI, ilibainika kuwa hii inasababishwa na makosa ya kiutendaji ya mfumo ambapo usimamizi wa kudhibiti na utambuzi wa mtu husika katika mahala husika kwa muda husika (session management) katika mfumo haufanyi kazi vizuri wakati wa wimbi kubwa la utumiaji mfumo.

Hii imesababisha miamala ambayo haitambuliwi na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwani wakati mtumiaji anaelekezwa/anahamishiwa kwa halmashauri tofauti. Miamala yote inayofanyika, itaandikwa na kuhifadhiwa katika kitabu cha fedha cha halmashauri nyingine aliyoelekezwa.

Ninapendekeza PO-TAMISEMI kurekebisha shida na kupata suluhisho la kudumu la makosa ya kiutendaji ya mfumo hususani kuhusu usimamizi wa kudhibiti na utambuzi wa mtu husika katika mahala husika kwa muda husika katika mfumo.

f) Mfumo kushindwa kuhifadhi historia ya miamala kwa vifaa vya POS vilivyopotea na vyenye kasoro

Kila POS lazima isajiliwe na kusanidiwa kwenye mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS) kabla ya kutumika. Maelezo yafuatayo yanahifadhiwa wakati wa usajili wa POS: Nambari ya IMEI na nambari ya kifaa ambayo ni nambari ya kipekee iliyopewa kifaa cha PoS. Wakati mkusanya mapato anapewa mashine ya POS, IMEI na nambari ya kifaa huwa imeunganishwa na nambari ya mlipaji, ambayo ni nambari ya kitambulisho ya kipekee anayopewa kila mkusanyaji mapato

aliyeidhinishwa. Nambari ya IMEI hutumiwa kutambua miamala yote iliyofanywa na kifaa cha POS tangu usajili wake, wakati nambari ya mlipaji inahifadhi kumbukumbu za miamala iliyofanywa na kila mkusanya mapato na historia ya malipo.

Mapitio yangu ya ripoti za ukusanyaji za POS za mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS) nilibaini kuwa endapo halmashauri itatumia nambari ya kifaa cha POS kilichopotea au chenye kasoro wakati wa usajili wa kifaa kipya cha POS, mfumo hubadilisha nambari ya IMEI ya kifaa kipya cha POS kwa nambari ya IMEI ya kifaa cha POS kilichopotea au chenye kasoro. Hii inapelekea kuhamisha rekodi zote za manunuzi kutoka katika kifaa cha POS kilichopotea au kibovu kwenda kwenye kifaa kipya kilichosajiliwa cha POS. Uchunguzi wangu zaidi uligundua kuwa mfumo unabadilisha nambari ya mlipaji ya mkusanya mapato wa POS iliyopotea au yenye kasoro kuwa nambari ya mlipaji ya mkusanya mapato wa POS mpya iliyosajiliwa. Kuhamisha miamala inamaanisha kuwa miamala yote ambayo haijapelekwa benki ya mkusanya mapato wa POS iliyopotea au yenye kasoro huhamishiwa kwa mkusanya mapato wa POS mpya iliyosajiliwa.

Kwa mfano, nilibaini kifaa cha POS kilichoripotiwa kuwa kimepotea chenye nambari ya kifaa 229 ambayo hapo awali ilitumiwa na mkusanyaji mapato mwenye nambari ya mlipaji 201900827198. Baada ya ripoti ya upotezaji wa kifaa cha POS, halmashauri iliipatia nambari ya kifaa '229' kwa kifaa kingine chenye nambari ya IMEI 359183093016484 inayotumiwa na mkusanyaji mapato mwenye namba ya mlipaji 2019 20191818976. Historia ya miamala ya mkusanyaji mapato wa zamani ilihamishiwa kwa mkusanyaji mpya bila kuacha kumbukumbu za miamala ya mkusanyaji wa mapato wa zamani.

Ni maoni yangu kwamba mapungufu yaliyobainika husababisha upotezaji wa kifaa cha POS na historia ya miamala ya mkusanyaji wa mapato na uhamisho usiofaa/wa kiholela wa historia ya malipo na miamala isiyolipwa (“unbanked transaction”) kwa wakusanyaji wa mapato wengine.

Ninapendekeza PO-TAMISEMI kuimarisha mfumo kuzuia matumizi ya nambari ya kifaa iliyotumika kabla ili kuhifadhi miamala na historia ya malipo ya kifaa cha POS na mkusanya mapato.

g) Maafisa wa TEHAMA hubadilisha nywila za wahasibu wa mapato na kuzitumia kufanya marekebisho

Katika mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS) marekebisho hufanywa ikiwa kuna makosa katika miamala ya ukusanyaji wa pesa ilitumwa na mkusanyaji mapato, marekebisho hayo yanaweza kupunguza au kuongeza kiwango cha fedha kilichokusanywa bila kuwasilishwa benki cha mkusanya mapato.

Nilikagua marekebisho ya miamala ya Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi na kubainisha kesi ambazo marekebisho yalianzishwa na kuidhinishwa na mtu huyohuyo mmoja. Wakati wa mahojiano yangu na wahasibu wa mapato na maafisa wa biashara ambao walihusika katika kesi zilizoainishwa za kuanzisha na kuidhinisha marekebisho niliarifiwa kuwa hawajui marekebisho haya, waliniambia zaidi kuwa wakati marekebisho haya yalipokuwa yanapitishwa hawakuwa ofisini, walinijulisha zaidi kuwa kulikuwa kuna kipindi ambapo hawakuweza/walishindwa kuingia kwenye mfumo ilihali/japokuwa walikuwa wanatumia nywila sahihi.

Mapitio yangu zaidi ya njia za ukaguzi (audit tail) kwa maafisa wa TEHAMA wa halmashauri, nilibaini kuwa afisa mmoja wa TEHAMA alihusika katika kubadilisha nywila za akaunti ya afisa wa mapato na biashara kisha kutumia nywila hiyo kurekebisha miamala.

Maoni yangu ni kuwa, matukio yaliyotajwa yanasababishwa na ukosefu wa udhibiti wa kutosha katika utayarishaji wa akaunti za watumiaji wa mfumo, na usimamizi wa ufikiaji/utumiaji wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo. Maafisa wa TEHAMA wa Halmashauri wamepeva mamlaka na vipaumbele/upendeleo katika utayarishaji wa akaunti za watumiaji wa mfumo na usimamizi wa haki za ufikiaji/utumiaji wa mfumo bila udhibiti na kusimamiwa ipasavyo

Ninapendekeza PO-TAMISEMI kuanzisha udhibiti katika uandaaji wa akaunti za watumiaji na usimamizi wa haki za ufikiaji wa mfumo kama vile uandaaji wa akaunti za watumiaji au kubadilisha hati/nywila za akaunti lazima iombwe rasmi na kupitishwa na wakuu wa vitengo husika. Kwa kuongeza, inapaswa pia kuwapo kwa uhakiki wa mara kwa mara wa akaunti za watumiaji wenye upendeleo/vipaumbele maalumu.

h) Kutozingatia mgawanyo wa majukumu na kipaumbele/upendeleo mdogo katika kuanzisha na kuidhinisha marekebisho

Katika ukaguzi wangu wa marekebisho ya miamala katika Halmashauri mbalimbali, nilibaini ukosefu wa mgawanyo wa majukumu ambapo nilibaini kuwa marekebisho huanzishwa na kuidhinishwa na mtu huyohuyo mmoja. Pia, niliona kwamba maafisa wa TEHAMA na wakaguzi wa ndani hufanya marekebisho katika mfumo, marekebisho hayo hukiuka kanuni za kipaumbele/upendeleo mdogo ambao unataka watumiaji kupaswa kuwa na haki za chini za ufikiaji mfumo na kufanya vitendo kulingana na majukumu yao.

Maoni yangu ni kuwa, hili linatokana na udhibiti duni katika kutoa haki za ufikiaji wa mfumo kwa watumiaji, Na pia ni maoni yangu kwamba hii inaweza kusababisha ulaghai na upotezaji wa mapato.

Ninapendekeza PO-TAMISEMI:

- (a) Kutekeleza udhibiti wa kuzuia katika mfumo ili mtumiaji aziweze kuidhinisha marekebisho ambayo ameyaanzisha yeye mwenyewe**
- (b) kufanya mapitio ya mara kwa mara kwa haki za ufikiaji wa mfumo kwa mtumiaji ili kuhakikisha kila mtumiaji ana haki sahihi za kuufikia mfumo kulingana na majukumu ya utendaji wake.**

i) Uchezeshaji/Ubadilishaji wa tarehe ya kifaa cha POS kwa wakusanya mapato

Wakati wa ukaguzi ilibainika kuwa wakusanyaji mapato walikuwa wakibadilisha tarehe za vifaa vya POS kuwa tarehe za mbele au za nyuma kuliko tarehe husika ya sasa ili kuzuia kifaa kukamata tarehe ya sasa kama tarehe ya miamala. Hii inapelekea miamala ya POS kuwa na tarehe tofauti kutoka tarehe ilipochukuliwa miamala hiyo, kwa sababu hiyo mfumo wa ukusanyaji wa mapato wa serikali za mitaa (LGRCIS) unapokea miamala ambayo ina tarehe za mbele au za nyuma kuliko tarehe ya sasa au mwaka halisi wa fedha.

Maoni yangu ni kuwa, uwezo huu wa kubadilisha tarehe unasababishwa na ukosefu wa vizuizi bora katika kupata nafasi ya kusanidi POS na mfumo kutumia tarehe ya POS badala ya tarehe ya sasa ya seva inayoshikilia/hifadhi mfumo.

Hii imesababisha upotoshaji wa miamala yenye tarehe za mbele au za nyuma, kwani mwaka wa sasa wa fedha hauonekani katika miamala ya mkusanya mapato ambayo hazijafikishwa benki (ripoti ya wadaiwa). Hii ni kwa sababu mfumo unazalisha ripoti katika kipindi cha mwaka wa fedha uliopo. Hivyo, kusababisha kuwapo kwa ripoti zisizo za kweli za wadaiwa.

Ninapendekeza ofisi ya raisi TAMISEMI:

- (a) Kuzuia upatikanaji wa usanidi wa POS**
- (b) Kutumia tarehe ya seva inayohifadhi mfumo kama tarehe ya miamala badala ya tarehe ya kifaa cha POS.**
- j) Wakusanya mapato wenye nambari za Utambulisho zaidi ya moja.**

Katika mapitio yangu ya utendaji kazi wa mfumo wa LGRCIS na utumiaji wa vifaa vya POS nilibaini kuwa wapo wakusanya mapato ambao wanapopewa kifaa cha POS wanahitaji kuwa na nambari ya utambulisho ya kipekee (payer ID) ambayo hutumiwa kutambua miamala inayokuwa imefanywa na mkusanya mapato husika kwani kifaa kimoja cha POS kinaweza kutumiwa na mkusanya mapato zaidi ya mmoja. Wakati wa usajili na usanidi wa kifaa cha POS mkusanya mapato anapewa nambari ya utambulisho “payer ID” ambayo inahusianishwa na POS yake. Hata hivyo, katika ukaguzi wangu wa miamala ya POS nilibaini kuwapo kwa wakusanya mapato wenye nambari za utambulisho zaidi ya moja, kwa sababu hiyo husababisha ugumu katika kufuatilia miamala na uwekaji wa pesa katika benki kwani mkusanya mapato anaweza kuweka pesa katika benki kwa kutumia nambari ya utambulisho ambayo ni tofauti na ile aliyotumia wakati wa kukusanya mapato hayo.

Hii inachangiwa na ukosefu wa namna ya kugundua kuwapo kwa nambari zaidi ya moja zilizohusianishwa na mkusanya mapato mmoja wakati wa usajili wao katika mfumo.

Nina wasiwasi kuwa hii inaweza kusababisha kushindwa kutambua walioshindwa kukusanya mapato na ugumu wa kufuatilia makusanyo dhidi ya kiwango kilichowekwa benki na mkusanya mapato husika

Ninapendekeza PO-RALG kuanzisha utaratibu utakaowezesha kuzuia usajili mara mbili wa wakusanya mapato.

k) Makosa ya kibinadamu katika kutuma miamala ya POS yanayopelekea marekebisho yenye shaka.

Katika mapitio yangu ya miamala ya POS niligundua makosa ya kibinadamu, kama vile kutumwa kwa miamala ya aina moja zaidi ya mara moja, Miamala yenye kiwango kisicho cha kweli na wakusanya pesa wanaoingiza nambari zao za utambulisho sehemu ya kuingiza kiasi cha mapato.

Ni maoni yangu kwamba hii imesababishwa na ukosefu wa uthibitishaji wa aina ya taarifa katika POS, mfano, POS inaweza kurekodi muamala lakini ikashindwa kutoa risiti ambapo hupelekea mkusanya mapato kufanya muamala huo huo kwa mara ya pili ili kupata risiti ambapo hupelekea kujirudia kwa miamala. Pia, sababu nyingine ni ukosefu wa mafunzo kwa wakusanya mapato kwani wengi wao hawajapata mafunzo ya kutosha kuhusu utumiaji wa vifaa vya POS.

Hii inahusishwa na hitaji la kurekebisha miamala ambayo hutumiwa kama mwanya wa kupitisha marekebisho ya uwongo yanayosababisha upotevu wa mapato.

Napendekeza PO-RALG kutengeneza udhibiti madhubuti katika uthibitishaji wa aina ya taarifa inayowekwa na mtumiaji katika vifaa vya POS ili kupunguza makosa ya kibinadamu na kuhakikisha mafunzo sahihi kwa wakusanya mapato.

l) Udhaifu wa Usimamizi wa watumiaji mifumo na usimamizi wa mabadiliko ya programu.

Nilikagua taratibu za ufanyaji mabadiliko ya programu na kubainisha kuwa mabadiliko yalitekelezwa katika mfumo bila kuzingatia mwongozo wa Serikali "e-Government standards for development, acquisition, operation, and maintenance of e-Government applications (eGAEXT/APA/005)". Miongozo inahitaji taasisi za umma kurekodi ipasavyo taarifa za maombi, mahitaji, idhini na majaribio ya mabadiliko kabla ya kuyatekeleza. Niligundua kuwa hakukuwa na nyaraka za mabadiliko yaliyotekelezwa. Utekelezaji wa mabadiliko bila kufuata taratibu na nyaraka sahihi kunaweza kusababisha kutokea kwa madhaifu ya kiusalama wa mfumo.

Katika kufanya mapitio yangu zaidi ya udhibiti wa watumiaji wa mfumo nilibaini Matumizi ya akaunti zisizo na majina halisi kuingia kwenye mfumo, na kwenye kanzidata ya mfumo ambayo huondoa uwajibikaji ikiwa itatokea matumizi mabaya ya mfumo. Niligundua pia matumizi ya akaunti yenye upendeleo (priveleged user account) bila utaratibu maalumu, ambapo matokeo yake hutumiwa na maafisa TEHAMA kujisajili wenyewe kwenye mfumo kwa kutumia majina ambayo sio halisi kwa nia ya kufanya uhalifu,

Ni maoni yangu kwamba udhaifu huu umesababishwa na kukosekana kwa utaratibu maalumu wa kusimamia watumiaji wa mfumo kama vile umbaji, uidhinishwaji na uangalizi wa haki kwa watumiaji wa mfumo.

Napendekeza uongozi wa ofisi ya raisi TAMISEMI kufanya yafuatayo:

- (a) Kukagua watumiaji wote wa mfumo na kuondoa akaunti za watumiaji zilizo na majina yasiyo halisi katika PO-RALG na kuzuia akaunti zenye majina yasiyo halisi katika mfumo,**
- (b) Kuweka upya na kubadilisha haki za upendeleo na kuhakikisha kuwa haki mpya zinatunzwa na mkurugenzi wa TEHAMA na mkurugenzi wa Serikali za Mitaa. Inapaswa pia kuhakikisha kuwa matumizi ya akaunti inapohitajika yanaidhinishwa ipasavyo na sababu ya matumizi hayo inawekwa katika nyaraka,**
- (c) Kuandaa, na kutekeleza miongozo ya usajili wa watumiaji na usimamizi wa uingiaji katika mfumo katika ngazi ya mawaziri.**

3.4.2 GoTHOMIS

Kulingana na waraka wa Hazina nambari 3 wa tarehe 4 Septemba 2017, mapato yote ya Serikali yanapaswa kukusanywa kupitia mfumo wa GEPG. Pia kulingana na barua kwa makatibu tawala wa Mikoa ya tarehe 19 Machi 2019 kutoka kwa Katibu Mkuu OR-TAMISEMI kuhusu usalama na utunzaji wa taarifa za mfumo wa menejimenti ya hospitali (GoT-HoMIS) uliagiza maafisa TEHAMA wa halmashauri Kuhakikisha wanachukua nakala ya kanzidata za mfumo wa GoT-HoMJS (Database backup) kila siku baada ya muda wa kazi na kuhifadhi mahali salama kwa ajili ya matumizi itakapotokea hitilafu. Barua hiyo pia inawataka maafisa TEHAMA wa Halmashauri kuhakikisha vifaa vya TEHAMA vinavyotumiwa na mfumo huu vinahifadhiwa mahali salama.

Mfumo wa GoTHOMIS unatumiwa na halmashauri katika utoaji wa huduma za afya katika ngazi ya vituo vya afya, zahanati na hospiatli za wilaya. Ukaguzi wangu wa mfumo wa GOTHOMIS katika Manispaa za Ilala, Temeke, na Lindi, na pia katika halmashauri za miji ya Kibaha na Masasi nilibaini mapungufu yafauatayo:-

- (a) Mfumo kutofungamana (integration) na mfumo wa malipo ya serikali wa GEPG, hivyo mapato yanapokelewa dirishani na mhasibu na kupelekwa benki.
- (b) Udhaifu wa udhibiti (Backup) wa taarifa za mfumo zinahifadhiwa kwenye ofisi ya mfawidhi ambayo ipo kwenye jengo moja na chumba ambacho “server” iliyo na mfumo ipo, hii inapelekea taarifa za kwenye “server” na “backup” ya taarifa hizo kuwa kwenye mazingira ya hatari endapo kutatokea majanga ya asili kama moto.
- (c) kutokuwapo kwa udhibiti wa kuzuia watumiaji wa jengo kuingia kwenye chumba cha “server”, vilevile hakuna udhibiti wa kuhakikisha kila afisa TEHAMA anayeingia kwenye “server” ya mfumo anatambulika ili kuweka uwajibikaji, maafisa wa TEHEMA wanatumia akaunti moja kuingia kwenye mfumo, badala ya kila mmoja kuwa na akaunti kwa jina lake ya kuingia kwenye mfumo.
- (d) Kanzidata ya mfumo kutokuwa na rekodi ya kinachofanywa (audit log) na wanaoingia kwenye kanzidata ambayo ni muhimu kuweka uwajibikaji.
- (e) Hakuna udhibiti wa kuzuia afisa TEHAMA wa Halmashauri kuingia kwenye kanzidata (database) ya mfumo. Kanzidata ya mfumo ipo wazi kwa yoyote mweye ujuzi wa TEHAMA kuweza kuingia na kufanya chochote bila kuzuizi chochote. Afisa TEHAMA wa Halmashauri hahitaji kuingia kwenye kanzidata kwani majukumu yake ni kutoa msaada kwa watumiaji wa mfumo. Majukumu ya afisa TEHAMA yanatakiwa kuishia kwenye kusimamia mfumo wenyewe bila kuingia kwenye kanzidata.
- (f) Usimamizi hafifu wa usalama na utunzaji wa taarifa katika mfumo wa GoTHoMIS, kulingana na barua ya katibu Mkuu Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwenda kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ya tarehe 19 Machi 2019 kuhusu usalama na utunzaji wa taarifa inayoelekeza maafisa

TEHAMA wa Halmashauri kuwasilisha nakala ya ‘database’ ya mfumo kila wiki kwa idara ya TEHAMA Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Ni maoni yangu kuwa mapungufu yaliyobainishwa yanaweza kusababisha ubadhirifu na kusababisha Halmashauri kukosa mapato. Pia inaweza kusababisha Halmashauri kupoteza taarifa za mfumo kama likitokea janga la asili kama moto. Vilevile, matumizi ya akaunti moja ambayo inatumiwa na maafisa TEHAMA kuingia kwenye “server” kunaondoa uwajibikaji endapo itatokea ukiukwaji wa matumizi ya mfumo.

Ninapendekeza Ofisi ya Rais-TAMISEMI:

- (a) Ihakikishe, mfumo wa GoTHoMIS unaunganishwa na mfumo wa malipo ya kieletroniki wa serikali “GEPG”.
- (b) Ihakikishe Halmashauri zinahifadhi “backup” ya taarifa za mfumo zinazohifadhiwa kwenye makao makuu ya Halmashauri na Afisa TEHAMA anaingia kwenye “server” ya mfumo kwa kutumia akaunti yenye jina lake.
- (c) Ihakikishe kuwepo kwa udhibiti wa maafisa kuingia kwenye mfumo, na kanzi data ya mfumo.
- (d) Computer zinazobeba mfumo “Hosting the system”. ziwekwe kwenye maeneo ambayo hayafikiki kwa urahisi na kuwepo na udhibiti wa watu kufika kwenye maeneo hayo.
- (e) Kwa kushirikiana na Uongozi wa Halmashauri inashauriwa kuweka utaratibu madhubuti wa kufuatilia usalama wa mifumo na vifaa vyake vilivyo simikwa kwenye Halmashauri na kufuatilia mara kwa mara uwasilishwaji wa nakala ya ‘database’ kila wiki.
- (f) Kuhakikisha kuwa idara ya TEHAMA inaweka udhibiti katika kanzidata (database) ya mfumo ili kuzuia maafisa TEHAMA kuingia kwenye kanzidata bila utaratibu ikiwa ni pamoja na kuwa na ‘audit log’ na ‘audit trail’ kwenye database ya mfumo.

3.4.3 Mifumo ya usimamizi wa taarifa za ardhi

Katika mwaka huu wa ukaguzi, nilifanya tathmini ya ufanisi wa udhibiti wa matumizi ya mifumo ya taarifa za usimamizi wa ardhi katika Wizara ya

Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Wizara ina mifumo mitatu ya maombi ya kusimamia shughuli za usimamizi wa ardhi: MOLIS ambao unatumika Kigamboni, Temeke, na manispaa ya Ilala, MOLIS v3 ambao hutumiwa katika mikoa mingine nje ya Dar es salaam, na ILMIS ambao unatumika Kinondoni, Ilala, Ubungo, manispaa ya Temeke na Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni nilibaini udhaifu ufuatao:

a) Kukosekana kwa uhusiano kati ya taarifa za wamiliki ardhi na taarifa za ardhi (spatial and non-spatial data) katika mifumo ya MOLIS na MOLIS v3

Kwa mujibu wa mpango mkakati wa wizara wa muda wa kati (2019/20 - 2023/24) sehemu nambari 3.3.4 (Lengo D), inaeleza uhitaji wa kuboresha ufanisi na uwazi katika utoaji wa huduma za usimamizi wa ardhi kwa kutekeleza mifumo wa kompyuta na kuandaa mifumo ya taarifa za ardhi Kitaifa, takwimu za maeneo, miundombinu ya kisasa ya upimaji na uchoraji ramani ambayo ni pamoja na uelekezaji wa kijiografia na mifumo ya upimaji ardhi vilevile kutawanya huduma za ardhi ili kusaidia kuhakikisha utoaji bora wa huduma za usimamizi wa ardhi.

Miundombinu ya taarifa za ardhi za taifa (National Spatial Data Infrastructure) ina jukumu muhimu katika kuratibu juhudi za kukuza mifumo ya taarifa za ardhi na kuunganisha taarifa za ardhi na taarifa za wamiliki wa ardhi.

Mapitio yangu ya mifumo ya MOLIS na MOLIS v3 yalibaini kuwa shughuli na vibali vyote vya ardhi hufanywa kwenye faili linalondikwa kwa mkono nje ya mfumo, taarifa zinapokamilika huingizwa kwenye mifumo kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu. Lakini, taarifa za upimaji, usajili, umiliki, na upangaji hazijaunganishwa katika mfumo. Mapitio yangu ya malalamiko ya ardhi, nilikutana na kisa. Mtu anayeonekana kuingilia eneo la shule ya serikali amesajiliwa kiwanja chake katika mfumo na amekuwa akilipa kodi kama sheria inavyomtaka.

Hali hii inasababishwa na utekelezaji usiofaa wa utaratibu wa utendaji kazi wakati wa kukusanya taarifa za utengenezaji wa mfumo.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa uhusiano wa taarifa za upimaji, usajili, umiliki, na maelezo ya upangaji katika mfumo unaweza kusababisha kasoro zifuatazo:

- Tathmini isiyo sahihi ya kodi ya ardhi kwa kuwa afisa anaingiza taarifa za eneo husika kwenye mfumo ili kutambua kiwango cha kodi ya ardhi kinachopaswa kulipwa. Hii hupelekea kuwa na taarifa zenye makosa ya kibinadamu na makosa ya kukusudia.
- Mfumo uweze kutambua nambari zisizo sahihi za mpango wa upimaji wa ardhi zinazoweza kutambuliwa na mfumo. Nambari hizo zinaweza zikasababisha maeneo yasiyopimwa kusajiliwa, hali hiyo inaweza kusababisha usajili wa maeneo yaliyotengwa, maeneo ya wazi ya umma, na ardhi zilizotengwa tayari.
- Mfumo kutoweza kufuatilia miamala inayohusiana na eneo au kiwanja husika. Miamala kama ya uhamishaji wa umiliki haiwezi kufuatiliwa ikitokea uhamishaji wa umiliki, mfumo hubadilisha taarifa za umiliki wa aali na kuweka taarifa za umiliki mpya bila kuweka kumbukumbu ya historia ya umiliki.

Kukosekana kwa kumbukumbu ya historia ya umiliki wa viwanja vilivyohamishwa kunaweza kusababisha uhamishaji wa umiliki wa ardhi kwa ulaghai na baadaye kusababisha migogoro ya ardhi.

Ninapendekeza uongozi wa wizara ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi, kutekeleza na kuweka udhibiti mbadala wa kuondoa udhaifu wa kimfumo kwa mikoa yote inayotumia MOLIS na MOLIS v3 na kuhakikisha ufanisi katika kuamua upangaji wa ardhi, upigaji picha sahihi ili kuzuia usajili wa matumizi ya ardhi yasiyoruhusiwa na kuboresha ufuatiliaji katika kipindi ambacho uongozi wa wizara uko katika mchakato wa kuimarisha na kusimika mfumo wa ILMIS kote nchini.

b) Udhaifu katika kuhariri malipo na ankara za kodi za ardhi.

Wakati nikifanya mapitio ya mchakato wa malipo ya kodi za ardhi katika mfumo wa MOLIS na MOLIS V3, nilibaini kuwa ankara hupatikana kwa kutengenezwa moja kwa moja na mfumo pamoja na tarehe ya kukamilisha malipo, hivyo mmiliki wa ardhi analazimika kulipia kiwango kilichoaminishwa. Lakini, afisa ardhi anaweza kuhariri maelezo ya ankara na kiasi kuonesha gharama za msamaha wa kodi kwa wazee au kubadilisha malipo ya kodi ya ardhi kwa viwanja ambavyo viko chini ya kituo cha uwekezaji cha Tanzania. Nilikagua mchakato wa uhariri wa ankara na kubaini kuwa mfumo hauna uwezo kuambatanisha nyaraka

zinazoonesha uthibitisho wa gharama za msamaha wa kodi za ardhi pia hakuna uhakiki wa kodi zilizolipwa.

Jambo hili linasababishwa na utekelezaji usiofaa wa utaratibu wa utendaji kazi wakati wa kukusanya taarifa za utengenezaji wa mfumo.

Maoni yangu ni kwamba, kukosekana kwa viambatisho na uhakiki wa kodi zilizohaririwa kwenye mfumo kunaweza kusababisha utumiaji mbaya wa mfumo na kusababisha upotezaji wa mapato ya serikali.

Ninapendekeza uongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhakikisha taarifa zinazowekwa kwenye mfumo zinahakikiwa na pia kuhakikisha mfumo una uwezo wa kuambatanisha nyaraka zinazoonesha uthibitisho wa gharama za msamaha wa kodi za ardhi wakati wa kutengeneza ankara kwenye mfumo wa ILMIS ambao utasimikwa nchi nzima.

c) Mapungufu katika uhakiki wa malipo ya nyuma

Nilifanya mapitio ya utendaji kazi wa mfumo ya MOLIS na ILMIS nilibaini kuwa katika mfumo yote afisa ardhi anatakiwa kuthibitisha malipo ya kodi ya ardhi ya kipindi cha nyuma yaliyofanywa kwa kutumia stakabadhi halisi. Hii ni kwa malipo yaliyofanyika kabla ya kuanza kutumia mfumo wa malipo wa GePG.

Afisa anathibitisha kama malipo ya kodi ya ardhi yalifanywa pindi mmiliki wa ardhi anapowasilisha stakabadhi halali ya malipo ya mwaka husika, hivyo basi afisa ardhi anahitajika kufuta kodi ya ardhi iliyobaki katika mfumo kwa mwaka huo husika ambao stakabadhi imewasilishwa na mmiliki wa ardhi.

Ukaguzi wangu pia ulibaini kuwa wakati wa kufuta deni la kodi ya ardhi pindi statabadhi ya malipo ya nyuma inapowasilishwa, mfumo hukusanya na kujumlisha malipo yote ya miaka iliyopita hadi tarehe ya stakabadhi ya malipo ilipotolewa badala ya kufuta kiwango maalum cha mwaka husika kulingana na stakabadhi hiyo.

Kwa hivyo, endapo afisa hatakuwa makini au atapuuza kiwango kilichopatikana, mfumo hufuta madeni ya miaka ya nyuma hata ambayo stakabadhi za malipo hazijawasilishwa. Katika mapitio hayo pia

iligundulika kuwa hakuna uhakiki unaofanywa ili kuidhinisha malipo ya nyuma.

Udhaifu huu unasababishwa na ufanyaji hafifu wa majaribio ya utendaji kazi wa mfumo.

Maoni yangu ni kwamba mapungufu katika uhakiki wa malipo ya nyuma unaweza kusababisha kufutwa kwa madeni ambayo hayajafanyika kwa hivyo kupoteza mapato ya serikali.

Napendekeza yafuatayo kwa uongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

- **kuimarisha udhibiti kwa kuanzisha utaratibu wa uhakiki wa malipo ya nyuma kwa ofisi ambazo zinatimia mfumo wa MOLIS ili kuhakikisha kuwa kila ankara ina stakabadhi halali na iliyoidhinishwa kwa malipo yaliyofanyika kabla ya kuanza kutimia mfumo wa malipo wa GePG.**
- **Kurekebisha kasoro kwenye mfumo wa ILMIS ili kuzuia malipo ya zamani yasiyoidhinishwa.**

d) Kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu katika shughuli ya usimamizi wa viwanja

Nilikagua mchakato wa shughuli ya usimamizi wa viwanja katika mfumo wa MOLIS v3 na kubaini watumiaji 22 wamepewa haki za utumiaji wa mfumo ambazo zinawawezesha kutengeneza, kutathmini, kusajili, kudhibitisha na kuidhinisha kiwanja kwenye mfumo.

Nimebaini kuwa kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu katika shughuli ya usimamizi wa viwanja (lot management) kunasababishwa na upungufu wa wafanyakazi, ambapo katika mikoa mingine kuna mfanyakazi mmoja tu anayehusika kutekeleza majukumu ya usimamizi wa viwanja kwenye mfumo. Hata hivyo, hakukuwa na mapitio na uhakiki wa shughuli za watumiaji kwenye mfumo.

Kukosekana kwa mgawanyo wa majukumu katika kusajili, kuhakiki na kuidhinisha kiwanja kipya kwenye mfumo kunaweza kusababisha makosa ya kibinadamu ya kukusudia au yasiyokusudiwa ambayo hayawezi kugunduliwa.

Napendekeza uongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kuanzisha udhibiti mbadala kama vile kukagua mara kwa mara shughuli za watumiaji katika mfumo ili kuhakikisha kwamba maafisa wote wa ardhi waliopewa haki ya utumiaji wa mfumo hawatumii vibaya haki zao.

e) Kushughulikia madai yanayohusiana na ardhi nje ya mfumo

Mapitio yangu ya usimamizi wa madai ya ardhi yalibaini kuwa madai yanapokelewa kupitia mfumo wa ofisi mtandao (e-ofisi). Huu ni mfumo wa usimamizi wa faili unaotumika katika usimamizi wa mafaili ya wateja na ya wafanyakazi. Mfumo huu haujaunganishwa na mifumo ya usimamizi wa ardhi yaani MOLIS na ILMIS, hivyo basi afisa hulazimika kusubiri nakala ngumu ya faili kwa ajili ya marejeo na kwa ajili ya kuendelea na kazi ya kushughulikia madai.

Kushughulikia madai yanayohusiana na ardhi nje ya mfumo kunasabishwa na kukosekana kwa moduli ya kushughulikia madai kwenye mifumo ya MOLIS na ILMIS.

Maoni yangu ni kwamba, utaratibu wa kushughulikia madai yanayohusiana na ardhi nje ya mifumo ya usimamizi wa ardhi unaweza kusababisha kuchelewesha utatuzi na kutokuwa na uwezo wa kufuatilia hali ya utatuzi wa madai yaliyowasilishwa.

Napendekeza uongozi wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhakikisha mfumo wa usimamizi wa ardhi unaotumika unakuwa na moduli ya kushughulikia madai yanayohusiana na ardhi na kuiunganisha na mafaili husika yaliyomo kwenye mfumo wa ofisi mtandao (e-ofisi).

3.4.4 MNRT portal

Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT) ilibuni na kutengeneza mfumo uliopewa jina la (MNRT portal) kwa ajili ya kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa wakala na mamlaka zote zilizo chini yake. Mfumo huu ukiwa ni mmoja kati ya mingine, ulilenga kuwa na mfumo mmoja kwa ajili ya mambo ya utalii na maliasili kwa ujumla ili kurahisisha ufuatiliaji na usimamizi wa shughuli na mapato. Katika mwaka uliokaguliwa nilitathmini ufanisi wa udhibiti uliowekwa katika mfumo uitwao (MNRT Portal) na kubaini madhaifu yafuatayo:

a) Udhaifu Katika usimamizi wa vibali vya wageni.

Mapitio yangu ya utoaji wa vibali kwa wageni kuingia Mbugani na katika vitalu vya uwindaji nilibaini kuwa, vibali vinatolewa na waendeshaji wa utalii kupitia mfumo uitwao "MNRT Portal" na malipo hufanywa kwa njia ya kielektroniki kupitia GePG. Wakati wa kuingia, Wageni wanahitajika kuwasilisha vibali vilivyolipiwa kwenye lango la kuingilia katika Hifadhi ya taifa husika. Vivyo hivyo wakati wa kutoka wanapaswa kuwasilisha vibali ili kuchunguzwa kama kuna ukiukwaji wa muda waliokaa mbugani kulingana na tarehe ya malipo ya kibali. Katika kupitia utaratibu wa ufuatiliaji wa wageni, na matumizi ya vibali nilibaini yafuatayo:

- **Kutokuwapo kwa lango la kuingia na lango la kutoka ndani ya hifadhi au vivutio vilivyo chini ya TAWA**

Kutowasilisha vibali wakati wa kuingia au kutoka nje ya hifadhi kumesababisha vibali kuonekana havijatumika wakati tayari vimetumika (paid but unutilized). Hali hii imesababisha kushindwa kukusanya mapato kwa watalii waliokaa mbugani zaidi ya muda waliolipia.

- Mapungufu yaliyobainika kwa kuangalia vibali vilivyotolewa kwa watalii mbalimbali kati ya tarehe 1 Januari, 2020 na tarehe 29 Septemba, 2020 ni kama ifuatavyo:
- **Vibali 223 vilivyo tolewa kwa watalii katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere vinaonyesha kuwa vimekwishalipiwa na havijatumika bado**, Wakati wa uchunguzi, niliarifiwa kuwa vibali vingi kati ya hivyo vilikuwa vimeshatumika ingawa vilikuwa vinaonyesha havijatumika kwa sababu havikuwekewa alama wakati watalii wanaingia na vilevile havikuwekewa alama wakati wanatoka. Kwa hivyo inasababisha uwezekanano wa upoteaji wa mapato ikiwa mgeni atakaa zaidi ya muda aliolipia. Vivyo hivyo, kutengeneza mwanya wa kutumiwa tena kwa vibali bila malipo.
- **Vibali 12 vyenye kiasi cha malipo ya sifuri (rejea Kiambatisho III)** ambayo inamaanisha kuwa wageni wenye vibali hivi walitumia huduma bure.

- **Vibali 432 vyenye tarehe ya maombi ya kibali ya mbele kuliko tarehe ya kuingia (rejea Kiambatisho IV)** ambayo inamaanisha kuwa vibali viliundwa baada ya huduma kutolewa.
- **Vibali vya siku 14 vina tofauti kati ya tarehe ya kuingia na tarehe ya kutoka kwa zaidi ya siku 1 (rejea Kiambatisho V)** ambayo inamaanisha udhaifu wa udhibiti wa mfumo kuhakikisha aina ya uingiaji iliyochaguliwa (selected entry type) inaendana na idadi ya siku husika. Safari ya siku inapaswa kuwa chini ya siku kama wageni wanaingia na kutoka siku hiyo hiyo. Kwa hivyo, wakati safari ya siku imechaguliwa kama aina ya kuingia, tofauti kati ya tarehe ya kuingia na tarehe ya kutoka inapaswa kuwa chini ya siku moja.
- **Jozi 21 za maombi zinatumia nambari moja ya kibali (Kiambatisho II)**, wakati kila ombi la kibali linatakiwa kuwa na nambari ya kipekee ya kibali inayohusishwa na kiwango chake kilicholipwa, kwa hivyo ikiwa maombi mawili yanatumia nambari moja ya kibali inaweza kumaanisha kibali kimoja kilitolewa bila malipo.
- **Vibali vinaandaliwa na afisa TEHAMA ambaye ni msimamizi wa Mfumo (Kiambatisho VI)** kwa hivyo inakiuka kanuni iitwayo (principle of least privilege) ambayo inahitaji watumiaji wa mfumo kupewa haki kulingana na majukumu yao. Ni maoni yangu kwamba jukumu alilopewa Msimamizi wa mfumo (system administrator) linakiuka majukumu ya wasimamizi wa mfumo (system administrators) kama ilivyoelezwa katika mpango wa huduma. Tuna wasiwasi kwamba kuwapa majukumu wasimamizi wa mfumo ambao hawana uwezo unaohitajika kunatuweka katika hatari ya uwezekano wa kushindwa kuwawajibisha ikiwa kuna makosa ya makusudi au ya bahati mbaya yatafanyika.

Ni maoni yangu kwamba, udhaifu huu unasababishwa na kutozingatia mahitaji muhimu ya udhibiti wakati wa kukusanya mahitaji ambayo mfumo unatakiwa ufanye.

Nina wasiwasi kuwa, udhaifu huu wa udhibiti unachangia katika upoteaji wa mapato na utoaji wa taarifa za mapato zisizo sahihi.

Napendekeza yafuatayo kwa uongozi wa MNRT:

- (a) Kuanzisha utaratibu mzuri wa kudhibiti namna ya kuingia na kutoka katika maeneo ya vivutio yaliyo chini ya TAWA.
- (b) Kuimarisha udhibiti kwenye lango la kuingilia na lango la kutokea ili kuhakikisha vibali vyote vinakaguliwa wakati wa kuingia na wakati wa kutoka, tunashauri pia kutumia lango la kielektroniki.
- (c) Kuchunguza vibali ambavyo malipo yake yanaonesha sifuri na vile ambavyo viliombwa baada ya huduma kuwa imeshafanyika, na kuchukua hatua stahiki.
- (d) Kuchunguza endapo maombi mawili tofauti yanaonekana kuwa na kibali kimoja ili kuhakikisha kuwa hakuna upotezaji wa mapato.
- (e) Kupitia vibali vyote vinavyoonesha havijatumika ili kutambua vibali vilivyotumiwa na ambavyo havijatumika ili kuweka sawa katika mfumo.
- (f) Kuboresha mfumo wa MNRT portal kuhakikisha kwamba aina ya uingiaji (entry type) inayochaguliwa inaendana na idadi ya siku kati ya tarehe ya kuingia na tarehe ya kutoka.
- (g) Kuzuia wasimamizi wa mfumo kutekeleza majukumu mengi hasa yaliyo nje ya majukumu wanayopaswa kufanya kama vile kuunda vibali.
- b) Mfumo kukosa namna ya kuthibitisha ruhusa ya vibali vilivyozidisha muda kutolipiwa malipo ya ziada.

Nilikagua utaratibu wa kuchunguza vibali vilivyotumika zaidi ya muda uliolipiwa nikagundua kuwa mfumo unaruhusu mgeni aliye na sababu sahihi kutoka bila kulipia siku zilizozi. Hata hivyo, mchakato huu hauhitaji idhini wala uthibitishaji katika mfumo. Mamlaka yote amepewa afisa anayehusika na mchakato wa kuangalia utokaji sehemu ya vivutio tu. Kwa kuongezea, hakuna udhibiti mbadala kama vile ukaguzi wa kawaida wa mara kwa mara unaoweza kufanyika na meneja wa lango.

Ni maoni yangu kwamba hii imesababishwa na mapungufu katika kukusanya mahitaji yanayotakiwa kufanywa na mfumo na kutokuzingatia utengenezaji wa namna ya kudhibiti vitu vya mhimu.

Ni wasiwasi wangu kuwa kukosekana kwa utaratibu wa kuthibitisha vibali vinavyoweza kuwa vimetumika zaidi ya muda uliolipiwa kunaweza kusababisha upotevu wa mapato.

Napendekeza uongozi wa MNRT kuimarisha mfumo ili vibali vyote viweze kuthibitishwa muda wake na kama kuna sababu maalumu ya ukiukwaji basi uhalali wa sababu zao uweze kukaguliwa kwa kuangalia idhini ya Meneja wa Lango.

c) Kukosekana kwa utaratibu thabiti wa uthibitishaji wa kuingia na kutoka kwa vibali vya wageni

Katika ukaguzi wangu wa mfumo wa MNRT Portal, niliangalia utaratibu mbadala wa kuhakikisha kunakuwepo huduma endelevu na ya kuridhisha kwa wateja ikiwa mfumo haupatikani au una hitilafu. Nikabaini ukosefu wa utaratibu mzuri wa kushughulikia utoaji wa huduma katika milango ya kuingilia ndani ya hifadhi za taifa wakati ambapo mfumo (MNRT portal) haufanyi kazi/una hitilafu au haujapata taarifa kuhusu kufanyika kwa malipo kutoka mfumo wa GePG ambapo katika mfumo kibali huendelea kuonekana hakijalipiwa wakati mteja ameshalipa. Kwa kipindi hiki, TANAPA na NCAA hutumia fomu kukagua wageni/watalii wakati wa kuingia na wakati wa kutoka katika maeneo ya hifadhi. Hata hivyo, hakuna utaratibu/namna ya kuingiza taarifa hizo kwenye mfumo wa MNRT Portal ili kuakisi taarifa iliyojazwa katika fomu zilizochapishwa. Vivyo hivyo, kwa taasisi nyingine zinazotoa huduma kama vile utalii wa picha, kupiga kambi, kutembea na uwindaji, hakuna mwongozo maalumu juu ya jinsi ya kushughulikia visa kama hivi wakati ambao mfumo haufanyi kazi.

Ni maoni yangu kwamba hii inasababishwa na ukosefu wa tathmini ya athari katika huduma za taasisi, na ukosefu wa utengenezaji wa utaratibu wa kuhakikisha huduma inakuwa endelevu.

Nina wasiwasi kuwa, hii inaweza kusababisha wageni/watalii kutoridhishwa na huduma na pia uwezekano wa kupoteza mapato kama itatokea watalii ambao watapitiliza muda wao katika hifadhi, au kama fomu zinazotumika wakati mfumo una hitilafu zitatumika vibaya. Hii ni kwa sababu fomu hizi zinaweza kutumika hata wakati ambao mfumo hauna shida.

Napendekeza uongozi wa MNRT kutengeneza fomu ya kielektroniki ambayo itakuwa inatunza taarifa za mteja bila kuwapo kwa mtandao sehemu za langoni wakati mfumo unapokuwa na hitilafu na kuweza kutuma taarifa hizo katika mfumo uitwao MNRT Portal pale huduma itakaporejeshwa.

d) Mfumo kutowezesha watumiaji kuweza kuomba huduma wenyewe mtandaoni.

Nilikagua uwezo wa mifumo kufanya kazi kwa kujiendesha wenyewe ili kuweza kusaidia mteja kuomba huduma mtandaoni kwa urahisi, na nikagundua kuwa kuna huduma mbalimbali katika mfumo wa MNRT portal ambazo haziruhusu kujihudumia kwa mteja. Kwa hiyo mteja anapaswa kupakua, kuchapisha na kujaza fomu ya maombi kisha kuwasilisha katika ofisi za taasisi husika, huduma hizo ni ruhusa ya mwendesha utalii, kibali cha uvunaji wa misitu, usafirishaji wa asali, nyara, leseni ya kuvuna mkaa, leseni ya mwendeshaji watalii, leseni ya kampuni na leseni ya uwindaji.

Ni maoni yangu kwamba, hii inasababishwa na kutozingatia maoni ya wateja wakati wa uainishaji wa mahitaji ambayo mfumo unatakiwa kufanya. Lakini pia baadhi ya usumbufu ulitokana na kutokuunganishwa kwa MNRT Portal na mifumo mingine kutoka katika taasisi mbalimbali za Serikali kama BRELA.

Nina wasiwasi kuwa udhaifu huu unasababisha upatikanaji wa huduma kwa wateja kuwa mgumu kwani wanahitajika kujaza fomu na kuwasilisha katika ofisi husika.

Napendekeza Uongozi wa MNRT kuboresha mfumo wa MNRT Portal ili wateja wawe na uwezo wa kujihudumia wenyewe kupitia mfumo huo ili kuepuka kutumia fomu zilizochapishwa.

e) Utolewaji wa nambari za uthibiti wa malipo zaidi ya moja kwa mteja mmoja

Nilikagua mchakato wa malipo ya kuomba vibali kutoka katika mfumo (MNRT Portal) hasa kwa wageni wanaotaka kutembelea vivutio vya utalii vilivyo chini ya taasisi/mamlaka tofauti. Na kubaini kuwa wateja wanaotaka kutembelea vivutio mbalimbali vilivyo chini ya taasisi tofauti wanalazimika kutoa namba tofauti za malipo (control number) ili kupata kibali kimoja kitakachotumika. Hii ni kwa sababu kila nambari ya malipo

inawakilisha mapato ambayo yatahesabiwa kwa ajili ya taasisi husika. Hii sio rahisi kwani inahitaji wateja kuzunguka katika benki tofauti ili kufanya malipo katika nambari zilizotolewa kama inavyohitajika katika mfumo wa GePG, kwa kila taasisi kuwa na akaunti moja ya benki.

Ninadhani kwamba kutolewa kwa nambari za malipo (control number) Zaidi ya moja kwa mteja mmoja kwa ajili ya malipo ya huduma ileile, kunasababishwa na kukosekana kwa uwiano wa namna ya kufanya malipo katika taasisi zilizopo chini ya wizara ya maliasili na utalii.

Nina wasiwasi kwamba hii inasababisha usumbufu kwa mteja na kutoridhishwa na huduma na inaweza kusababisha kupoteza uaminifu juu ya matumizi ya mifumo.

Napendekeza uongozi wa MNRT kutengeneza mazingira yatakayowezesha kutolewa kwa nambari moja ya malipo kwa mteja kutoka mfumo wa GePG ambayo itawezesha malipo kufanyika kwa ajili ya huduma mbalimbali chini ya taasisi tofauti huku malipo yakiingia kwa kugawanywa katika taasisi husika.

f) Ukosefu wa utaratibu wa kushughulikia maoni ya wateja katika mfumo

Wakati wa ukaguzi wangu wa MNRT Portal kama mfumo mkuu wa utoaji wa huduma za utalii, nilibaini kuwa mfumo hauna namna ya kuwezesha wateja kutuma maoni yao. Ni maoni yangu kwamba katika taasisi kama hiyo, maoni ya wateja ni muhimu kwa uboreshaji wa huduma. Wakati wa ukaguzi, nilijulishwa na uongozi kwamba malalamiko yanashughulikiwa na taasisi binafsi na hakuna utaratibu wa wizara kujulishwa kwa hivyo inaleta ugumu katika kufuatilia huduma.

Ni maoni yangu kwamba kutoridhika kwa wageni kunaweza kusitambulike katika ngazi ya utawala na hivyo kusababisha athari katika soko letu la utalii.

Napendekeza uongozi wa MNRT kutengeneza na kutumia mfumo utakaotumika kupokea maoni ya wateja na kuyasambaza katika mifumo ya taasisi zilizo chini yake.

3.5 Mfumo wa kieletroniki wa maegesho ya magari (e-parking)

e-parking ni mfumo wa ukusanyaji wa mapato unaotumiwa na Wakala wa Barabara Vijijini Tanzania (TARURA) kukusanya ada ya maegesho bila hitaji la kuwa na wakusanya malipo na vifaa vyao katika maeneo ya maegesho. Mfumo huo ulijaribiwa katika mkoa wa Mwanza kama mfano. Mfumo huu unafanya kazi kuu mbili, ambazo ni; sehemu inayotumika kuchukua taarifa za gari (scanning) na sehemu ya kutengeneza ankara ya malipo (bill generation). Mkusanya mapato anachukua taarifa za gari, mmiliki pamoja na namba yake ya simu. Taarifa hizo zinatumiwa kwenye sehemu ya mfumo inayotumika kutengeneza ankara ya malipo na nambari ya malipo (control number) na kutuma kwa mhusika kupitia namba yake ya simu ili afanye malipo. Nilikagua ufanisi wa mfumo katika kufanya udhibiti na kubaini yafuatayo: -

a) Udhibiti dhaifu kwenye Mfumo wa Maegesho wa kielektroniki.

Ukaguzi wa mfumo wa maegesho (e-parking) ulibaini kuwa mkusanyaji anayekagua gari kwa kutumia kifaa cha kukagua (scanning device) ili kunasa namba ya usajili inayotumika kutambua gharama ya malipo, eneo la maegesho hutumiwa kuamua ada ya maegesho.

Mapitio yangu ya mfumo yalibaini kuwa mzabuni (vendor) hulinganisha kwa mikono namba za usajili wa gari zilizochunguzwa na faili la gari kwenye kanzi-data ya TRA ili aweze kuamua malipo kulingana na aina ya gari, kwani mfumo hauna utaratibu wa kuhakikisha namba ya usajili wa gari kupitia mifumo ya TRA. Ilibainika pia kuwa mfumo hauwezi kuamua moja kwa moja eneo la maegesho badala yake eneo linaingizwa kwa mikono jambo ambalo linakabiliwa na makosa ya kibinadamu. Kwa kuongezea, kuwa mfumo hauna njia ya ukaguzi (Audit Trail) ili kurekodi shughuli za watumiaji.

Ninaelezea udhaifu uliojulikana unatokana na kutozingatia udhibiti muhimu wakati wa kukusanya mahitaji na kubuni mfumo.

Nina wasiwasi kuwa kulinganisha kwa mikono namba ya usajili wa magari, na faili la kanzi-data ya TRA na kuingizwa kwa eneo la maegesho kunakabiliwa na makosa ya kibinadamu ambayo yanaweza kusababisha kutoza ada isiyofaa. Ukosefu wa njia za ukaguzi zitasababisha wakala kushindwa kuwawajibisha watumiaji wa mfumo ikiwa watautumia vibaya.

Ninapendekeza kwa uongozi wa TARURA

(a) Kuunganisha mfumo mpya ambao utachukua nafasi ya mfumo wa maegesho wa e-parking na Mfumo wa TRA-car na Mfumo wa Usajili wa Magari (CMVRS) ili kuhakikisha uhakiki wa mtandaoni wa magari yaliyokaguliwa.

(b) Kuhakikisha mfumo huo una habari sahihi ya mahali pa maegesho ambapo TARURA imeidhinishwa kukusanya ada ya maegesho.

(c) Kuhakikisha shughuli za watumiaji zimerekodiwa.

b) Magari yaliyokaguliwa bila malipo

Vifungu vya 7 na 8 vya ukusanyaji wa ada ya maegesho katika jiji la Mwanza na manispaa ya Ilemela mkataba no.ae/092/2017/2018/hq/cr/013 wa tarehe 10 "Julai 2018 kati ya Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (TARURA) (mkuu) na m / s NPK technologies ltd (wakala) inasema kuwa: -

- Wakala atahakikisha taarifa zote zilizopatikana zinakuwepo kwenye kifaa (digital enforcement) kila siku.
- Taarifa zote zinazohusu mapato ya ada za maegesho zitamilikiwa na mkuu (principal).

Nililinganisha orodha ya magari yaliyokaguliwa toka Januari hadi Juni 2020 na orodha ya tiketi za malipo kwa vipindi husika. Nikabainisha kuwa kwa kipindi hiki mzabuni alichunguza magari 1,398,140 lakini magari 1,139,483 hayakuwa kwenye orodha ya tiketi za malipo ambayo inamaanisha kuwa magari haya hayakulipiwa.

Maoni yangu ni kuwa, kasoro zilizobainishwa zinasababishwa na ukosefu wa ujumuishaji kati ya moduli ya malipo na mfumo wa SCANaCAR na upatanisho kati ya magari yaliyokaguliwa na kulipishwa.

Nina wasiwasi kuwa magari 1,139,483 yaliyokaguliwa ambayo hayamo kwenye orodha ya malipo sawa na asilimia 81.5 ya jumla ya magari yaliyokaguliwa yanaashiria kutofaulu kwa mchakato wa ulipaji.

Ninapendekeza Uongozi wa TARURA: -

- **Kutanua mchakato wa upatanisho (reconciliation process) ili kufanikisha upatanisho wa magari yaliyokaguliwa na magari yaliyotozwa.**
- **Kushirikiana na mzabuni sambamba na mkataba ili kuhakikisha urejeshaji wa hasara inayopatikana**
- **Kufanya ufuatiliaji wa haraka wa usimikaji wa mfumo wa TeRMIS, ambao moduli ya kukagua (scanning model), na malipo zimejumuishwa.**

c) Ankara zilizopita muda wa kulipiwa kutotozwa ada ya adhabu

Katika kutengeneza ankara za adhabu Mzabuni anahakiki faili la malipo ili kuhakikisha malipo yaliyozidi kwa siku tano. Baada ya hapo wakala hujumlisha ankara zote ambazo hazijalipwa na kuandaa orodha ya faili la adhabu. Mzabuni anapakia faili la adhabu kwenye mfumo wa e-Parking (mfumo wa utozaji), mfumo unaongeza Nambari ya SP, na nambari ya GFS kuomba nambari ya malipo (control number) kutoka GePG. Baada ya kupokea nambari ya malipo kutoka GePG, mfumo hutengeneza ankara ya adhabu.

Nilichukua baadhi ya vibali kutoka kwenye mfumo ambavyo malipo yalicheleweshwa kwa zaidi ya siku tano kutoka kwenye orodha ya vibali vya malipo na kuvipatanisha (reconcile) na orodha ya adhabu zilizolipiwa kutoka Januari hadi Juni 2020 na kubaini kuwa kati ya vibali 9289 vilivyocheleweshwa malipo, vibali 3889 havikuwemo kwenye orodha ya malipo ya adhabu. Wakala alipata hasara ya Sh. 77, 780,000 kutokana na vibali 3889 ambavyo havikulipiwa.

Mapungufu haya niliyogundua yanatokana na mchakato wa malipo ya adhabu kufanyika kwa mkono, na ukosefu wa upatanisho kati ya malipo yaliyocheleweshwa na ankara za adhabu.

Ninapendekeza Uongozi wa TARURA

- (a) Kutanua mchakato wa upatanisho ili kufanikisha upatanisho wa malipo yaliyocheleweshwa na bili za adhabu zilizoinuliwa.**
- (b) Kushirikiana na mzabuni (vendor) kwa mujibu wa mkataba ili kuhakikisha urejeshaji wa hasara inayopatikana**

3.6 Mfumo wa uendeshaji wa bandari

Mfumo wa TOS ni programu inayotumiwa na Mamlaka ya Bandari Tanzania TPA, kusimamia shughuli za bandari kwa vyombo vya kimataifa vinavyoingiza na kusafirisha mizigo. Mfumo una moduli kuu tatu ambazo ni; Mtazamo wa Bandari (Harbour view), shehena na malipo, moduli ambazo zimejumuishwa kupitia jukwaa la kubadilishana ujumbe (message exchange bus). Moduli ya ankara imejumuishwa na Mfumo wa malipo mtandaoni kwa malipo ya ankara. Moduli ya Mtazamo wa Bandari hutumiwa kusimamia vyombo na shughuli zao, moduli ya mizigo hutumiwa kudhibiti uhifadhi wa mizigo na utoaji idhini wakati moduli ya malipo inatumika katika uundaji wa ankara za malipo ya bandari. Mapitio ya mfumo na uhakiki wa ripoti za shehena na malipo ziligundua udhaifu ufuatao katika udhibiti;

- Idadi ya siku ambazo shehena imehifadhiwa hazihesabiwi moja kwa moja na mfumo badala yake idadi hiyo inapatikana wakati wa utoaji wa kibali. Jambo hili linakabiliwa na makosa ya kibinadamu na matumizi mabaya kwa faida binafsi.
- Tofauti kati ya tarehe halisi ya kuwasili na kuondoka kwa chombo kwa ajili ya hesabu ya malipo ya bandari huhesabiwa kwa mikono wakati wa kuunda ankara ya mwisho. Matokeo yake ni kuchaji zaidi au malipo ya chini kwa sababu hesabu inakabiliwa na makosa.
- Ukosefu wa njia ya kuchanganya Ankara Zaidi ya moja katika namba moja ya malipo (control number) katika moduli ya bili jambo ambalo linasababisha namba ya malipo kutengenezwa kwa mkono kutoka kwenye mfumo wa GEPG, na kusababisha ufuatiliaji wa historia ya malipo na upatanisho kuwa mgumu kwani malipo ya ankara hayatapatikana katika mfumo wa malipo (e-payment).
- Ukosefu wa ujumuishaji kati ya moduli ya shehena na mfumo wa TANCIS kwenye nyaraka zenye maalezo ya mizigo zilizowasilishwa TRA, kwa sasa nyaraka hizo zinapakuliwa kutoka kwenye mfumo wa TANCIS huko TRA na kupakiwa kwenye moduli ya mizigo na maafisa wa TPA utaratibu ambao unakabiliwa na mabadiliko ya kukusudia au yasiyokusudiwa.

Nina wasiwasi kuwa kuna uwezekano kwamba maelezo kadhaa ya shehena kutoka TANCIS yanaweza yasipakiwe kwenye mfumo wa shehena (cargo

system) na kusababisha ufuatiliaji kutowezekana, kwa mfano wakati wa ukaguzi nilibaini visa viwili ambavyo idadi ya mizigo katika mfumo wa mizigo ni ndogo kuliko idadi iliyoko kwenye nyaraka (Manifest) kutoka TANCIS kama ilivyoelezwa hapo chini

Jedwali Na. 3: Tofauti ya idadi ya mizigo kati ya mfumo wa Cargo wa Bandari na Mfumo wa TANCIS wa mamlaka ya mapato

Jina la meli	Call ID	ATA	ATD	TANCIS Namba ya Shehena	Mfumo wa Shehena/Na ya Shehena	Kituo
KOTA MEGAH	13549	29/09/2019	30/09/2019	843	838	TEHAMA
JENS MAERSK	1474	31/05/2020	17/05/2020	557	539	TEHAMA

Chanzo: Mfumo wa mizigo wa bandari na mfumo wa wa TANCIS mamlaka ya mapato

- Uthibitishaji duni wa data inayoingizwa kwenye mfumo, baadhi ya mizigo haina maelezo ya nchi inayokwenda hivyo kusababisha kutambua idadi ya siku za kuhifadhi shehena bure, kuwa kugumu.
- Malipo ya kodi ya jahazi na lighter Quay hayafanyiki kiotomatiki taarifa zinaingizwa kwa mikono.
- Malipo ya Mafuta (bulk oil billing) hayafanyiki kiautomatiki, hesabu hufanyika kulingana na hati iliyotolewa na sio data halisi kutoka kwenye pampu.
- Haijajumuishwa na mfumo ya TEHAMA ya kufuatilia kutoka kwa kontena, utoaji, kupokea na kupakia kwenye kituo cha TICS.

Maoni yagu ni kuwa, udhaifu huu unasababishwa na usanidi wa mfumo usiofaa na kutofaulu kuanzisha uhibitaji unaohitajika wakati wa kubadilisha mfumo.

Nina wasiwasi kuwa udhaifu uliotajwa unaweza kusababisha upotezaji wa mapato na uwezekano wa kupatikana taarifa zisizo sahihi za mapato katika taarifa ya kifedha

Ninapendekeza Uongozi wa mamlaka ya bandari;

- (a) Uboreshe matumizi ya TOS na uhakikishe idadi ya siku shehena ambazo zimehifadhiwa zinahesabiwa moja kwa moja na mfumo,**

- (b) Uhakikishe tozo za bandari zinahesabiwa moja kwa moja na mfumo, kwa kuhesabu moja kwa moja masaa kati ya tarehe halisi ya kuwasili kwa meli na kuondoka.
- (c) Utekeleze matumizi ya nambari moja ya malipo (control number) kwa ankara nyingi kwenye moduli ya malipo na mfumo wa malipo (e-payment system).
- (d) Ujumuishe moduli ya shehena (cargo module) na mfumo wa TANCIS ili kuepuka upakiaji wa nyaraka (manifest) kwenye mfumo kufanyika kwa mikono.
- (e) Utambue na kutekeleza vidhibiti vyote vinavyohitajika kwenye uingizaji wa data katika mfumo wa TOS,
- (f) Uweke utaratibu wa kulipa Kodi ya jahazi, Lighter Quay na malipo ya mafuta (bulk oil) kiatomatiki, na
- (g) Ujumuishe mfumo wa TOS na Mfumo wa TEHAMA ili kufuatilia kutoka kwa kontena, upokeaji na upakiaji kwenye kituo cha TICS.

3.7 Mfumo wa Safari portal

Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA) ilitengeneza mfumo unaoitwa safari portal unaotumika kusimamia ukusanyaji wa mapato katika milango yake ya kuingia na kutoka. Vyanzo vya mapato vinavyokusanywa na mfumo huu ni ada ya shughuli tofauti kwenye mbuga kama vile; ada ya kuingia, ada ya gari na ada ya makazi.

Wakati wa ukaguzi wa Mfumo wa Safari Portal, nilibaini udhaifu ufuatao.

- Udhaifu katika udhibiti wakati wa kuruhusu kibali kutumika baada ya kibali hicho kufunguliwa, ambapo mtu mmoja anaweza kuruhusu kibali kilichofunguliwa kutumika tena bila idhini. Mfumo unazuia kibali ambacho kimekaa kwa zaidi ya siku 30 bila kutumika, mchakato wa kuwezesha vibali kama hivyo huhitaji mwendeshaji wa utalii (tour operator) aandike barua kuomba kibali kufunguliwa ili kiweze kutumika tena ambapo maombi hayo yanapitishwa na mamlaka husika kisha afisa wa NCAA aliye na idhini anafungua kibali hicho katika mfumo. Nina wasiwasi kuwa ufunguaji wa kibali ndani ya mfumo hauna utaratibu wa idhini (approval), jambo hili linaweza kusababisha matumizi mabaya ya vibali vilivyofunguliwa ambapo vinaweza kufunguliwa na kutumiwa bila ombi kutoka kwa mmiliki na idhini sahihi.

- Ukosefu wa utaratibu wa kuthibitisha leseni ya TALA moja kwa moja (automatic). Nilikagua orodha ya waendeshaji wa utalii waliosajiliwa katika mfumo wa Safari Portal na kubaini kuwa mfumo hauna utaratibu mzuri wa kuthibitisha leseni za TALA za waendeshaji wa utalii. Uthibitishaji wa sasa unafanywa kwa mikono nje ya mfumo ambao unakabiliwa na makosa ya kibinadamu. Nililinganisha ripoti ya waendeshaji wa Utalii kutoka kwenye mfumo wa Safari Portal na orodha ya waendeshaji utalii waliosajiliwa na leseni zao za TALA kutoka kwenye mfumo wa Safari portal, nakabaini kuwapo kwa waendeshaji utalii 411 kwenye Safari wasio na leseni halali za TALA. Nina wasiwasi kuwa kutokuwapo kwa uthibitishaji wa leseni za TALA wa moja kwa moja kunaweza kusababisha wafanyabiashara wasio na leseni kufanya kazi na Mamlaka.
- Uthibitishaji duni wa uzito wa magari na uthibitishaji wa gari iliyosajiliwa ndani ya nchi. Niligundua kuwa tarifa ya uzito wa gari huchaguliwa kutoka kwenye orodha ya uzito wa magari uliosanidiwa badala ya kuthibitisha moja kwa moja kwa kutumia mfumo ya TRA. Nina wasiwasi kuwa mchakato huu unakabiliwa na makosa na unaweza kusababisha kutoza ada ndogo ikiwa uzito usio sahihi umechaguliwa.
- Hakuna uhakiki na utoaji idhini wa sababu zilizotolewa kwenye vibali vilivyotoka bila malipo. Tuna wasiwasi kuwa afisa anayehusika na mchakato, amepewa mamlaka makubwa ya konesha kuwa kibali kimetoka (check out), kwamba mtu anaweza kuamua kwa hiari kuidhinisha kutoka bila malipo kwa vibali vilivyozidisha muda wake ndani ya hifadhi ambavyo vilitakiwa kulipiwa.

Nina maoni kwamba udhaifu huu unasababishwa na usanidi duni wa mfumo na kutofaulu kuanzisha udhibiti unaohitajika wakati wa kutengeneza na kuunda mfumo.

Nina wasiwasi kwamba udhaifu uliobainishwa unaweza kusababisha upoteaji wa mapato na kupatikana kwa taarifa sisizo sahihi za mapato katika taarifa za kifedha.

Ninapendekeza uongozi wa NCAA:

- (a) Kutoa taarifa kwa waendeshaji watalii iwapo kibali kilichofunguliwa kitafunguliwa ili kuzuia matumizi mabaya.**

- (b) Kuthibitisha udhibiti unaofaa ili kuhakikisha kuwa leseni za mwendeshaji wa watalii zinathibitishwa ipasavyo wakati wa usajili kwa kujumuisha mfumo wa Safari Portal na mamlaka husika.
- (c) Kuboresha mfumo kwa kuuunganisha na Mfumo wa Usajili wa Magari wa TRA ili kuhakikisha kunasa moja kwa moja uzito wa gari kwa kuingiza nambari ya usajili wa gari husika.
- (d) Kuboresha mfumo ili vibali vyote vilivyotoka bila malipo vinawekwa alama ili kukaguliwa uhalali wa sababu zilizotolewa ili kibali kutoka bila malipo na idhini iliyotolewa na Meneja wa Lango.

3.8 Mfumo wa kukusanya kodi za mapato (ITAX)

Mapitio yangu kwenye mfumo wa ITAX wa Mamlaka ya Mapato (TRA), hasa juu ya ukamilifu wa taarifa za mapato yanayopatikana kulingana na miongozo iliyowekwa kwenye uandaaji wa ripoti za IPSAs unaohitaji Mamlaka ya Mapato ya Tanzania kutambua kodi iliyotathminiwa wakati ilipopaswa kukusanywa na si wakati wa inalipwa ylipolekea yafuatayo:

- Uwekwaji usio sahihi wa taratibu za utambuzi wa mapato yaliyopatikana ili kutoa ripoti IPSAS zilizopokelewa: Ilibainika kuwa, ripoti za IPSAS zilitumika kwa uzalishaji wa taarifa ya mapato kwa ukaguzi wa msingi wa hesabu za madeni zisizo sawa badala ya msimamo wa akaunti ya walipa kodi. Njia hii inakiuka taratibu za biashara, ambapo deni lisilo sawa linatokea hata ikiwa kiasi kilipingwa au kuna ushahidi wa malipo yanayotokana na kutothibitishwa kwa nambari ya udhibiti juu ya ushuru wa kodi na vilevile nambari za utozaji kutoka kwa tathmini zilizokatiwa rufaa. Hii ni kinyume na IPSAs 1.7 juu ya utambuzi wa mali (zinazopokelewa) kama rasilimali zinazodhibitiwa na taasisi kama taarifa zilizopita na ambayo faida za baadaye za kiuchumi au uwezo wa huduma unatarajiwa kutumiwa na taasisi.
- Kiasi cha kodi kinacho tarajiwa kupokelewa bila kuwa na nambari ya malipo, hii inaashiria kwamba kiasi hicho hakikuandaliwa kutoka kwenye mfumo, kwani nambari ya malipo inatokea wakati tathmini inafanywa kupitia mfumo

Nina maoni kwamba hii ilisababishwa na kuchelewesha kukamilika kwa uboreshaji wa mfumo wa ITAX

Mapungufu haya yanasababisha ukosefu wa ukamilifu wa taarifa za kifedha na mwanya wa ukwepaji wa kodi na vilevile upotezaji wa mapato ya serikali

Ninapendekeza uongozi wa mamlaka ya mapato kuhakikisha

(a) Hatua muhimu za kukamilisha uboreshaji wa mfumo wa ITAX umetayarishwa na unakamilishwa kwa wakati.

(b) Kuainisha muda maalumu na mikakati ya namna ya kufikia lengo la ukamilifu wa taarifa kwenye mfumo.

(c) Kuandaa kwa usahihi taarifa kulingana na miongozo ya IPSAS na,

(d) Tathimini ya malipo ya kodi inafanywa kwenye mfumo.

3.9 Mfumo wa ufuatiliaji wa mizigo ya forodha (Electronic Cargo Transit System -ECTS)

ECTS ni mfumo wa ufuatiliaji wa mizigo ambao umeunganishwa na vifaa vya kieletroniki kwa ufuatiliaji wa mizigo ambayo iko chini ya udhibiti wa forodha. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa ufanisi wake maswala yafuatayo yalibainika:

- **Ukosefu wa mgawanyo wa tahadhari zinazotolewa na mfumo katika makundi ya taadhari za taarifa na zile za kufanyiwa kazi, mapitio ya taarifa ya mfumo kwa siku ya tarehe 26 Oktoba, 2020, saa 14:07, kulikuwa na tahadhari 2,312,140 kwa safari 3596. Kutokana na rasilimali za sasa za wafanyakazi wanne (4) hadi sita (6) kwa zamu inakuwa ni vigumu kuamua ni tahadhari gani ya kushughulikia na ipi sio ya kushughulikia kwa kuzingatia uwezo wa utendaji wa kushughulikia tahadhari moja kwa dakika tano hadi dakika 20, kama ilivyoielezwa katika mahojiano niliyofanya na wafanyakazi wanaohusika. Kwa hivyo naamini kuwa kugawanya tahadhari katika makundi itahakikisha tahadhari zenye umuhimu mkubwa hazitoachwa kuzingatiwa**
- **Kufanyia kazi tahadhari badala ya ufuatiliaji wa njia:** Nilibaini kuwa wafanyakazi hufanya kazi kwa zamu ambayo inakuwa ngumu kuweka uwajibikaji kwa tahadhari zilizofanyiwa kazi na uhakika mdogo kwamba tahadhari za muhimu zinashughulikiwa. Kwa hivyo ninaamini kuwa italeta ufanisi kama mgawanyo wa kazi utazingatia njia za

magari badala ya taadhari zinazotolewa na mfumo. Kila mtumishi wa kituo cha ufuatiliaji na udhibiti apewe njia yake ya kufuatilia badala ya kila mmoja kuwa anashughulikia taadhari zinazotolewa na mfumo.

- **Matumizi yasiyo ya notisi za mfumo kwa mawasiliano ya ukiukwaji wa taribu,**

Mfumo wa ECTS una sehemu ya notisi ambayo inamwezesha afisa katika chumba cha udhibiti kupokea maelezo ya ukiukwaji wa taratibu au tahadhari ambazo hazijagunduliwa kutoka kwa maafisa waliopo kwenye vituo vya upekuzi vya forodha ambao wameshuhudia ukiukwaji au tahadhari, hii ilitengenezwa kama udhibiti wa pili kuripoti ukiukwaji ambao haujagunduliwa na mfumo. Hata hivyo, mapitio yangu yaligundua kuwa notisi hii haitumiwi badala yake maafisa waliopo kwenye vituo vya forodha hutumia barua pepe kuwasilisha ukiukwaji ulionekana, nina wasiwasi kwamba barua pepe sio njia yenye ufanisi kwa kupeana habari za kina kwa wakati za ukiukwaji wa taratibu, pia kwa matumizi ya barua pepe ni ngumu kufuatilia utekelezaji wa ukiukwaji uliotolewa taarifa.

- **Kutopitiwa kwa tahadhari ili kuhakikisha uwajibikaji wa watoa huduma:** Utendaji wa wauzaji wa kufuli za kielektroniki unaongozwa na mkataba wa usambazaji wakati kwa madereva wa magari yanayobeba mizigo ya forodha wanaongozwa na sheria za forodha. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa tahadhari zilizotolewa na mfumo wakati wa safari zinafutwa baada ya safari kumalizika, hii inafanywa bila kukagua tahadhari hizi kutambua ni mtoa huduma gani anapaswa kuwajibika kwa tahadhari zilizotumwa ili kuwaadhibu kwa mujibu wa mkataba na sheria.

Ni muono yangu kuwa bila utaratibu mzuri wa ufuatiliaji na ufanisi, malengo yaliyokusudiwa ya ufuatiliaji wa wavunjaji wa taratibu za bidhaa za forodha zinazosafirishwa hayawezi kufikiwa. Pia kutokuwapo kwa ushahidi wa afisa anayewajibika lakini pia utolewaji wa tahadhari nyingi na mfumo huficha tahadhari za kweli na muhimu.

Ninapendekeza uongozi wa mamlaka ya mapato kuhakikisha

- (a) Tahadhari zigawanywe katika makundi ya tahadhari za kufanyiwa kazi na tahadhari za taarifa.**
- (b) Kupitia taratibu za utendaji kazi kuleta tija kwenye ufuatiliaji na ufanyiwaji kazi wa taadhari,**

- (c) Kuna ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba ya watoa huduma na sheria za forodha katika usimamizi wa tahadhari zinazotolewa na mfumo, na,
- (d) Kuna utaratibu wa ufuatiliaji wa safari za magari ya mizigo ya forodha ambazo zinahakikisha uwajibikaji kwa wafanyakazi.

3.10 Mfumo wa kukusanya kodi za majengo (Non-Tax Revenue System -NTRS)

Aya ya 6 (1) (b) na (c) ya Miongozo ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (Ukadiriaji) (Ukusanyaji wa Kanuni za Viwango vya majengo), 2020 inahitaji Mamlaka katika eneo lililopimwa kuandaa rejista ya walipaji wote na kusajili majengo na wamiliki, pamoja na taarifa sawia za viwango vya ukusanyaji wa kodi za majengo katika rejista husika.

Nilipitia rejista ya majengo ya manispaa za Kinondoni, Ilala, Ubungo, Kigamboni na Temeke kutoka kwenye mfumo wa NTRS na kubaini yafuatayo:

- **Kuwapo kwa mlipa kodi mwenye nambari ya mlipa kodi zaidi ya moja.** Kila mlipa kodi ana nambari ya kipekee ya mlipa kodi ambayo hutumika kwenye kulipa na kufuatilia taarifa za malipo, kuwapo kwa walipa kodi wenye zaidi ya nambari moja ya mlipa kodi kunaweza kukasababisha kukosekana kwa uhalisia wa kodi iliyopokelewa kutoka kwa mlipa kodi mwenye nambari zaidi ya moja ya mlipa kodi, kunaweza kusababisha kodi kulipwa na moja kati ya nambari za mlipa kodi na hivyo kuacha nambari zingine za mlipa kodi kuwa na deni.
- **Kuwapo kwa majengo yenye kodi sifuri au kodi hasi.** Kiwango kikuu cha kodi ya majengo kwa manispaa zote za mkoa wa Dar es Salaam ni Sh. 10,000 kwa jengo la kawaida na Sh. 50,000 kwa kila roshani katika majengo ya ghorofa. Lakini, nilibaini kuwapo kwa majengo yaliyosajiliwa yakiwa na kodi hasi na sifuri.

Maoni yangu ni kuwa, mapungufu yaliyobainishwa yamesababishwa na:

- Uhamishaji usiofaa wa taarifa kutoka kwenye mfumo wa zamani wa kieletroniki wa usimamizi wa malipo ya kodi za majengo na kukosekana kwa uthibitisho wa viwango vya kodi .
- Kuendelea kutumia taarifa za mfumo wa zamani wa PRMS kutoka Serikali za Mitaa ambapo taarifa za walipa kodi hazikutambuliwa kiurahisi kwa kuwa nambari ya utambulisho ya mlipa kodi (TIN) haikuwa inatumika.

- Ukosefu wa utambulisho wa majengo yanayopatikana katika maeneo yasiyopimwa.

Ni maoni yangu kuwa, mapungufu haya yanaweza kusababisha utunzaji wa rejista ya majengo isiyo sahihi ambayo itaathiri taarifa ya mapato ya kodi.

Napendekeza uongozi wa Mamlaka ya Mapato:

- (a) Kupitia mfumo na kuboresha kanzidata ya mfumo na kuhakikisha taarifa za majengo zinatambulika kipekee na kuondoa taarifa zinazojirudia.
- (b) Kubainisha majengo yote yenye viwango visivyo sahihi vya kodi na kurekebisha viwango hivyo.
- (c) Kuhakikisha uhamishwaji sahihi wa data kutoka katika mfumo wa zamani wa usimamizi wa kodi za majengo.

3.11 Gaming Licensing, Inspection and Compliance Applications (GLICA)

Mfumo wa maombi ya leseni za michezo ya kubahatisha ni mfumo uliotengenezwa na bodi ya michezo ya kubahatisha (GBT) ili kusaidia usimamizi wa shughuli za bodi kulingana na miongozo, era, na sheria. Sehemu ambazo zilikuwa zimekamilika na kutumiwa na watumiaji ni pamoja na: Utoaji leseni, Burudani na Bahati Nasibu, Ukaguzi na Utekelezaji, Vifaa na Usimamizi wa Programu, Marejesho ya Bahati Nasibu, Malalamiko, Migogoro, Matangazo na Ombi la Taarifa, uchezaji unaofuata misingi ya uwajibikaji, taarifa mbalimbali na taadhari za kimfumo.

Nilifanya mapitio kwenye mfumo wa GLICA kutambua ufanisi wa udhibiti wa matumizi na kubaini madhaifu yafuatayo: -

- Mfumo unatoa nafasi kwa afisa mtoa leseni kuruka hatua katika maombi ya leseni ya mchezo wa kubahatisha. Maombi ya leseni yaliyowasilishwa yanapokelewa na msimamizi wa leseni ambaye humpa afisa wa leseni ili ahakiki maombi hayo, baada ya uhakiki afisa anapaswa kuchagua hatua inayofuata ambayo maombi yanapaswa kuendelea.

Kulingana na aina ya leseni inayoombwa baadhi ya maombi mapya yanapaswa kupitia hatua ya uchambuzi wa uwezo wa kifedha wa muombaji ili kuhakiki wa mwombaji katika kuendesha michezo ya kubahatisha. na kuangalia historia ya mwombaji ili kujiridhisha kuwa hana rekodi ya makosa ya jinai ikiwemo utakatishaji wa pesa na ukwepaji wa kodi.

Mfumo ulipaswa kupeleka maombi moja kwa moja kwenye hatua ya uchambuzi wa kifedha baada ya uhakiki kwa maombi ambayo ni lazima kufanyiwa uchambuzi wa kifedha badala ya kuruhusu afisa leseni kuamua hatua inayofuata. Ni maoni yangu kwamba hii inaweza kusababisha kurukwa kwa makusudi au kwa bahati mbaya kwa hatua hii ambayo inaweza kusababisha kutolewa kwa leseni kwa mwombaji asiyekidhi vigezo vya kifedha.

- Mfumo hauwezi kutambua muda uliotumika kutoa leseni za waajiriwa wa kampuni za michezo ya kubahatisha kutoka tarehe ya maombi hadi tarehe ya kutoa leseni. Kumekuwa na matukio ya kucheleweshwa kwa utoaji wa leseni hizo.
- Ukosefu wa ripoti kwa waendeshaji ambao hawajawasilisha marejesho ili kuwezesha ufuatiliaji. Pia, hakuna ripoti ya stika za mashine za michezo ya kubahatisha ambazo hazijatumika wakati wa usajili wa mashine kwa ufuatiliaji wa matumizi ya stika kwa urahisi.

Ni maoni yangu kwamba kasoro zilizobainika zinachangiwa na tathmini isiyofaa ya udhibiti wa matumizi wakati wa uainishaji wa mahitaji na muundo wa mfumo.

Nina maoni kuwa ukosefu wa udhibiti mzuri wa maombi ya leseni kunaweza kusababisha ucheleweshaji wa kutoa leseni, ukosefu wa uwajibikaji na kutofuata sheria na kanuni.

Ninapendekeza uongozi wa bodi ya kubahatisha

- (a) Kuboresha mfumo ili maombi mapya ya leseni yenye ulazima wa kupitia uchambuzi wa kifedha upitie na hatua zingine zinazohitajika kulingana na sheria na kanuni badala ya kumwachia afisa wa leseni kuamua hatua inayofuata.**

- (b) Kuhakikisha mfumo unatunza taarifa ya muda unaotumika kufanyia kazi maombi ya leseni za wafanyakazi wa michezo ya kubahatisha.
- (c) Kutengeneza taarifa inayoonesha waendeshaji wa michezo ya kubahatisha ambao hawajawasilisha marejesho na stika za mashine za michezo ya kubahatisha ambazo hazikutumika wakati wa usajili wa mashine za michezo ya kubahatisha.

3.12 Regulatory Central Electronic Monitoring System (GREMS)

Mfumo wa Kielektroniki wa Kudhibiti na Ufuatiliaji wa michezo ya kubahatisha (GREMS) unatumiwa na bodi ya michezo ya kubahatisha kufuatilia na kuhakiki udhibiti wa mapato ya serikali, uwajibikaji wa wachezaji na ufahamu wa soko la michezo ya kubahatisha. Watumiaji wa mfumo huu ni bodi yenyewe na waendeshaji wa michezo ya kubahatisha. Mfumo huu umeunganishwa na mifumo ya waendeshaji wa michezo ya kubahatishaili kubadilishana taarifa kati ya bodi ya michezo ya kubahatisha na waendeshaji wa michezo hiyo kuhusu shughuli za uchezaji kama vile dau la kubashiri, kiwango cha kushinda, kodi kwa ushindi na washindi.

Mapitio yangu juu ya utendaji kazi na muundo wa mfumo wa GREMS nilibaini kuwa, kwa mashine za michezo ya kubahatisha zinazotumiwa na waendeshaji wa michezo ya kamari na maduka ya mashine za 'slot' bodi imeunda na kutengeneza kifaa maalum kinachoitwa Sigma ambacho kitaingizwa kwenye mashine za michezo ya kubahatisha ili kunasa moja kwa moja shughuli za uchezaji pamoja na miamala na kuzituma kwenye 'server' kuu ya mfumo wa GREMS kwa ufuatiliaji wa papo kwa hapo. Kwa kuongezea, kwa upande wa michezo ya kamali za mtandaoni na michezo ya kubashiri kuna Mfumo Uunganishi (API) ambao hupokea habari kutoka kwa mifumo ya waendeshaji na kupeleka kwenye mfumo wa GREMS. Lakini, ukaguzi wangu wa ufanisi wa udhibiti ili kuhakikisha ufuatiliaji na ugunduzi wa kutosha wa kutofuata sheria ulibaini mapungufu yafuatayo;

- Ukosefu wa udhibiti madhubuti wa kuhakikisha usahihi wa taarifa kutoka kwenye mifumo ya waendeshaji wa michezo ya kubahatisha kabla ya kutumwa kwenye mfumo wa GREMS hasa kwa michezo ya kamari za mtandaoni na michezo ya kubashiri

Kwa sasa, bodi imeanzisha utaratibu wa kufanya upatanisho wa taarifa baina ya mfumo wa GREMS na mifumo ya waendeshaji wa michezo ya

kubahatisha ambapo waendeshaji wanapaswa kutuma taarifa za kila siku za miamala yao. Kisha miamala hiyo, inalinganishwa na taarifa ambazo zimewasilishwa moja kwa moja kwenye mfumo wa GREMS na mifumo yao.

Hata hivyo nina mashaka na ufanisi wa utaratibu huu kwani bado ni ngumu kugundua ikiwa taarifa zilizowasilishwa ni halisi na hazijafanyiwa marekebisho kabla ya kutumwa kwa bodi. Kwa hivyo nina wasiwasi kuwa hii inaongeza hatari kwamba taarifa zilizopokelewa kutoka kwa waendeshaji wa michezo ya Kamari za mtandaoni na michezo ya kubashiri zinaweza kuwa sio halisi.

- Mfumo hautoi taarifa ambayo inaonesha kucheleweshwa kwa kupokelewa kwa taarifa kutoka kwa watoa huduma. Taarifa hii inaweza kusaidia kuwabaini watoa huduma ambao mifumo yao haijatuma taarifa kwenye GREMS kwa wakati na hatua stahiki kuchukuliwa.
- Mchezo wa kamari ya mezani haujajumuishwa katika mfumo wa GREMS kwa hivyo ufuatiliaji wa shughuli zake na uthibitisho wa mapato bado zipo nje ya mfumo,
- Ukosefu wa ugrunduzi wa uchezaji usiowajibishwa kwa wachezaji wa michezo ya kubahatisha licha ya kwamba mfumo kuwa na uwezo wa kurekodi taarifa na matukio ya wachezaji.
- Mfumo haujaunganishwa na mfumo wa GLICA kwa ajili ya kuthibitisha usajili na idadi ya mashine za michezo ya kubahatisha ambazo zinatuma taarifa. Hii itasaidia kutambua mashine zote zilizosajiliwa na ambazo hazijasajiliwa pia kujua mashine zilizosajiliwa lakini hazitumi taarifa kwenye mfumo wa GREMS ili kufanya ufuatiliaji.

Ni maoni yangu kuwa ukosefu wa udhibiti mzuri wa kimfumo unaweza kusababisha upotezaji wa mapato kwa sababu ya kuchelewa kupokea taarifa juu ya shughuli za uchezaji.

Ninashauri uongozi wa GBT:

- (a) **Kuchunguza udhibiti bora ili kuhakikisha ukamilifu wa data zilizotumwa kwenye mfumo wa GRAMS na kasino za mtandaoni na waendeshaji wa kubashiri michezo ya kubashiri.**

- (b) Tengeneza utaratibu bora wa kuripoti waendeshaji ambao mifumo yao inachelewa kutuma data kwenye mfumo wa GREMS.
- (c) Kuandaa ukusanyaji wa miamala ya kasino zisizokua za mtandaoni kwenye mfumo wa GREMS,
- (d) Kuainisha na kuhimiza kamari inayotakiwa,
- (e) Kuunganisha GREMS na GLICA kwa uhakiki wa usajili wa mashine za uchezaji na kufuatwa kwa taratibu.

3.13 Mfumo wa maombi mtandaoni wa shirika la viwango Tanzania (TBS Online Application System - OAS)

OAS ni mfumo wa maombi mtandaoni unaowezesha wateja wa TBS kupeleka maombi mtandaoni kwa huduma zifuatazo, Ukaguzi wa mahali inapofikia, PVoC , utoaji wa masharti, usajili wa bidhaa na msaada wa kiufundi kwa wauzaji bidhaa nje (TAE)

Mapitio katika mfumo wa matumizi ya OAS ulibaini udhaifu ufuatao wa kiudhibiti:

- Ukosefu wa udhibiti wa mfumo kuzuia sampuli kujaribiwa kabla ya malipo, udhibiti kwa sasa unategemea afisa anayepokea ambapo wakati wa kupokea sampuli, afisa atathibitisha kwenye mfumo ikiwa malipo yamefanywa. Tuna wasiwasi kwamba udhibiti huu haufanyi kazi badala yake mfumo unapaswa uundwe kuzuia programu kwenda kwenye hatua ya kupokea sampuli ikiwa malipo ya ada hayajafanywa.
- Hesabu ya ada hufanywa kwa mikono nje ya mfumo ambao unakabiliwa na makosa ya kibinadamu na makosa ya kukusudia.

Nina maoni kwamba makosa haya yanaweza kusababisha upotezaji wa mapato, hesabu isiyo sahihi ya ada na usumbufu kwa wateja.

Ninapendekeza uongozi wa shirika la viwango

- (a) Kuboresha OAS kuhakikisha kuwa maombi yanazuiliwa kwenda hatua ya kupokea sampuli ikiwa malipo ya ada hayajalipwa.
- (b) Kuweza kujiendesha na kutoa hesabu ya ada haswa kwa hesabu zisizo ngumu.

3.14 MAKOSA KATIKA USANIDI WA ADA NA USHURU KWENYE MIFUMO YA MAPATO

- a) Kutolandana kwa viwango vya ushuru vilivyosanidiwa katika mfumo wa “MNRT Portal “na vile vilivyoidhinishwa na taasisi husika.

Nimepitia viwango vya ushuru wa huduma katika taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Maliasili na Utalii ambazo zinatimia mfumo wa MNRT Portal, na kubaini kuwa viwango vya ushuru wa huduma zilizosanidiwa kwenye mfumo vinatofautiana na viwango vya huduma vilivyoidhinishwa na taasisi moja kwa moja kwa mujibu wa sheria, taratibu, na kanuni za taasisi husika. Jedwali lifuatalo linaonesha tofauti iliyobainika:

Jedwali Na. 4: Tofauti kati ya viwango vya ushuru vilivyosanidiwa katika mfumo wa “MNRT Portal” na vile vilivyoidhinishwa na taasisi husika.

HUDUMA	KIWANGO CHA USHURU KWENYE MIFUMO WA MNRT PORTAL	KIWANGO CHA USHURU MUJIBU TANGAZO SERIKALI	TOFAUTI
Tozo ya michezo ya Usiku - Watoto wenyeji	SH. 25,000	SH. 5,000	SH. 20,000
Tozo ya michezo ya Usiku - Watoto wenyeji	DOLA ZA MAREKANI 100	DOLA ZA MAREKANI 50	DOLA ZA MAREKANI 50
Tozo ya michezo ya Usiku - Watoto wenyeji	DOLA ZA MAREKANI 50	DOLA ZA MAREKANI 25	DOLA ZA MAREKANI 25
Conservation Adult (NR)	DOLA ZA MAREKANI 15	DOLA ZA MAREKANI 60	DOLA ZA MAREKANI -45
Conservation Child (NR)	DOLA ZA MAREKANI 25	DOLA ZA MAREKANI 20	DOLA ZA MAREKANI 5
Kiingilio cha Wakubwa (E)	DOLA ZA MAREKANI 50	-not defined	-
Kiingilio cha Watoto (NR)	DOLA ZA MAREKANI 30	-not defined	-
Pikipiki t.w 2001 - 3000kg (R)	SH. 50,000	SH. 35,000	SH. 15,000
Magari ya Wazi - uzito wa kati ya 3001 - 7000 Kgs (L)	SH. 112,500	SH. 90,000	SH. 22,500
Pikipiki t.w 7001 - 10000kg (R)	SH. 125,000	SH. 150,000	SH. -25,000

HUDUMA	KIWANGO CHA USHURU KWENYE MFUMO WA MNRT PORTAL	KIWANGO CHA USHURU MUJIBU TANGAZO SERIKALI	TOFAUTI
TAWA			
Aircraft Landing (13> Seater) - TZ - (Per Cycle in Game Reserves)	SH. 80,000	SH. 30,000	SH. 50,000
Aircraft Landing (1-4-Seater) - NonTZ - (Game Reserves)	DOLA ZA MAREKANI 100	DOLA ZA MAREKANI 30	DOLA ZA MAREKANI 70
Kutua Ndege (1-4-Seater) - TZ - (Per Cycle in Game Reserves)	SH. 50,000	SH. 15,000	SH. 35,000
			TFS
Mianzi kutoka Misitu na Uoto wa Asili - Daraja la I - Chini ya sm 5 - Kiwango cha nguzo 20	SH. 16,000	SH. 20,000	SH. -4,000
Mianzi kutoka Misitu na Uoto wa Asili - Daraja la II - Chini ya sm 5 - Kiwango cha nguzo 20	DOLA ZA MAREKANI 600	DOLA ZA MAREKANI 100	DOLA ZA MAREKANI 500
Mianzi kutoka Misitu na Uoto wa Asili - Daraja la II - Chini ya sm 5 - Kiwango cha nguzo 20	DOLA ZA MAREKANI 1,000	DOLA ZA MAREKANI 1,200	DOLA ZA MAREKANI - 2000
Kibali cha Kupiga Kambi katika Mahema kwa Wageni (Zaidi ya watu 5) - A/Mash.	DOLA ZA MAREKANI 2,000	DOLA ZA MAREKANI 1,500	DOLA ZA MAREKANI 5,000
Kibali cha Kupiga Kambi katika Mahema kwa Wageni (Zaidi ya watu 5) - A/Mash.	DOLA ZA MAREKANI 20	DOLA ZA MAREKANI 15	DOLA ZA MAREKANI 5
Kibali cha Kupiga Kambi katika Mahema kwa Wageni (Zaidi ya watu 5) - A/Mash.	DOLA ZA MAREKANI 15,000	DOLA ZA MAREKANI 20,000	DOLA ZA MAREKANI 5,000

Chanzo: Usanidi wa Mkaguzi baada ya kulinganisha viwango vya ushuru vilivyopo kwenye mfumo na viwango vilivyoidhinishwa na taasisi husika.

Nina shaka kuwa swala hili linaweza kusababisha makosa katika taarifa za mapato na vilevile kusababisha taasisi husika kutoza gharama za juu katika utoaji huduma jambo ambalo ni kinyume na sheria, kanuni, na taratibu za uanzishwaji wa taasisi hizo.

Ninapendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuchukua hatua zifuatazo;

- (a) Kufanya mapitio ya viwango vya ushuru vilivyosanidiwa katika mfumo wa MNRT Portal ili kuhakikisha kuwa viwango hivyo ni sahihi kwa mujibu wa sheria, kanuni, na taratibu za uanzishwaji wa taasisi hizo.**
- (b) Kuanzisha utaratibu wa usimamizi katika kufanya mabadiliko ya usanidi wa mfumo ili kuhakikisha kuwa viwango vya ushuru vilivyoidhinishwa na taasisi husika vinasanidiwa kwa usahihi katika mfumo.**
- (c) Kuzielekeza taasisi kufanya mapitio ya viwango vyao vya mapato ili zifanye marekebisho stahiki katika taarifa za fedha.**
- (d) Makosa katika ankara za mfumo wa Ankara wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Manispaa ya Iringa**

Nilifanya ukaguzi katika Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Manispaa ya Iringa (IRUWASA) ambao nimebaini kuwa Ankara za maji zilikuwa na makosa. Katika ukaguzi wangu nilitathmini Ankara za mfumo wa SBM unaotumiwa na Mamlaka na kubaini kuwa jumla ya miamala 365 ilikuwa na makosa katika utengenezaji wa Ankara, kama ifuatavyo.

- Wateja katika miamala 41 walilipishwa zaidi kwa jumla ya Sh. 45,310/=.
- Wateja katika miamala 81 walilipishwa pungufu kwa jumla ya Sh.12,300/=.
- Wateja katika miamala 243 hawakulipishwa ingawa, kwa mujibu wa makundi ya mita zao walitakiwa, mamlaka ilitakiwa itoe ankara zenye jumla thamani ya Sh. 15,347,720/=.

Pia, nimebaini kuwa mamlaka haifanyi mapitio ya mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa bei za ankara zilizosanidiwa kwenye mfumo

zinaendana na bei za Ankara kwa mujibu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Maji na Nishati (EWURA).

Ninashaka kuwa kuchaji kiwango cha zaidi katika anakara za maji kutapelekea makosa katika taarifa ya fedha, na kuchaji pungufu kutapelekea upotevu wa mapato.

Ninapendekeza menejimenti ya IRUWASA ichunguze chanzo cha sababu iliyopelekea utofauti wa ankara na kuchukua hatua stahiki katika kurekebisha utofauti huo. Aidha, menejimenti ifanye mapitio ya mara kwa mara katika viwango vya Ankara vilivyosanidiwa katika mfumo ili kuhakikisha kuwa viwango hivyo vinaendana na viwango vilivyoidhinishwa na EWURA.

- b) Mapungufu katika ukokotozi wa ada za katika kazi na miradi ya ujenzi inayosajiliwa na Bodi ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB)

“Ibara ya 34(5) Architects and Quantity Surveyors (Registration) Act No. 10 ya mwaka 2010 inaelekeza kuwa kila msanifu majengo au mkadiriaji ujenzi anayepata mradi anawajibika kuusajili mradi huo kwa Bodi ya Wasanifu Majengo na Wakadiriaji ujenzi ndani ya siku 30 baada ya kuingia makubaliano, vinginevyo atawajibika kupata adhabu.” - Itabidi kwaona wanasheria kuhakikisha usahihi wa tafsiri.

Ukaguzi wa idadi ya miradi iliyosajiliwa na mapato yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2019/20 niliufanya katika Bodi Usajili wa Wasanifu Majengo na Wakadiriaji, nimebaini ada za usajili miradi ya usanifu majengo na ukadiriaji ujenzi zilikuwa chini ya kiwango stahiki. Upungufu huo niliubaini umesababisha mapato yaliyoripotiwa kwenye taarifa ya fedha kuwa pungufu kwa jumla ya Sh. 21,018,920.56. Nilipotaka ufafanuzi wa suala hili, menejimenti ilinitaarifu kuwa kulikuwa na hitilafu katika mfumo wa taarifa wakati wa uingizaji wa taarifa kulikopelekea makosa ya ukokotozi wa gharama za miradi kulingana na viwango vilivyoidhinishwa.

Nina shaka kuwa hii imepelekea upotevu wa mapato ya takriban Sh. 21,018,920.56

Ninapendekeza menejimenti ya AQRB kuhakikisha inafuata mwongozo wa ukokotoaji wa ada za usajili wa miradi kama zilivyo idhinishwa na Bodi.

- c) Kukosekana kwa ushahidi wa uidhinishwaji wa viwango vya ada vilivyosanidiwa katika mfumo wa Maegesho wa Kieletroniki (e-Parking)

Nimefanya mapitio ya usanidi wa ada za maegesho kwenye mfumo wa maegesho wa kieletroniki unaotumiwa na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili kutoa uhakika juu ya usahihi wa viwango vya ada za maegesho zilizosanidiwa kwenye mfumo kama ziliidhinishwa na Menejimenti ya Wakala. Katika ukaguzi wangu niliomba taarifa zinazoonesha viwango vilivyo idhinishwa na menejimenti ili nijiridhishe usahihi wa viwango vya ada vilivyosanidiwa katika mfumo. Hata hivyo, sikuweza kupata taarifa hizo.

Jedwali Na. 5: Ada za maegesho zilizosanidiwa kwenye mfumo wa e-Parking.

Eneno la Maegesho	Aina ya Gari	Kiwango cha ada (SH.)
Soko la Mwaloni Kirumba	Small cars (Saloon Cars and SUV)	1,500
Soko la Mwaloni Kirumba, Miembeni na aeneo mengine ya kupandisha na kushushia mizigo	Pickup (Business)	2,000
Soko la Mwaloni Kirumba, Miembeni na aeneo mengine ya kupandisha na kushushia mizigo	Pickup (Private)	1,500
Maeneo yote ya H/Jili I Mwanza	Motorcycles	200
Maeneo yote ya H/Jili I Mwanza	Tricycle	500
Soko la Mwaloni Kirumba, Miembeni na aeneo mengine ya kupandisha na kushushia mizigo	Lorry/car Weighing below 3.5 tonnes	2,000
Soko la Mwaloni Kirumba, Miembeni na aeneo mengine ya kupandisha na kushushia mizigo	Lorry/car weighing between 3.5 to 10 tonnes	3,000

Chanzo: Ada zilizosanidiwa kwenye mfumo wa e-Parking

Ninashaka kwamba hali hii inaweza kupelelekea makosa ya ada zilizosanidiwa kwenye mfumo kinyume na maamuzi ya menejimenti hivyo kusababisha upotevu wa mapato.

Ninapendekeza menejimenti ya TARURA kufanya mapitio ya ada zilizosanidiwa kwenye mfumo ili kujiridhisha kama ada hizo ni sahihi kwa mujibu wa maelekezo ya Bodi ya Wakurugenzi. Aidha menejimenti itathmini kiwango cha pesa kilichopotea kama itabainika kuna tofauti kati ya viwango vya ada vilivyoidhinishwa na viwango vya ada vilivyosanidiwa kwenye mfumo.

SURA YA NNE

4.0 UTEKELEZAJI WA MIFUMO YA KIFEDHA SERIKALINI

Kwa mujibu wa waraka nambari 5 wa tarehe 18 Novemba 2019 uliotolewa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa maafisa masuuli, inazitaka sekta za umma kuomba kibali kutoka wizara ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha za serikali.

Waraka pia umeainisha nia ya serikali kuufanya na kuutambua MUSE kuwa mfumo wa kihesabu unatakiwa kutumika na sekta za umma. Kadhalika serikali kupitia wizara ya fedha na mipango imeidhinisha mfumo wa kieletroniki wa usimamizi wa rasilimali, yani “Electronic Resource Management System (ERMS)” uliotengenezwa na kusimamiwa na Mamlaka ya Mtandao wa Serikali (eGA) kuwa ni mfumo rasmi wa usimamizi wa fedha utakaotumika katika sekta za umma.

Lengo la serikali ni kuhakikisha usawa, uhimilivu wa gharama, kurahisisha majumuisho ya fedha za serikali, kufuata miongozo na kanuni za kifedha kwa mifumo ya usimamizi wa kifedha inayotumika katika sekta za umma.

Katika mwaka huu wa fedha, nilibaini yafuatayo katika utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha za serikali katika sekta ya umma;

(a) Maelekezo yasiyo bayana juu ya utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa fedha za serikali.

Mapitio ya utekelezaji wa mifumo ya usimamizi wa kifedha za serikali katika sekta ya umma yalibaini kwamba kuna uelewa tofauti miongoni sekta za umma wa namna ya kuutambua mfumo wa usimamizi wa kifedha unavyotakiwa kutumika.

Wizara ya Fedha na Mipango imeidhinisha mifumo ya MUSE na ERMS kuwa mifumo ya usimamizi wa fedha ambayo inaweza kutumiwa na sekta za umma.

Hata hivyo, hakuna mwongozo kwa sekta za umma kuwafahamisha namna ya kuchagua mifumo ya kifedha iliyoidhinishwa. Badala yake, taasisi na idara za serikali zinaelekezwa kutumia tu MUSE. Hivyo kusababisha mkanganyiko kwa taasisi hizo ambazo hupendelea kutumia ERMS kulingana na mahitaji yao.

Kwa mfano, katika ukaguzi wangu wa utekelezaji wa agizo la serikali kuhusu kusimika na kutumia mfumo ya kifedha nilibaini kwamba, Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) limesimika na kuanza kutumia mfumo wa ERMS. Pamoja na kuanza kutumia mfumo huo, shirika pia limefanya mafunzo kwa watumiaji wa mfumo kufanya shughuli za awali kama vile kuongeza watumiaji kwenye mfumo, na watumiaji kupewa haki za kuingia na kutumia mfumo. Hata hivyo, niliarifiwa kuwa uongozi wa shirika la utangazaji (TBC) ulipokea maagizo ya kutumia MUSE kwa shughuli za kiuhasibu na Planrep kwa shughuli za upangaji.

Pia tulibaini changamoto za taasisi juu ya uwezekano wa kuboresha mfumo wa muse ili uweze kutumika kulingana na mahitaji ya taasisi husika, katika taasisi ambazo zimaeanza kutumia mfumo wa MUSE.

Mapitio yangu ya mpango wa kupata na kuanza kutumia mfumo wa MUSE niliofanya katika Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) yalibaini kwamba uongozi wa chuo kiliunda timu iliyoenda wizara ya fedha na mipango kuangalia kama mfumo wa MUSE utakidhi mahitaji ya chuo. Timu hiyo ilibaini moduli sita za mfumo ambazo zinahitaji kuboreshwa ili mfumo uweze kutumika kwa shughuli za kifedha za chuo.

Timu hiyo pia ilipendekeza kupitiwa kwa Kanuni na Sera za Fedha ili kuendana matumizi ya MUSE. Katika kutafuta ufanisi wa utendaji, sera zinaweka udhibiti wa ndani kulingana na mazingira ya taasisi ili kupunguza athari na kuboresha ufanisi. Hivyo basi, utekelezaji wa MUSE unapaswa kuzingatia kanuni na sera hizo.

Ni maoni yangu kwamba MUSE haitakidhi matakwa ya Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine hadi pale itakapofanyiwa maboresho ili kuendana na kanuni na sera za kifedha za chuo hicho. Jambo hili litawezekana endapo kutakuwa na uwezekano wa kuboresha mfumo wa MUSE ili kukidhi mahitaji ya taasisi moja moja hata hivyo MUSE ni mfumo wa jumla uliotengenezwa kwa lengo la kukidhi matakwa ya kiujumla ya taasisi zote za serikali.

Maoni yangu ni kwamba, changamoto hii inasababishwa na kukosekana kwa juhudi zilizoratibiwa na kuweka wazi dira ya mpango wa kusimamia mfumo ya usimamizi wa kifedha serikalini.

Ukosefu wa maelekezo bayana utapunguza kasi ya kufanikiwa kwa mfumo ya usimamizi wa fedha iliyosanifiwa na yenye gharama nafuu serikalini.

Pia, utasababisha utekelezaji wa usimamizi wa kifedha ulioidhinishwa na serikali ambao haukidhi mahitaji ya taasisi za umma.

Ninapendekeza Wizara ya fedha na mipango kufanya yafuatayo:

- (i) Kutoa agizo kwa sekta na taasisi za umma ambalo litabainisha kanuni na vigezo vya uchaguzi na utekelezaji wa kusimika mifumo ya usimamizi wa fedha serikalini.
- (ii) Kuzitaarifu taasisi na taasisi za umma namna ya kufanya maboresho katika mfumo MUSE ili kukidhi mahitaji ya taasisi zao.

(b) Kukosekana kwa mpango wa utekelezaji wa mfumo wa MUSE

Wakati mapitio ya mfumo wa MUSE, nilibaini kuwa baadhi moduli za mfumo hazijatekelezwa. Moduli hizo ni pamoja na moduli ya ukusanyaji wa mapato. Pia nilibaini kwamba mfumo wa MUSE haujaunganishwa na mfumo wa GePG kwa ajili ya ukusanyaji wa fedha za umma. Nilipouliza, uongozi ulinifahamisha ya kwamba, mfumo bado unatekelezwa.

Niliomba dira ya utekelezaji ili kutathmini hali ya utekelezaji na kuangalia shughuli iliyofanyika na ratiba ya utekelezaji, hata hivyo, hakukuwa na dira wala nyaraka zinazoeleza mpango wa kukamilisha utekelezaji wa mfumo.

Ni maoni yangu kwamba, mfumo wa MUSE ulitekelezwa kwa ajili ya kuwa mfumo wa uhasibu wenye viwango, unaodhibitiwa na wa gharama nafuu kwa taasisi za serikali na kuwezesha utayarishaji wa taarifa za kifedha za pamoja. Hivyo basi, kutokamilisha utekelezaji kwa wakati kutasababisha kuendelea kutumika kwa mifumo ya uhasibu isiyoratibiwa na isiyosimamiwa ambayo ni ya gharama kubwa na haina tija katika kutoa taarifa za kifedha za taasisi za umma.

Ni maoni yangu kwamba, kukosekana kwa dira au mpango wa kutekeleza mfumo wa MUSE kunaweza kuhusishwa na kutokuwa na uhakika kwamba mradi utakamilika, na mfumo utatekelezwa kwa wakati.

Hii pia inazuia utekelezaji wa mifumo mingine muhimu kama vile Mfumo wa majumuisho wa Uhasibu wa Serikali (GACS).

Ninapendekeza uongozi wa wizara ya fedha na mipango kuandaa dira ya utekelezaji wa utendaji uliobaki wa MUSE na kuhakikisha mpango unafuatiliwa.

SURA YA TANO

5.0 UDHIBITI WA USALAMA MTANDAONI

5.1 Udhibiti dhaifu dhidi ya shambulio la ransomware

Ransomware ni aina ya programu ambayo hutumiwa na wadukuzi kwa lengo la kuficha mafaili ya mwathirika na kumtaka alipe kiasi cha fedha kama masharti au kigezo cha kufunguliwa kwa mafaili yalizofichwa.

Mapitio yangu kuhusu udhibiti wa usalama wa mitandao kwa baadhi ya taasisi za serikali hususan juu ya ufanisi wa ulinzi dhidi ya mashambulizi ya programu haribifu (malware attacks), nilibaini visa vitatu ambapo ransomware ilishambulia taasisi za kiserikali.

Katika kisa cha kwanza, seva za taasisi hizo zilishambuliwa na Ransomware iitwayo RYUK. Ripoti ya tukio hilo inaonyesha kwamba programu hiyo haribifu iliathiri mazingira mbadala ya uzalishaji programu ya kuzuia virusi vinavyoathiri komputa inayoitwa *Kaspersky* na seva za programu za taasisi. Programu hiyo haribifu ilipakuliwa kupitia kompyuta ya wafanyakazi na kuenea katika mtandao wote wa shirika. Shambulio hilo lilisababisha kukosekana kwa huduma katika mifumo muhimu ya matumizi kwa masaa 12.

Katika kisa cha pili, baadhi ya seva katika taasisi zilishambuliwa na Ransomware ambayo iliathiri Mfumo wa Uhasibu na mfumo wa Usimamizi wa Mtaji watu (Human Capital Management Application). Inaonyesha wadukuzi walitumia udhaifu uliokuwa katika huduma inayotumiwa na wafanyakazi kuingia katika kompyuta iliyoko mbali ili kufanya kazi zao (Remote Desktop protocol (RDP)). Shambulizi hilo liliathiri shughuli za usimamizi wa rasilimali watu ambazo ni pamoja na usimamizi wa utendaji kazi, taarifa za mwajiriwa, usimamizi wa likizo, usimamizi wa muda wa ziada, na ugawaji wa mafaili ya kiutendaji. Kwa hiyo, huduma hizi zililazimika kufanywa kwa mikono kwa takribani miezi miwili kwa sababu ya shambulio hili. Hata hivyo, athari za shambulio hilo kwenye kazi za uhasibu na fedha zilikuwa ndog kwa sababu mfumo wa kiuhasibu umehifadhiwa katika sehemu tofauti na ile iliyoathiriwa katika mtandao.

Katika kisa cha tatu, taasisi ilishambuliwa na programu haribifu ambayo iliyaficha mafaili/taarifa na kuyafanya yasipatikane kabisa. Shambulio hilo lilienezwa katika taasisi baada ya mfanyakazi kupakuwa kiambatisho cha barua pepe kilichoambukizwa. Shambulio hilo lilikuwa kubwa sana kwa taasisi kwani nakala mbadala (backup data) zilikuwa zimehifadhiwa katika

sehemu moja na mazingira ya uzalishaji yenyewe. Hii ilisababisha takwimu na mafaili ya programu sita kufichwa (encrypted) katika mazingira ya uzalishaji na katika seva za nakala mbadala (backup servers). Kwa hivyo, taasisi hiyo haikuweza kufanya mrejesho wa taarifa na kusababisha kushindwa kutoa ripoti za taarifa za kifedha (Financial Statements Reports).

Napendekeza uongozi wa taasisi husika kuchukua hatua stahiki katika kulinda taarifa za taasisi dhidi ya mashambulizi ya programu haribifu ikiwa ni pamoja na:

- (a) Kuteua afisa usalama wa habari (information security officer) anayehusika kuandaa na kutekeleza mkakati wa usalama katika taasisi;
- (b) Kufanya mafunzo yanayolenga kutoa ufahamu wa masuala ya uhalifu wa kimtandao kwa wafanyakazi mara kwa mara;
- (c) Kuanzisha miundombinu ya kuhifadhi nakala za taarifa sehemu tofauti na eneo la uzalishaji wa taarifa ili kusaidia urejeshaji wa taarifa pindi inapotokea upotevu wa taarifa katika mazingira ya uzalishaji;
- (d) Kufanya usasaishaji wa programu ya kuzuia virusi (antivirus) katika sehemu kuu moja na kutumia programu za kuzuia programu haribifu (antimalware); na
- (e) Kupitia na kurekebisha udhaifu wa mitandao katika taasisi.

5.2 Udhaifu wa Usalama wa Mifumo ya Kimtandao

Nilikagua taasisi saba za kiserikali kutathmini udhibiti wa usalama wa programu za taasisi na kubaini kuwa programu hazikuwa na namna ya kuficha (encrypt) mawasiliano kati ya mtumiaji na seva na pia hazina namna ya kuthibitisha utambulisho (identity) wa mtumiaji. Pamoja na hilo, niliona moja ya tovuti ya taasisi hiyo ikiwa imeathiriwa na programu haribifu (malware) ambayo ilielekeza watumiaji wa programu za taasisi kwenye wavuti ya wadukuzi (malicious website).

Maoni yangu ni kwamba, kutokuficha mawasiliano kati ya mtumiaji na seva na namna ya kuthibitisha utambulisho wa mtumiaji (digital certificates) katika huduma za tovuti inaweza kusababisha wadukuzi kufanya uharibifu wa mfumo wa kutoa majina kwa kompyuta, huduma nyingine, au vifaa vingine vinavyounganishwa na mtandao (Domain Name System). Hii

itasababisha kuelekeza watumiaji kwenye wavuti za wadukuzi na kuiba data za watumiaji. Pia, mdukuzi anaweza kufanya uhalifu zaidi kama vile kuingiza data isiyoidhinishwa, kufuta au kubadilisha mafaili.

Ninapendekeza uongozi wa taasisi husika kutengeneza huduma salama za wavuti kulingana na mwongozo wa Usalama wa Mifumo wa “eGovernment Security Architecture - Standards and Technical Guidelines” wa Mamlaka ya Mtandao wa Serikali. Aidha, ninapendekeza kuhakikisha wanaanzisha na kuendesha mafunzo juu ya usalama wa mtandao kwa wafanyakazi wao.

5.3 Ukosefu wa mafunzo yakutoa ufahamu wa usalama wa mifumo na mashambulio ya kimtandao.

Kulingana na aya ya 2.3.8.1 ya Mwongozo wa Usalama wa Mifumo wa “eGovernment Security Architecture - Standards and Technical Guidelines” wa Mamlaka ya Mtandao wa Serikali, taasisi za umma zinatakiwa kuanzisha mipango ya kutoa elimu inayohusu usalama mtandaoni kulingana na sera za usalama wa habari za taasisi ya umma na taratibu husika.

Katika ukaguzi wangu wa udhibiti wa usalama wa taarifa ilibainika kuwa taasisi tano za serikali zilikuwa hazijatoa mafunzo yanayojenga uelewa wa usalama mtandaoni.

Maoni yangu ni kwamba, ukosefu wa mafunzo ya ufahamu juu ya usalama mtandaoni huziweka taasisi za serikali hatarini zaidi dhidi ya vitendo vya kihalifu mtandaoni. Hii ni kwa sababu wadukuzi wanaweza kutumia tabia za binadamu ambazo ndizo njia rahisi zaidi zinazoweza kufanikisha mashambulizi hatari ya mtandao.

Niliwasiliana na kutoa mapendekezo kwa uongozi wa taasisi husika kufanyia kazi mapungufu haya.

5.4 Mapungufu katika Sera ya Usalama wa Teknolojia ya habari na mawasiliano

Aya ya 37 (a) ya Sheria ya mamlaka ya Mtandao wa Serikali ya 2019 inazitaka taasisi za umma kutengeneza na kutekeleza sera ya usalama wa TEHAMA ya taasisi pamoja na mpango mkakati wa usalama wa teknolojia ya habari na mawasiliano ambao utatoa dira sahihi ya usimamizi wa masuala ya usalama katika taasisi.

Nilikagua usimamizi na usalama wa TEHAMA na kubaini kuwa, kulikuwa na taasisi nne ambazo hazikuwa na Sera ya Usalama wa Teknolojia ya habari

na mawasiliano iliyoidhinishwa kwa ajili ya kuongoza wafanyakazi katika masuala ya usalama wa habari. Taasisi moja ilikuwa na Sera ya Usalama, ingawa sera hiyo haielezi taratibu za utunzaji wa mali za TEHAMA, usimamizi wa vifaa vinavyoweza kutolewa kwenye kompyuta (removable media), Uteketezaji wa vifaa na taarifa chakavu, udhibiti wa taarifa fiche, na usajili na uondoaji wa usajili kwa watumiaji wa kawaida na wale wenye haki za upendeleo (privileged users).

Maoni yangu ni kuwa kukosekana kwa Sera ya Usalama ya TEHAMA na mapungufu katika sera zilizopo kunaweza kusababisha mapungufu katika usimamizi usiofaa wa masuala ya usalama wa teknolojia ya habari na mawasiliano.

Ninapendekeza kwamba, uongozi wa taasisi husika utengeneze na kutekeleza Sera ya Usalama wa Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Aidha, ninapendekeza kwamba wakague sera za usalama ambazo wanatumia kwa sasa na kuhakikisha kuwa zinajitosheleza kulingana na miongozo na viwango vya mamlaka ya Mtandao wa Serikali.

5.5 Mapungufu katika usalama wa mtandao wa kompyuta

Kulingana na aya ya 2.3.4.6 ya Mwongozo wa Usalama wa Mifumo wa Mamlaka ya Mtandao wa Serikali, taasisi za umma zinahitajika kutenganisha miundombinu ya mtandao wa taasisi katika sehemu tofauti zitiwazo Virtual Local Area Network (VLANS) kulingana na umuhimu wa mifumo yenyewe.

Ukaguzi wangu wa udhibiti wa usalama wa mtandao ulibaini kuwa taasisi tatu za serikali hazijatenganisha miundombinu yao yenye rasilimali muhimu za mtandao na mtandao unaotumiwa na wafanyakazi kwa huduma za kawaida za intaneti. Niligundua pia taasisi nyingine zinakosa nyaraka muhimu za muundo wa mtandao na hazikuwa na taratibu za kusimamia watumiaji wa mtandao.

Maoni yangu ni ni kwamba kutotengwa kwa mitandao kunaweza kusababisha wadukuzi kuingia katika seva zenye mifumo muhimu ya matumizi bila ruhusa maalumu kupitia teknolojia ya kuingia kwenye seva kutokea mbali (remote server access). Kwa kuongezea, muundo huu wa mitandao usiotenganishwa kwa teknolojia ya VLAN unaweza kusababisha kuenea kwa programu haribifu kama vile Ransomware ambayo inaweza kupakuliwa katika mtandao kupitia mashambulio hadaa (phishing attacks).

Ninapendekeza uongozi wa taasisi husika kufanya yafuatayo:

- (a) Kutenga mtandao kwa kutumia teknolojia ya virtual private network (VPN) au kuzitenganisha kwa kuweka katika miundombinu tofauti kama vile seva zinazoshikilia mifumo muhimu ya programu kuwa katika mtandao tofauti wa kibinafsi**
- (b) Kutengeneza muundo wa mtandao kwa kufuata Viwango na Miongozo juu ya Usanifu wa Usalama kutoka mamlaka ya Mtandao wa Serikali.**

5.6 Ukosefu wa maafisa usalama wa TEHAMA.

Kulingana na Aya ya 2.2.2.1 (ii) ya Mwongozo wa Usalama wa Mifumo “eGovernment Security Architecture - Standards and Technical Guidelines” wa Mamlaka ya Mtandao wa Serikali, taasisi za umma zinapaswa kuteua Afisa Usalama wa TEHAMA atakayehusika na usimamizi wa kila siku wa mkakati wa usalama wa TEHAMA, ikiwa ni pamoja na majukumu mengine ya yanayohusiana na usalama wa TEHAMA.

Ukaguzi wangu katika Usimamizi wa Usalama wa Habari katika baadhi ya taasisi za serikali ulibaini kuwa kulikuwa na taasisi kumi ambazo hazina Maafisa Usalama wa Habari wanaohusika na usalama wa TEHAMA na kuhakikisha kuna upatikanaji wa huduma inapohitajika, idhini inafuata utaratibu, na kuhakikisha hakuna uchakachujaji wa taarifa.

Maoni yangu ni kwamba kukosekana kwa afisa usalama wa habari kunaweza kusababisha kutotambuliwa kwa ukiukaji wa usalama wa habari, pamoja na mashambulio ya wahalifu wa mtandao, mashambulizi ya virusi, na majaribio ya uhalifu yasiyoidhinishwa kutoka ndani na nje ya taasisi hiyo.

Ninapendekeza kwamba uongozi wa taasisi husika uteue afisa usalama wa TEHAMA rasmi na kutoa majukumu yake ya kazi ya usalama kulingana na miongozo ya mamlaka ya Mtandao wa Serikali.

5.7 Udhaifu Katika kudhibiti wa kutoa haki za watumiaji wa mifumo

Nilikagua usimamizi wa watumiaji wa mifumo na mitando na kubaini kuwa kulikuwa na taasisi tano ambazo hazikuwa na utaratibu rasmi wa kukagua shughuli zilizokuwa zikifanywa na watumiaji wenye haki zote za kwenye mfumo, akaunti za upendeleo (privileged accounts). Vilevile, taasisi hizo zilikuwa hazikagui rekodi za matukio (Audit trails) kwenye mifumo na walikuwa hawafanyi uhakiki wa mara kwa mara wa haki walizopewa watumiaji kwenye mifumo muhimu. Katika taasisi nyingine, nilibaini kuwa kubatilishwa kwa haki za watumiaji hakufuatwi ipasavyo ambapo ilipelekea

wafanyakazi walioondoka kazini kuendelea kuwa na haki za kuingia katika mfumo wa Uhasibu. Katika hali nyingine, taasisi hiyo haikuwa na taratibu maalumu wa namna ya kumpa mtumiaji usajili na kumuondolea usajili katika mifumo.

Kwa kuongezea, ukaguzi wangu ulibaini kuwa taasisi tano za serikali hazikuwa na mgawanyo wa majukumu kwa watumiaji wa mfumo ambao unabainisha kazi inayotakiwa kufanywa kulingana na majukumu ya mtu husika. Mgawanyo wa majukumu unaoanisha utaratibu wa utendaji kazi na namna mfumo unavyotakiwa kufanya kazi ikiwa ni pamoja na haki za mtumiaji, hutumika kama sehemu ya kumbukumbu ya mfumo, kuwazuia watu kufanya vitendo nje ya majukumu yao na haki zao.

Maoni yangu ni kuwa:

- (i) Kukosekana kwa mapitio ya mara kwa mara ya haki za watumiaji kwenye mifumo pamoja na rekodi za matukio yaliyofanywa na watumiaji wa mifumo zinaweza kusababisha kushindwa kugundua shughuli zisizoidhinishwa kwa wakati unaofaa.
- (ii) Ukosefu wa mgawanyo wa jukumu kunaweza kusababisha mtumiaji wa mfumo kupewa haki zaidi ya majukumu yake ambayo inaweza kusababisha ukiukaji wa mgawanyo wa majukumu katika mfumo.
- (iii) Ukosefu wa nyaraka za usajili wa watumiaji na utaratibu wa kumuondolea usajili katika mfumo hupelekea usahaurifu wa taarifa ya kumuondolea usajili mwajiriwa ambaye ajira yake imefikia kikomo.

Napendekeza uongozi wa taasisi husika:

(a) Kuanzisha na kuhakikisha mgawanyo wa majukumu unatekelezwa kwenye mifumo yote. Mgawanyo unapaswa kuhakikisha majukumu yanayokinzana hayafanywi na mtumiaji mmoja.

(b) Kutekeleza mapitio ya mara kwa mara ya shughuli/matukio katika mifumo na haki za watumiaji wa mifumo na kuandaa tathmini ili kubaini kama shughuli zinazofanyika zinaendana na utaratibu wa utendaji kazi bila ya kutiliwa shaka.

(c) Kuandaa nyaraka za utaratibu wa kuondoa usajili wa watumiaji wa mifumo na kuhakikisha haki za watumiaji na watumiaji wa mifumo mingine zinaondolewa mapema pale ukomo wa ajira unapofikiwa

SURA YA SITA

6.0 UPATIKANAJI, UTENGENEZAJI, UDUMISHAJI NA UTOAJI WA MSAADA WA MIFUMO YA TEHAMA

Mifumo ya Teknolojia ya habari na mawasiliano imekuwa ikitumika katika kuongeza ubora na ufanisi wa shughuli mbalimbali za taasisi za umma. Taasisi za umma zimekuwa zikiwekwa katika upatikanaji na utengenezaji wa mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano ili kuwasaidia katika kufikia maelengo mkakati ya taasisi kwa wakati na kwa ufanisi.

Katika mapitio yangu ya miradi ya upatikanaji, utengenezaji na udumishaji wa mifumo katika taasisi za umma kulingana na miongozo ya Mtandao wa Serikali, nilibaini mapungufu yafuatayo: kutokamilika kwa miradi ya TEHAMA kwa wakati, kutofanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo “UAT”, ukosefu wa nyaraka za mradi, ufuatiliaji dhaifu wa miradi, kutofuatilia gharama, na ukosefu wa uratibu katika kusimamia upatikanaji na matengenezo ya mifumo. Mapitio yangu yalihusisha miradi ifuatayo: Mradi wa MNRT Portal, upatikanaji wa mfumo wa uhasibu wa Navision Baraza la Mazingira la Taida NEMC, mradi wa kituo cha kidigitali kukuza utalii katika mitandao ya kijamii katika Bodi ya Utalii Tanzania, uboreshaji wa mfumo jumuishi wa taarifa za usimamizi wa ardhi (ILMIS) katika wizara ya ardhi, nyumba na makazi, usanifishaji jumuishi, uhakikisho wa ubora, mradi wa mfumo wa mitaolojia na upimaji (iSQMT) Shirika la viwango Tanzania, na mipango ya maendeleo ya mifumo ya NACTE. Masuala yaliyotambuliwa yamefafanuliwa hapa chini:

6.1 Kushindwa Kufuatilia Gharama za Maendeleo

Aya ya 55 ya IPSAs 31 inayohusu mali isiyogusika (intangible assets) inayotokana na maendeleo (au kutoka kwa awamu ya maendeleo ya mradi wa ndani) itatambuliwa ikiwa, na ikiwa tu, taasisi inaweza kuonyesha yote hayo, kati ya mengine, uwezo wake wa kiufundi wa kukamilisha mali isiyogusika (intangible assets) ili iweze kupatikana kwa matumizi au uuzaji na uwezo wake wa kupima kwa uhakika matumizi yanayotokana na mali iiyogusika (intangible assets) wakati wa ukuzaji wake.

Wakati nikikagua mifumo ya taarifa katika Wizara ya Fedha na Mipango ilibainika kuwa Wizara haina utaratibu wa ndani wa kufuatilia gharama kwa mifumo ya maombi ambayo ilitengenezwa ndani. Wizara ina mifumo 20 ya maombi ambapo kati yake mifumo 17 ya maombi ilitengenezwa ndani, kwa

ombi la gharama iliyotumika kwa maendeleo ya usimamizi wa mifumo husika ya wizara haikuweza kutoa gharama ya mifumo hii.

Mapitio yangu kama hayo ya mradi wa kukuza Mfumo wa Habari wa Usimamizi wa Mapato (TeRMIS) huko TARURA ulibaini kuwa gharama ya kuunda mfumo haikujulikana kwa sababu ya ukosefu wa utaratibu mzuri wa kufuatilia gharama hizo.

Nina wasiwasi kwamba hii inaweza kuhusishwa na taarifa potofu ya takwimu za mali zisizogusika (intangible assets) katika taarifa za kifedha. Pia, inaweza kusababisha matumizi mabaya ya mfuko huo kutambulika ikiwa hayafuatikani vizuri.

Ninapendekeza usimamizi wa Wizara ya Fedha na Mipango na TARURA:

- (a) Kuhakikisha kuwa gharama ya mradi imewekwa na kuripotiwa kwa ushahidi wa matumizi
- (b) Gharama zimegharimiwa na kuwekwa mtaji ipasavyo ili kuunda thamani ya programu itakayotumika na kuripotiwa katika taarifa za kifedha.

6.2 Kucheleweshwa Kukamilika kwa mradi wa MNRT Portal

Wizara ya maliasili na utalii imeanza kusimika mfumo wa MNRT Portal kuchukuwa nafasi ya mifumo ya binafsi, mifumo ya kitaasisi ya utoaji wa huduma, ukusanyaji wa mapato, na takwimu katika maliasili, tamaduni, na sekta za utalii.

Kwa mujibu wa mpango wa kusimika mfumo (deployment plan), mfumo huo ulitarajiwa kuanza kutumika kuanzia tarehe 18 Septemba, 2018 katika taasisi 16. Hata hivyo, hadi wakati nilipomaliza ukaguzi huu - yaani tarehe 30 Oktoba, 2020 kulikuwa na vipengele vya utendaji kazi vya mfumo (functionalities) na moduli ambazo bado hazikukamilika. Sambamba na hayo, mfumo ulikuwa umesambazwa katika taasisi 12 tu kati ya taasisi 16. Jedwali Na. 8 hapa chini limeainisha kwa ufupi shughuli za mradi ambazo hazijakamilika kulingana na mpango wa utekelezaji wa mradi. Wakati wa ukaguzi nilijulishwa kuwa ucheleweshwaji huu unasababishwa na ukosefu wa fedha na uhaba wa wafanyakazi kupelekwa kwenye utengenezaji wa mfumo.

Jedwali Na. 6: Shughuli zinazosubiri utekelezaji wa mradi wa MNRT Portal

	Shughuli za matengenezo ya mfumo	Mwenendo/hali
1	Huduma ya vibali	90%
2	Huduma ya uwindaji	95%
3	Ripoti	90%
4	Fomu zinazoshabihana	85%
5	Kuweka hifadhi ya kupanda mlima	Inasubiri
6	kuweka hifadhi ya kuona Chimpanzee	Inasubiri
7	Ufuatiliaji wa watalii	90%
8	API - API	90%
9	Nyaraka za mfumo	75%

Chanzo: Ripoti ya hatua ya mradi wa MNRT Portal

Maoni yangu ni kuwa ucheleweshwaji huu unasababisha kuwa na mifumo mingi inayofanya kazi inayofanana kwa taasisi ambazo mfumo wa MNRT Portal haijasimikwa kwani bado wanadumisha mifumo yao ya sasa.

Ninapendekeza menejimentiya wizara Kufanya yafuatayo:

- (a) Kuhakikisha kuwa Mradi wa MNRT unakamilika kwa wakati kwa kuhakikisha fedha za mradi zinapatikana
- (b) Kushauriana na Mamlaka ya Mtandao wa Serikali na vyombo vingine vya serikali kama vile Wizara ya Fedha na Mipango na Benki kuu ya Tanzania kupata watumishi wenye ujuzi na uwezo wa kushiriki katika mradi huo.
- (c) Kuhakikisha usimikwaji wa mfumo kwa taasisi nne zilizobaki

6.3 Utekelezaji usiofanisi wa mkataba wa utoaji wa huduma za kitaalamu na ushauri wa matengenezo ya mfumo wa usimamizi wa barabara za wilaya (DROMAS).

Kwa niaba ya serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, TARURA iliingia mkataba na M/s Cardno IT Transport Marylebone tarehe 16 Agosti 2010 kwa bei ya mkataba wa Paundi za Uingereza 108,925.20 ambazo ni sawa na TSH 269,106,164.00. Sehemu ya nne ya orodha ya vitu vinavyopaswa kufanywa na mzabuni inahitaji muuzaji/mzabuni kuandaa mpango wa uhamishaji wa maarifa na kukabidhi 'source code' za mfumo ifikapo 28 Februari 2019. Wakati sehemu ya tano ya orodha ya orodha hiyo inaeleza kuwa mfumo kamili kiutendaji na makabidhiano ya ripoti za mwisho: Ripoti ya usanifu wa mfumo, mwongozo wa mtumiaji kama inavyotakiwa kwa kujumuisha

marekebisho yote, mwongozo wa msimamizi wa mfumo, na mwongozo wa mafunzo vitakamilika ifikapo tarehe 31 Machi, 2019.

Kinyume cha matakwa haya ya mkataba, tathmini yangu ya usimamizi na uendeshaji wa mfumo kulingana na uwezo wa TARURA kuchukuwa na kumiliki mfumo ikiwa pamoja na ukarabati wa kiufundi, msaada na usimamizi niligundua madhaifu yafuatayo.

- (i) Mzabuni hajakabidhi (source codes) za mfumo kwa TARURA, wala mpango wa kuhamisha maarifa (knowledge transfer road map) haupo, hadi wakati nilipohitimisha ukaguzi huu tarehe 29 Januari 2021.
- (ii) Mwajiri (TARURA) hakuwa amepokea ripoti ya ubunifu/usanifu/muundo wa kina ya mfumo, mwongozo wa mtumiaji kama inavyotakiwa kujumuisha marekebisho yote, na mwongozo wa usimamizi wa mfumo.
- (iii) Mwajiri (TARURA) hana umiliki na udhibiti kamili wa mfumo, hivyo ikiwa kuna mabadiliko yoyote ya mfumo basi lazima amtumie muuzaji/mzabuni kufanya mabadiliko,
- (iv) Ukosefu wa nyaraka zifuatazo kuligana na mahitaji ya miongozo ya Mtandao wa Serikali: nyaraka ya madhumuni na faida za mradi (business case), nyaraka ya maelezo ya mahitaji ya mfumo, Hati za ubunifu/usanifu/muundo wa mfumo, nyaraka ya vipengele vya mfumo vinavyotakiwa kujaribiwa- 'Test Cases', na Ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo(UAT) kwa DROMAS 2.

Maoni yangu ni kwamba madhaifu yaliyotambuliwa yanatishia uendeleu wa mfumo na kukosekana kwa thamani ya pesa kwa rasilimali za Serikali zilizowekezwa

Ninapendekeza uongozi wa TARURA kuhakikisha:

- (a) Muuzaji/Mzabuni anahamisha taarifa kwa kitengo cha TEHAMA kwa lengo la kuweza kusaidia na kudumisha mfumo ili kupunguza utegemezi kwa muuzaji/mzabuni wa mfumo.
- (b) 'Source code' zinakabidhiwa kulingana na mkataba.

- (c) Muuzaji anakabidhi ripoti za mwisho: Ripoti ya ubunifu/usanifu/muundo wa mfumo, mwongozo wa mtumiaji kama inavyotakiwa kwa kujumuisha marekebisho yote, mwongozo wa msimamizi wa mfumo, na mwongozo wa mafunzo.
- (d) Nyaraka ya mahitaji ya mfumo, nyaraka ya ubunifu/usanifu/muundo wa mfumo, kesi za majaribio, na Ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo kwa DROMAS 2 iliyotolewa katika mkoa wa Dar es Salaam imeandikwa na kukabidhiwa kwa idara ya TEHAMA ya TARURA kwa marejeo ya baadaye.

6.4 Ukosefu wa ushahidi wa ufanywaji wa majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (UAT) wa MNRT Portal.

Kwa mujibu wa kifungu 2.1.6.1 cha mwongozo wa Mtandao wa Serikali wa utengenezaji, upatikanaji, uendeshaji na utunzaji wa mfumo (eGAEXT/APA/005), taasisi za umma zinatakiwa kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (UAT) ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa mfumo unakidhi mahitaji ya mtumiaji.

Wakati ninapitia utekelezaji wa mfumo wa MNRT portal, nilifuatilia kuhusu ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo na kubaini kuwa hakukuwa na uthibitisho wowote wa majaribio hayo kufanywa.

Maoni yangu ni kwamba kukosekana kwa majaribio ya mfumo humaanisha kwamba hakuna uhakika kwamba mfumo uliosimikwa unakidhi mahitaji ya mtumiaji

Ninapendekeza uongozi wa Wizara ya Maliasili na Utalii:

- (a) Kufanya na kuandaa ripoti ya majaribio ya utenda kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo huo.
- (b) Kurejea miongozo ya Mtandao wa Serikali kwa kufanya na kutunza kumbukumbu za majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (UAT) kwa mabadiliko yoyote ya mfumo.

6.5 Mapungufu katika uboreshaji wa Mfumo wa Usimamizi wa taarifa za Ardhi

Kwa mujibu wa sehemu ya 2.3.2.1 ya viwango vya utengenezaji, upataji, uendeshaji na udumishaji wa mifumo (eGAEXT/APA/005) ya Mtandao wa Serikali inahitaji maombi ya mabadiliko kuanzishwa kwa kujaza fomu ya maombi ya mabadiliko. Fomu ya maombi ya mabadiliko lazima itazame kwa undani jina la mwombaji, cheo chake, tarehe, kitu cha kubadilisha, na maelezo ya ziada ya mabadiliko hayo. Fomu zote za ombi la mabadiliko zinapaswa kupitiwa na msimamizi wa kitengo cha TEHAMA na timu ya ukarabati. Kisha, kitengo cha TEHAMA kiinahitajika kufanya uchunguzi wa awali na tathmini juu ya ombi hilo la mabadiliko.

Nilikagua uboreshaji wa mfumo jumuisi wa usimamizi wa taarifa za ardhi (ILMIS) katika Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi, na kubaini mapungufu yafuatayo: -

- (i) Sababu za mabadiliko zilizowasilishwa hazina maelezo ya kina ya mabadiliko kama vile jina la mwombaji, cheo chake, tarehe na maelezo ya ziada ya mabadiliko;
- (ii) Hakuna ushahidi wa mapitio na uidhinishaji wa mabadiliko uliofanywa na Meneja wa TEHAMA na timu ya ukarabati;
- (iii) Nilipitia sababu zilizowasilishwa za mabadiliko na niligundua kuwa baadhi ya sababu zilizotolewa zinaweza kushughulikiwa vizuri kiutendaji badala ya kujumuishwa kuwa miongoni mwa sababu za kuimarisha mfumo;
- (iv) Hakuna ripoti ya uchambuzi wa kiufundi inayoelezea athari zinazoweza kutokana na mabadiliko hayo. Vilevile, hakuna ripoti ya uchambuzi wa athari kwa mabadiliko, ili kuthibitisha rasilimali zinazohitajika na mpango wa utekelezaji wa mabadiliko hayo; na
- (v) Kutoainishwa kwa vipengele vinavyotakiwa kufanyiwa majaribio na watumiaji (test cases) vinavyofungamana na mahitaji ya mfumo ili kujiridhisha juu ya ufanisi wa mfumo wakati wa majaribio ya utendaji kazi wa mfumo.

Ni maoni yangu kuwa mapungufu yaliyoorodheshwa hapo juu yanaweza kusababisha kusimikwa kwa mfumo ambao haufungamani na mahitaji ya watumiaji wa mfumo.

Ninapendekeza uongozi wa Wizara ya Ardhi Nyumba na Makazi:

- a) Kuunda na kutekeleza taratibu za usidhibiti wa mabadiliko katika mifumo;
- b) Kuandaa mahitaji ya watumiaji wa mfumo kwa mabadiliko yanayotarajiwa kutekelezwa na kuhakikisha idara za watumiaji zinasaini mahitaji haya;
- c) Kuandaa nyaraka ya mpango wa majaribio na vipengele vinavyotakiwa kujaribiwa ili kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya utumiaji wa mfumo yanazingatiwa na kushughulikiwa na mfumo unaotarajiwa; na
- d) Kupitia na kurekebisha nyaraka za usimamizi na utumiaji wa mfumo kujumuisha mabadiliko ambayo yanatekelezwa.

6.6 Mapungufu ya mradi wa usanifu na utengenezaji wa mfumo wa usimamizi wa taarifa za uchunguzi (CIMIS)

Nilikagua mradi wa usanifu na utengenezaji wa mfumo wa usimamizi wa taarifa za uchunguzi katika Mamlaka ya Mapato (TRA) na kubaini kuwa mfumo uliotekelezwa haujajumuisha mahitaji yote kama ilivyotakiwa toka idara ya watumiaji wa mfumo, mahitaji hayo ni pamoja na ukusanyaji wa ushahidi, ufuatiliaji wa upelelezi ulipofikia, nyaraka za matokeo ya kesi, kesi zilizofungwa, na hitimisho kwa kila kesi iliyokamilika.

Kwa kuongezea, niliomba nyaraka ya mahitaji ya mfumo, mpango kazi wa mradi, na majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (User Acceptance Test) ili kuhakikisha kama utekelezaji wa mradi huo unafuata mwongozo wa Mtandao wa Serikali wa upatikanaji, utengenezaji na ukarabati wa mifumo. Hata hivyo, nyaraka hizo hazikupatikana.

Maoni yangu ni kwamba mapungufu haya yanaweza kusababisha kutofaulu kwa mfumo wa CIMIS kufikia malengo yaliyokusudiwa na kukosekana kwa thamani ya pesa kwa rasilimali zilizowekezwa. Aidha, maoni yangu ni kwamba ukosefu wa nyaraka kunaondoa uthibitisho kuwa taratibu za kusimamia mradi zilifuatwa na kusababisha ugumu katika kusimamia na kuboresha mfumo katika siku za usoni.

Ninapendekeza uongozi wa TRA:

- (a) Kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya watumiaji wa mfumo ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa ushahidi, ufuatiliaji wa mwenendo wa uchunguzi, nyaraka za matokeo ya kesi, kesi zilizofungwa, na hitimisho kwa kila kesi iliyokamilishwa zinatekelezwa,
- (b) Kutengeneza mpango wa mradi ambao unataja hatua muhimu, hali/mwenendo wa shughuli, na kuhakikisha ufuatiliaji wake ni endelevu, na
- (c) Kuwandika vizuri muundo wa mfumo, vipengele vinavyotakiwa kujaribiwa, na kuandaa programu za kufanya majaribio.

6.7 Mapungufu katika usimamizi na ufuatiliaji wa mradi wa mfumo wa ISQMT

Mfumo wa Usanifishaji Jumuishi, Uhakiki wa Ubora, Metrolojia na Upimaji (iSQMT) ni mfumo wa uliochukuwa nafasi ya mfumo wa usimamizi wa ubora wa shirika la viwango (TBS) wa QUALIMIS na mifumo mingine ya metrolojia na upimaji.

Baada ya kupitia mradi huu nilibaini mapungufu yafuatayo:

- (i) Majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (UAT) hayakuhusisha mahitaji yote ya kiutendaji ya mfumo yaliyoainishwa katika nyaraka ya mahitaji ya mfumo 'System requirements specification'. Mahitaji 139 tu ndiyo yalifanyiwa majaribio kati ya mahitaji 220 ya kiutendaji ya mfumo yaliyoainishwa kwenye nyaraka ya mahitaji ni mahitaji.
- (ii) Hakukuwa na ushahidi kwamba vipengele vinavyotakiwa kujaribiwa vya utendaji kazi wa mfumo ambavyo havikufaulu na kutoa zao lililokusudiwa vilijaribiwa tena na kuthibitishwa na watumiaji. Kati ya mahitaji ya mfumo 139 ya utendaji yaliyojaribiwa, 46 yalishindwa majaribio, na 12 hayakujaribiwa kabisa kwa sababu ya kutokamilika kwa maeneo husika ya utendaji wa mfumo.
- (iii) Ukosefu wa mpango mpya wa mradi baada ya mpango wa awali kupitwa na wakati, kwa hivyo, haikujulikana ni shughuli zipi ambazo hazijatekelezwa na wala muda wa utekelezaji wake.

- (iv) Kutofanyika kwa tathmini ya kugundua udhaifu wa usalama wa mifumo (vulnerability assessment).

Maoni yangu ni kwamba udhaifu huu unaweza kusababisha kutofaulu kwa mradi kufikia malengo yake yanayotarajiwa.

Ninapendekeza uongozi wa TBS:

- (a) Kupitia nyaraka ya uainishaji wa mahitaji ya mfumo (SRS) na ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (UAT) ili kuhakikisha mahitaji ya mfumo ya kiutendaji yanaendana na vipengele vinavyotakiwa kujaribiwa ili kutambua mahitaji ya mfumo ya kiutendaji ambayo hayajajaribiwa;
- (b) Kuhakikisha vipengele vinavyotakiwa kujaribiwa ambavyo havikufaulu majaribio na vile ambavyo havikujaribiwa kwa sababu ya kutokamilika kwa utekelezaji wa baadhi ya vipengele vya utendaji kazi wa mfumo vinajaribiwa, na matokeo ya majaribio yanathibitishwa na watumiaji;
- (c) Kuboresha mpango wa mradi kwa kubainisha maeneo yaliyokamilika na maeneo yanayosubiri kutekelezwa na muda wake husika; na
- (d) Kufanya tathmini ya kugundua udhaifu wa usalama wa mifumo (Vulnerability assessment).

6.8 Kutozingatia taratibu za kutengeneza mifumo na taratibu za udhibiti wa mabadiliko kwenye mifumo

Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam (DIT) imetengeneza mifumo yake ya ndani kama vile mfumo wa dawati la Msaada (Help desk system), Jukwaa la kidigitali la ujifunzaji (Digital learning platform), mfumo wa usimamizi wa utunzaji wa vifaa (Inventory management system), mfumo wa Wavuti wa Mkutano (Web Conferencing Application - Mconf & BBB) na Mfumo wa Usimamizi wa taarifa za Wanafunzi (OSIM).

Nilikagua mifumo iliyotengenezwa ili kuhakikisha kwamba Taasisi inafuata miongozo ya Mtandao wa Serikali ya utengenezaji, upataji, uendeshaji na udumishaji wa mifumo. Mapitio yangu yaligundua mapungufu yafuatayo:

- (i) Kulikuwa na makusanyo dhaifu ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo ambapo ilibainika kuwa mfumo wa usimamizi wa utunzaji wa vifaa na mali ambao ulizinduliwa mnamo 2017/2018 ulikuwa na rejista ya mali za TEHAMA iliyoingizwa mnamo 11/9/2018 na baada ya hapo hakukuwa na taarifa zingine zilizoingizwa tena. Hii ina maana kwamba mfumo hautumiwi ipasavyo na huenda inasababishwa na mfumo kutokidhi mahitaji ya watumiaji. Kwa kuongezea, ombi la nyaraka ya mahitaji ya watumiaji wa mfumo halikujibiwa hadi wakati wa ukaguzi mnamo 4 Desemba 2020.
- (ii) Mifumo inakosa nyaraka muhimu ikiwa ni pamoja na nyaraka inayoelezea dhumuni, malengo na faida ya mradi, mahitaji ya mfumo, usanifu wa mfumo, mipango ya mradi, vipengele vya mfumo vinavyotakiwa kujaribiwa, ripoti za majaribio ya mfumo, na miongozo ya watumiaji.
- (iii) Pia niliona kuwa mabadiliko yalitekelezwa katika mfumo wa Usimamizi wa taarifaza Wanafunzi (OSIM) tangu kusimikwa kwake, Hata hivyo, taasisi haikuwa ikiandika na kudhibiti/kusimamia kwa ufanisi mabadiliko yaliyotekelezwa.

Ninapendekeza uongozi wa DIT uzingatie Miongozo ya Mtandao wa Serikali kuhusu matengenezo, upataji, uendeshaji na utunzaji wa mifumo ili kutekeleza utengenezaji wa mifumo na utekelezaji wa mabadiliko ya mifumo.

6.9 Upungufu wa Nyaraka za miradi ya TEHAMA

Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) lilifanya miradi mitatu ya TEHAMA mnamo mwaka wa fedha wa 2019/20. Miradi hiyo ilijumuisha uimarishaji wa mfumo uliopo, kutengeneza mfumo mpya, na kutengeneza upya mfumo wa zamani.

Mapitio yangu ya miradi yaligundua mapungufu juu ya kuwapo kwa nyaraka kama vile maelezo ya lengo na faida ya mifumo husika, mpango kazi wa mradi, uainishaji wa mahitaji ya mradi, usanifu wa mfumo, mwongozo wa kiufundi, mwongozo wa mtumiaji, na ripoti ya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo. Pia, nilibaini kuwa Baraza halijaanzisha miongozo ya usimamizi wa miradi ya TEHAMA na miongozo ya upataji wa TEHAMA, na miongozo ya upatikanaji/utengenezaji wa mfumo.

Maoni yangu ni kuwa upungufu wa nyaraka za mradi wa TEHAMA yanaweza kusababisha udumishaji na utoaji wa msaada wa mifumo kuwa hafifu kwa siku za usoni. Pia, ni maoni yangu kwamba ukosefu wa nyaraka sahihi hufanya iwe ngumu kutathmini ufanisi wa mifumo iliyopo.

Ninapendekeza uongozi wa NACTE:

(a) Kuhakikisha nyaraka ya usanifu wa kiufundi kwa mifumo yote zinaandaliwa.

(b) Kuhakikisha idara husika za watumiaji wa mifumo zinashirikiana na kitengo cha TEHAMA kufanya majaribio ya utendaji kazi wa mfumo kwa watumiaji wa mfumo (UAT) ili kuthibitisha mahitaji na matarajio ya mtumiaji wa mfumo uliotengenezwa na pia bila kusahau kuandika matokeo ya majaribio hayo.

6.10 Mapungufu ya mradi wa kituo cha kidigitali cha ukuzaji wa utalii katika mitandao ya kijamii

Nilitathmini utekelezaji wa mradi wa kituo cha kidigitali cha ukuzaji wa utalii katika mitandao ya kijamii katika Bodi ya utalii (TTB) na kubaini mapungufu yafuatayo:

(i) Mpango wa mradi unabainisha kamati ya uongozi/usimamizi inayojumuisha wakilishi mmoja kutoka taasisi zifuatazo: TANAPA, NCAA, TFS, NMT, TAWA na TTB. Mpango ulihitaji kamati kuandaa ripoti za maendeleo ya mradi ya kila mwezi, na kila robo mwaka ili kuripoti utendaji wa mradi. Hata hivyo, kamati hiyo ya mradi haikukutana kama inavyotakiwa.

(ii) Kucheleweshwa utengenezaji na idhini ya viwango na miongozo ya utendaji wa kituo hicho kama Sera ya Maudhui na Mkakati, Mkakati wa Ushirikiano, Mpango wa kampeni ya Media ya Jamii, Usimamizi wa vihatarishi 'risk management', Mkataba wa Mradi, Mpango wa Usimamizi wa Mradi, Mpango wa Usimamizi wa Mabadiliko, Mpango wa Kazi, na Kalenda ya Yaliyomo. Hati/nyaraka na miongozo hii ilitakiwa kukamilika tarehe 30 Juni 2020 kulingana na mpango wa mradi.

(iii) Shilingi, 30,057,066.12 za kitanzania ikiwa ni gharama za ziada zilizotokana na mafunzo ya uelimishaji wa mradi, gharama ya vikao vya bodi ya zabuni, mikutano ya tathmini, na mchakato wa kuwajiri

watumishi wa kituo. Kamati ya usimamizi wa mradi haikuidhinisha mabadiliko haya wakati wa utekelezaji wa bajeti.

- (iv) Mpango wa usimamizi wa mradi haukuainisha ni vipi ada ya kila mwaka ya malipo ya usajili wa mfumo itagawanywa baina ya taasisi za wanachama baada ya kituo kuanza kufanya kazi. Utaratibu wa uhamishaji wa maarifa kwenye utunzaji na kutoa msaada wa mfumo haujaonyeshwa wazi kwenye mpango wa mradi.
- (v) Kuna sintofahamu kuhusu ufadhili wa malipo ya baadaye ya kazi yanayohusiana na mradi huo kuwanzia tarehe 1 Julai 2020, hii inasababishwa na vyanzo vya mapato vya wachangiaji wakuu Mamlaka ya Uhifadhi wa Ngorongoro na Mamalaka ya Hifadhi za Taifa NCAA na TANAPA) kuhamishiwa kwa Mamlaka ya Mapato.

Maoni yangu ni kuwa kasoro zilizobainika zinaweza kuathiri kukamilika kwa wakati kwa mradi wa kituo hiki.

Ninapendekeza uongozi wa bodi ya utalii:

- a) Kuitisha mkutano wa kamati ya usimamizi wa mradi kukagua mwenendo/hali ya sasa ya mradi na kuhakikisha kamati inabaki hai hadi kukamilika kwa mradi;
- b) Kuhakikisha matumizi ya mradi yanaambatana na bajeti iliyopangwa na mabadiliko yoyote au upungufu kutoka kwa bajeti unaidhinishwa na kamati ya usimamizi wa mradi;
- c) Kuandaa na kupitisha viwango vyote vinavyohitajika, miongozo, na nyaraka,
- d) Kutengeneza muongozo ambao unabainisha jinsi gharama za uendeshaji wa kituo cha media zitakavyoshirikiwa/gawanywa katika taasisi sita; na
- e) Kuwasiliana na Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha juu ya kuziba pengo la kifedha ili mradi uendelee kusalia wa muhimu na hai.

6.11 Mapungufu katika Kusimamia Miradi ya TEHAMA ya mamlaka ya Bandari

Kwa mujibu wa Sehemu ya 6.2.3 ya sera ya TEHAMA ya Mamlaka ya Bandari, uundaji na matengenezo yote ya ndani yatasimamiwa kama miradi inayotumia viwango vya matengenezo ya mifumo na utaratibu wa usimamizi wa miradi. Sehemu ya 6.2.4 ya sera hiyo inataka nyaraka zote ziboreshwe mara kwa mara. Kifungu cha 12.1.1 cha sera hiyo hiyo kinaelezea kwamba, kabla ya kuanza kwa mradi wowote, ripoti ya kuwanzishwa kwa mradi inapaswa kuwasilishwa kwa mkurugenzi wa huduma za TEHAMA kisha kwa menejimenti ili kuhalalisha/thibitisha hitaji la mradi na kuleta tija kwenye uwekezaji, na kupitishwa zaidi na mkurugenzi mkuu au bodi ya wakurugenzi.

Sehemu ya 12.1.3 ya sera inahitaji msimamizi wa mradi kuteuliwa na Mkurugenzi Mkuu na msimamizi wa mradi atakuwa msimamizi wa mradi aliyeidhinishwa na vyeti vinavyotambuliwa. Zaidi ya hayo, kifungu cha 12.1.5 na 12.1.6 cha sera hiyo kinahitaji ripoti za maendeleo ya mradi kuwasilishwa mara kwa mara kwa mkurugenzi wa huduma za TEHAMA, kamati ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi, pia, usimamizi wa mabadiliko ya mradi utafanyika kabla na kuanza kwa mradi, wakati wa utekelezaji na baada ya utekelezaji ili kuhakikisha mabadiliko mazuri na umiliki wa watumiaji.

Mapitio yangu ya utaratibu wa usimamizi wa miradi ya Mamlaka ya Bandari yalibainisha udhaifu ufuatao:

- (i) Mamlaka haijaweka viwango au miongozo inayofaa kuwezesha upatikanaji/utengenezaji wa mifumo ya habari kulingana na viwango vya utengenezaji wa mifumo na utaratibu bora wa usimamizi wa miradi.
- (ii) Ukosefu wa ofisi ya miradi au wafanyakazi wenye utaalam wa usimamizi wa miradi ambao watahakikisha uzingatiaji wa taratibu bora na uhakikisho wa ubora wa miradi ya TEHAMA. Kuzingatia sera ya TEHAMA ya Mamlaka inahitaji miradi kusimamiwa na Meneja wa Mradi aliyethibitishwa.

Maoni yangu ni kwamba udhaifu huu unaweza kuhusishwa na ukosefu wa usanifishaji wa taratibu za usimamizi wa miradi ambayo itasababisha kufeli kwa miradi kufikia malengo katika bajeti na ratiba ya nyakati iliyopangwa.

Ninapendekeza uongozi wa mamlaka ya bandari:

- a) Kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mradi wa TEHAMA kulingana na miongozo ya usimamizi wa mradi wa mamlaka ya Mtandao wa Serikali;
- b) Kuimarisha udhibiti ili kuhakikisha mwongozo uliotengenezwa wa usimamizi wa miradi ya TEHAMA unafuatwa;
- c) Kuwanzisha ofisi au sehemu ya miradi chini ya Mkurugenzi wa TEHAMA na uipe vifaa na wafanyakazi waliofunzwa katika ustadi wa usimamizi wa miradi

6.12 Udhaifu wakati wa upataji wa mfumo wa uhasibu wa Navision kutoka NEMC

Baraza la Kitaifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limepata mfumo wa Microsoft Navision ili kusaidia kazi zake za uhasibu.

Katika mapitio yangu ya mchakato wa upatikanaji wa mfumo huo nimebainisha yafuatayo: -

- (i) Hakuna ushahidi unaoonesha kuwapo kwa mahitaji yaliyobainishwa katika mfumo na mtumiaji wa mfumo wala ushahidi wa majaribio ya mfumo yaliyofanywa na watumiaji wa mfumo.
- (ii) Taratibu za udhibiti wa usalama wa mfumo hazijazingatiwa.
- (iii) Kukosekana kwa mgawanyo wajukumu kwenye mfumo ambapo mwanzishaji wa muamala anaweza kuidhinisha muamala aliouanzisha.
- (iv) Utaratibu wa kutoa uwezo kwa watumiaji wa mfumo ya kuweza kuingia katika mfumo haukuzingatia kanuni za mgawanyo wa majukumu. Kwa mantiki hiyo, kulikuwa na watumiaji wengine wa kawaida waliopewa majukumu makubwa ambayo hayakupaswa kuwa ya kwao.

Maoni yangu ni kwamba ukosefu wa mchakato sahihi wa upatikanaji wa mfumo unaweza kusababisha kushindwa kufikia lengo la mfumo au programu iliyopatikana.

Ninapendekeza uongozi wa NEMC: -

- (a) Kuzingatia Miongozo ya Mtandao wa Serikali ya uundaji/utengenezaji, upataji, uendeshaji, na udumishaji wa mifumo wakati wa mchakato wa upatikanaji wa mfumo;
- (b) Kuhakikisha kwamba ruhusa kwa watumiaji wa mfumo ya kuweza kuingia katika mfumo imetolewa kwa usahihi kulingana na majukumu ya watumiaji;
- (c) Kuboresha udhibitiwa usalama, kuhakikisha mgawanyo sahihi wa majukumu kwenye mfumo

SURA YA SABA

7.0 UJUMUISHI, MATUMIZI NA UWIANISHI WA MIFUMO

7.1 KOTOKUWAPO KWA UJUMUISHI BAINA YA MIFUMO MIKUU YA TEHAMA YA SERIKALI

Kwa mujibu wa kifungu cha 2.4 cha mwongozo wa mpango Mkakati wa kielektroniki wa serikali (e-Government strategies), kati ya Maswala muhimu ya Utekelezaji na Utendaji yenye changamoto ni, kutokuwa na miundombinu ya TEHAMA nchi nzima iliyotengenezwa na serikali na kujumuishwa iweze kuwasiliana na ikasanifishwa. Jambo hili linapelekea kukosekana kwa usawa kwenye mifumo ya TEHAMA ambayo huongeza gharama za msaada na matengenezo. Kifungu cha 3.4 cha mpango Mkakati wa kielektroniki wa serikali (e-Government strategies) kimeelezea malengo ya kimkakati ya serikali ambayo ni pamoja na kutoa suluhisho jumuishi, lililo salama na ubunifu ili kuwezesha utoaji wa huduma bora na uboreshaji wa michakato ya kazi.

Wakati wa ukauzi wangu wa ufanisi wa vidhibiti vilivyopo kwenye mifumo tofauti ya serikali, nilibaini kuwa mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na taasisi za serikali haijajumuishwa na mifumo mingine mikubwa ya serikali. Katika ukaguzi wangu nilibaini mambo yafuatayo:

7.1.1 Kutokujumuishwa kwa mfumo wa manunuzi pamoja na Mifumo mengine ya Serikali

Mfumo wa manunuzi serikalini (TANePS) ni mfumo ambao hutumika kusimamia shughuli za ununuzi katika tasisi za serikali. Nilikagua mfumo wa TANePS uliopo Mamlaka ya udhibiti wa manunuzi katika sekta ya umma (PPRA) na kubaini kuwa, mfumo huo haujajumuishwa na mifumo ya bajeti: PLANREP kwa Halmashauri na CBMS kwa serikali kuu na haijaunganishwa na MUSE ambao ni mfumo wa uhasibu unaoshughulikia matumizi ya serikali pamoja na malipo ya wauzaji. Kwa kuongezea, nilibaini kuwa mfumo haujajumuisha na GPPSA kwa utambuzi wa wakati halisi na kuondoa wauzaji waliozuiliwa.

Nina wasiwasi kuwa, kutokujumuishwa kwa mfumo wa TANePS na mifumo ya MUSE, PLANREP, CBMS, na GPSA kunaweza kusababisha manunuzi kufanyika nje ya bajeti iliyopangwa na serikali, wauzaji kulipwa malipo

yasiosahihi na yasiyoidhinishwa, na utoaji wa zabuni kwa wasambazaji wasio na sifa.

Ninapendekeza uongozi wa PPRA kuwasiliana na wizara ya fedha na mipango, TAMISEMI, na GPPSA kwa dhumuni la kuandaa utaratibu wa kujumuisha mfumo wa TANEPS na mifumo ya MUSE, PLANREP, CBMS na GPSA ili kuhakikisha usimamizi mzuri wa mchakato wa manunuzi.

7.1.2 Kutojumuishwa kwa mfumo wa TANEPS na mfumo wa e-Payment Gateway (GePG)

Aya ya 44 (1) ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 inataka pesa zote za serikali kukusanywa kupitia Lango la Malipo ya Serikali(e-Payment Gateway (GePG)), na aya ya 44 (2) ya Sheria hiyo inawaamuru Maafisa Masuuli kuhakikisha kuwa pesa zote za serikali zinakusanywa kupitia Lango la Malipo ya serikali (GePG).

Kinyume na mahitaji ya hapo juu, ukaguzi wangu wa njia za malipo katika mfumo wa TANEPS ulibaini kuwa malipo ya mtandaoni hufanywa moja kwa moja kwenye akaunti ya benki kwa kuhamisha kupitia kadi za benki na benki Mtandaoni bila kupita kupitia lango la malipo ya serikali GePG.

Nina wasiwasi kuwa, ukusanyaji wa mapato/ada nje ya bila kupitia kwenye lango la malipo ya serikali GePG, kunasababishwa na kutokufuata sheria ya Fedha ya mwaka 2017. Pia kunazuia muonekano wa mapato yaliyokusanywa, na kunasababisha PPRA kuingia gharama za kulipa tozo za kibenki.

Ninapendekeza uongozi wa PPRA kuhakikisha kuwa, Mamlaka zinatumia huduma ya GePG kwa malipo ya mtandaoni ili kuhakikisha Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 inafuatwa vyema.

7.1.3 Kutojumuishwa kwa Mfumo wamamlaka ya bandari wa ‘Terminal Operating System’ na mifumo ya TANCIS na TICTS.

‘Terminal Operating System’ ni mfumo ambao unasimamia shughuli za bandari kwa meli za kimataifa zinazoingiza na kutoa mizigo nchini. Mfumo huu una moduli tatu:

- (i) Muonekano wa bandari: Moduli hii inatumika kusimamia vifaa na shughuli zake,
- (ii) Mizigo: kwa kusimamia uhifadhi wa mizigo na utoaji wa vibali, na
- (iii)Bili: kwa kutengeneza ankara za malipo ya bandari.

Moduli zimejumuishwa kupitia jukwaa la kubadilishana ujumbe. Moduli ya bili imejumuishwa na Lango la Malipo ya serikali ya GEPG.

Ukaguzi wangu wa mfumo wa Uendeshaji wa Kituo ulibaini kuwa hakuna mjumuisho kati ya moduli ya mizigo na mfumo jumishi wa forodha (TANCIS) kwenye nyaraka (manifest) iliyowasilishwa TRA. Hati ya sasa imepakuliwa kutoka kwenye mfumo wa TANCIS na kupakiwa kwenye moduli ya mizigo na maafisa wa TPA. Hati hiyo ipo kwenye hatari ya kubadilishwa taarifa zake kwa kukusudia au kwa kutokukusudia. Nina wasiwasi kuwa kuna uwezekano kwamba baadhi ya maelezo ya mizigo kutoka TANCIS yanaweza yasipakiwe kwenye mfumo wa mizigo na hivyo kufanya ufuatiliaji wa mizigo kutokuwezekana. Kwa mfano, wakati wa ukaguzi nilibaini visa viwili ambavyo idadi ya shehena katika mfumo wa mizigo ni chini ya ile iliyopo katika hati dhahiri kutoka TANCIS kama ilivyoelezwa hapo chini.

Jedwali Na. 7: Tofauti ya wingi wa mizigo kati ya mfumo wa mizigo na TANCIS

JINA LA CHOMBO	CALLI D	ATA	ATD	NAMBA YA MIZIGO TOKA TANCIS	IDADIYA MIZIGO TOKA MFUMO WA MIZIGO	KITUO
KOTA MEGAH	13549	29/09/2019	30/09/2019	843	838	TICTS
JENS MAERSK	1474	31/05/2020	17/05/2020	557	539	TICTS

Chanzo: Ripoti ya mfumo wa mizigo na hati kutoka TANCIS

Niligundua pia Mfumo wa TOS haujaunganishwa na mifumo ya TICTS ya kufuatilia kutoka kwa kontena, kupokelewa na kupakiwa kwa kontena kwenye kituo cha TICTS.

Nina wasiwasi kuwa kutokujumuishwa kwa mifumo ya TOS na TANCIS inawezapelekea makosa ya kibinadamu yanayosababisha upoteaji wa mapato bandarini kwani mizigo mingine inaweza isiingizwe katika mfumo wa mizigo kutoka TANCIS. Kwa kuongezea, kutokujumuishwa na mifumo ya TICTS husababisha ufuatiliaji usiofanisi wa kontena zilizotolewa, zilizowasili, zilizopokelewa, na zilizopakiwa kwenye kituo cha TICTS.

Ninapendekeza uongozi wa Mamlaka ya Bandari:

- (a) Kujumuisha moduli ya mizigo na mfumo wa TANCIS ili kuepuka upakiaji wa manifesto usiokuwa wa kiautomatiki.

(b) Kujumuisha mfumo wa TOS na Mifumo ya TICTS ili kufuatilia utokaji wa makontena, upokeaji na upakiaji kwenye kituo cha TICTS

7.1.4 Ujumuishaji usio fanisi kati ya mfumo wa EFDMS na e-filling

Kifungu cha 67- (1) cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (Sura ya 148), Sheria Kuu iliyofanyiwa marekebisho toleo la 2019 inasema kwamba, jumla ya kodi ya ongezeko la thamani inayolipwa na mtu anayepaswa, kulingana na kipindi cha ushuru itahesabiwa kwa: (a) kujumlisha ushuru wote wa pato ambao unalipwa na mtu katika kipindi hicho cha ushuru, (b) kutoa mikopo yote ya ushuru ya pembejeo inayoruhusiwa katika kipindi hicho cha ushuru, na (c) kurekebisha kiwango kilichobaki kwa: (i) kuongeza marekebisho yote yanayohitajika kufanywa katika kipindi hicho cha ushuru, na (ii) kutoa marekebisho yote yanayoruhusiwa katika kipindi hicho cha ushuru.

Nilikagua mfumo wa EFDMS na mfumo wa ITAX ili kutathmini ufuatwaji wa sheria iliyotajwa hapo juu na kuhakikisha kuwa TIN ya mnunuzi katika risiti ya EFD imenaswa kiotomatiki ili kuweza kuhesabu jumla ya VAT. Ukaguzi wangu umegundua kasoro zifuatazo katika taarifa iliyotolewa kwenye z-ripoti ya kutoka EFDMS.

- (i) Kuwapo kwa miamala ambayo inakosa TIN ya Mnunuzi, hii inamaanisha kuwa mfumo hauwezi kurekodi kiotomatiki kiwango cha ushuru wa VAT kwa Mnunuzi. Kwa hivyo, mpaka mnunuzi aweke wazi ushuru (input tax) wakati wa uwasilishaji wa mapato ya VAT katika mfumo wa e-filling system, mfumo hauwezi kutambua kiwango cha VAT (input VAT).
- (ii) Mashine za EFD zinazotumia itifaki (protocol) ya 2.0 zinawasilisha kwenye mfumo wa EFDMS jumla ya viwango vya ushuru vya kila siku kulingana na TIN ya muuzaji tu badala ya namba ya TIN na namba ya risiti. Hata hivyo, miamala ya wanunuzi haiwezi kutambuliwa kwenye akaunti za ushuru wa VAT ya kuingiza (input VAT).
- (iii) Miamala 535 katika ITAX ilifanywa kwa kutumia TIN zilizofungwa na miamala kama hiyo ilibainika kwenye mfumo wa EFDMS ambapo kuna miamala iliyofanyika kwa kutumia TIN zilizofungwa.

Maoni yangu ni kwamba, makosa yaliyobainika yamesababishwa na kuwapo kwa baadhi ya vifaa kadhaa vya EFD ambavyo vinatumia itifaki ya

mawasiliano (communication protocol) iliyojitwa na wakati, na mjumuisho duni kati ya mfumo wa EFDMS na ITAX.

Nina wasiwasi kuwa, kasoro zilizobainika hutengeneza mianya ya ulaghai kwa sababu kiasi halisi cha VAT hutafutwa nje ya mfumo. Vivyo hivyo, inatengeneza mwanya wa ukwepaji wa Ushuru kwa kumiliki TIN zaidi ya moja au kuficha utambulisho wa mlipa ushuru na kuathiri tathmini ya kiasi cha ushuru anachotakiwa kulipa mfanya biashara au biashara iliyofungwa kuendelea kufanya Miamala ya kibiashara.

Ninapendekeza uongozi wa Mamlaka ya Mapato:

- (a) Kuboresha mfumo wa EFDMS kufuatilia TIN ya Biashara, nambari ya stakabadhi ya manunuzi na tarehe ya siku stakabadhi inapotolewa katika EFDMS kupitia mashine za EFD ili kuthibitisha kiasi cha VAT ya kuingiza(input VAT) kwa Wanunuzi wa Biashara na VAT ya Pato kwa mauzo yaliyofanywa,
- (b) Kuanzisha nambari ya kumbukumbu ya muamala kati ya EFDMS na mfumo wa ITAX kwa kutumia TIN za wanunuzi na nambari ya stakabadhi ya ununuzi kwa uhasibu mzuri wa Ushuru wa VAT na ushuru mwingine na c)kuchochea ujumuishaji wa EFDMS and ITAX kuwezesha mfumo wa ITAX kutafuta ushuru wa VAT kiotomati, na kuhakikisha maelezo ya mlipa ushuru yamesawazishwa kwenye EFDMS wakati wowote mabadiliko katika wasifu wa mlipa ushuru yanatokea katika TIN

7.1.5 Ujumuishaji usio fanisi kati ya TANCIS na CMVRS

Nilikagua mifumo ya TANCIS na CMVRS iliyopo mamlaka ya mapato (TRA) ili kutathmini ufanisi wa ujumuishaji uliopo kati ya mifumo hiyo miwili na kubainisha yafuatayo: -

- (i) Magari 167,872 ya IM4 na IM9 yenye thamani ya Sh. 1,365,824,128,727.32 hayakusajiliwa katika mfumo wa CMVRS.
- (ii) Magari 223 yaliyotolewa maelezo kuwa yanasafirishwa (IM8) yamesajiliwa kwenye mfumo wa CMVRS kwa matumizi ya ndani: Ada ya usajili tu ndiyo iliyolipwa katika kusajili magari haya.

- (iii) Magari matano ambayo yaliyotolewa maelezo kuwa yanasafirishwa, yalisajiliwa ndani bila hata kulipa ushuru unaohitajika wa usajili.

Nina maoni kuwa, kasoro zilizobainika zimesababishwa na ukosefu wa mawasiliano kati ya mfumo wa TANCIS na CVMRS.

Nina wasiwasi kuwa kutojumuishwa kwa mifumo ya TANCIS na CMVRS husababisha ukwepaji wa ushuru kwa kusema kuwa magari ni yakusafirishwa wakati yanatumika ndani.

Ninapendekeza kwa uongozi wa TRA:

- (a) Kupitia mjumuisho uliopo kati ya CMRVS na TANCIS na uhakikishe kuwa magari yanayoingizwa nchini kwa matumizi ya ndani yamesajiliwa ipasavyo.
- (b) Wahakikishe kwamba TANCIS inazuia kuonekana kwa magari yanayosafirishwa (IM8) katika mchakato wa usajili ili kusaidia uzingatiji wa taratibu za matumizi ya ndani.
- (c) Kuchunguza kasoro zilizobainika ili kujua kiwango cha ushuru ambacho hakijakusanywa na wakusanye kiwango hicho.

7.1.6 Kutokujumuishwa kwa Mfumo wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha (GBT) na Mifumo mingine muhimu ya serikali.

Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ya Tanzania ina mifumo miwili mikubwa: mfumo wa Leseni za Michezo ya Kubahatisha, Ukaguzi na Utekelezaji (GLICA), mfumo ambao umerahisisha utekelezaji wa majukumu yanayofanywa na Bodi, na Mfumo wa ufuatiliaji Taratibu (Regulatory Central Electronic Monitoring System (GREMS) unaotumika kufuatilia na kudhibiti mapato ya serikali, michezo ya kubahatisha, mwamko wa soko na uwelewa wa biashara zote za michezo ya kubahatisha.

Ukaguzi wangu uligundua yafuatayo katika muktadha wa ujumuishaji wa mfumo:

- a) Mfumo wa GLICA haujajumuishwa na mifumo ya TRA- ITAX kwaajili ya uthibitishaji wa Namba ya kitambulisho cha mlipa kodi (TIN).

- b) GLICA haujaunganishwa na BRELA - Mfumo unaohusika na Usajili wa Biashara na kutoa leseni za biashara.
- c) Mfumo wa GLICA haujajumuishwa na mfumo wa GREMS.

Nina wasiwasi kwamba:

- (i) Kutokujumuishwa kwa mfumo wa GLICA na TRA- ITAX unaweza kusababisha uhakiki wa TIN za waendeshaji wa michezo ya kubahatisha kuwa duni.
- (ii) Ukosefu wa mjumuisho kati ya GLICA na BRELA unaweza kusababisha uthibitisho usiosanifu wa usajili wa biashara ya mwendesha michezo ya kubahatisha na hali ya utoaji leseni.
- (iii) Ukosefu wa muunganiko kati ya mfumo wa **GREMS** na mfumo wa GLICA unapunguza ufanisi wa Bodi katika usimamizi na ufuatiliaji, kama vile kutambua mashine zilizosajiliwa na ambazo hazijasajiliwa ambazo hazitumii data kwa GREMS.

Ninapendekeza uongozi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania: -

- (a) Kujumuisha mfumo wa Leseni za Michezo ya Kubahatisha, Ukaguzi na Utekelezaji GLICA na Mfumo wa GREMS ili kuhakikisha ufuatiliaji mzuri wa waendeshaji wa michezo ya kubahatisha.
- (b) Kujumuisha mfumo wa GLICA na ITAX kuhakikisha uthibitisho wa TIN unafanyika kwa ufanisi.
- (c) Kujumuisha mfumo wa GLICA na BRELA ili kuthibitisha leseni za biashara za waendeshaji wa michezo ya kubahatisha.

7.1.7 Kutokujumuishwa kwa mifumo ya Wakala wa Meli (TASAC) na mifumo ya Mamlaka ya Bandari (TPA)

Shirika la Usafirishaji Tanzania (TASAC) hutumia Mfumo wa Usimamizi wa Biashara ya Usafirishaji (SBMS) kusimamia shughuli za usafirishaji. Hivi sasa, zinatumiwa moduli mbili nazo ni : moduli ya Udhhibiti wa Hati na moduli ya Usafirishaji na usambazaji.

Ukaguzi wangu wa mfumo wa SBMS ulibaini kuwa mfumo hauna udhibiti wa kutosha kuhakikisha kuwa meli zote za usafirishajizinasilisha hati

(manifest) TASAC kabla ya kutia nanga. Nililinganisha ripoti za meli kutoka kwenye mfumo wa TOS ulipo TPA na ripoti kutoka SBMS nakubaini kuwa meli 284 zimetiananga katika bandari za Dar es Salaam, Tanga, na Mtwara toka Novemba 2019 hadi Agosti 2020 bila kuwasilisha nyaraka TASAC. Pia, uthibitishaji wa yaliyomo kwenye nyaraka haufanywi vyema na TASAC kwasababu kuna nyaraka ambazo zina shehena moja wakati nyaraka hiyo ilionekana TPA ikiwa na shehena zaidi ya moja jambo hili linamaanisha kuwa nyaraka hizi hazithibitishwi kwa ukamilifu na TASAC.

Nina wasiwasi kwamba kukosekana kwa udhibiti wa kutosha kuhakikisha meli zote zinawasilisha nyaraka TASAC kabla ya kutia nanga bandarini na ukosefu wa uthibitisho wa nyaraka za usafirishaji kunaweza kusababisha usimamizi usiosanifu wa shughuli za kutia nanga.

Ninapendekeza uongozi wa wakala wa meli:

- (a) Kuimarisha Udhibiti wa Mfumo wa SBMS kuhakikisha meli zote za kimataifa zinazotia nanga kwenye bandari zetu zinawasilisha nyaraka zote zinazohitajika.**
- (b) Kuunganisha SBMS na Mfumo wa TPA (Terminal Operations System) ili kuwezesha TASAC kuona kwa wakati halisi wa laini zote za usafirishaji kugundua vyombo ambavyo havijawasilisha nyaraka zinazohitajika.**
- (c) Kuanzisha utaratibu wa kuthibitisha yaliyomo kwenye nyaraka hizo kwa ukamilifu.**

7.1.8 Kutokujumuishwa kwa mfumo wa MNRT Portal na mifumo mingine ya Serikali.

Wizara ya Maliasili na Utalii imeanza kutumia mfumo wa MNRT portal uliochukuwa nafasi ya mifumo iliyopo kwenye taasisi mojawoja zilizopo chini ya wizara, inayotumika katika ukusanyaji wa mapato, na kukusanya takwimu za maliasili, tamaduni, na sekta za utalii.

Nilikagua mfumo wa MNRT portal na kubaini kuwa kuna ucheleweshwaji wa utekelezaji wa mpango wa Wizara wa kujumuisha mfumo huu na mifumo mingine ya serikali kama vile CMVRS: kwa uthibitishaji wa usajili wa magari, DLS: kwa uthibitisho wa leseni ya udereva, BRELA: kwa uhakiki wa usajili wa Leseni ya Biashara, UHAMIAJI: kwa kuthibitisha uraia wa watalii, TMA:

kwa kutoa taarifa za hali ya hewa kwenye vituo vya utalii, NIDA: kwa uhakiki wa uraia, NBS: kwa kukamata na Kuripoti takwimu za watalii, na TIRA-MIS: kwa uthibitisho wa bima ya gari. Pia hadi wakati wa kumaliza ukaguzi huu, Wizara haikuwa na mpango wa kujumuisha mfumo huu wa MNRT porta na mfumo wa uhasibu wa Serikali: MUSE.

Nina wasiwasi kwamba, kutokuunganishwa kwa mfumo wa MNRT portal na mifumo iliyoainishwa hapo juu inaweza kusababisha kutokuwa na ufanisi na usumbufu katika kusimamia shughuli za maliasili, utamaduni, na utalii kwa sababu ya kuthibitisha taarifa nyingi nje ya mfumo huo.

Ninapendekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kuharakisha utekelezaji wa uunganishaji uliopangwa kwa kuwasiliana na vyombo husika na kuandaa miongozo ya uunganishaji na kila mfumo na kuanzisha utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mwongozo huo.

7.1.9 Kutokujumuishwa kwa mfumo wa MOLIS na GePG

MOLIS ni mfumo unaotumika na Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi ya Watu (MLHSD) kwa usimamizi wa ardhi. Mfumo huu una matoleo mawili, MOLIS: hutumiwa Manispaa ya Kigamboni, Temeke, na Ilala, na MOLIS: v3 inatumika katika mikoa mingine tofauti na Dar es salaam.

Ukaguzi wangu wa mfumo wa MOLIS ulibaini kuwa mchakato wa ulipaji unafanywa nje ya mfumo katika miamala yote ya ardhi isipokuwa kodi ya ardhi. Afisa wa ardhi anatathmini kiwango kinachopaswa kulipwa kwa muamala husika, anatengeneza ankara, kisha anaenda kwenye moduli ya malipo ya jumla ya GePG kutengeneza bili. Baada ya kupokea ushahidi wa malipo, mhasibu anaweka pesa zilizolipwa kwenye mfumo wa MOLIS ili kutambua malipo ya ada yaliyolipwa.

Maoni yangu ni kwamba, malipo ya bili kufanywa nje ya mfumo kunasababishwa na mfumo wa MOLIS kutokuwasiliana na mfumo wa GePG, Kutoza bili nje ya mfumo kunasababisha kukosea kwa kukusudia au kwa kutokukusudia, makosa ambayo yanaweza kusababisha kuwa na taarifa za malipo zisizo sahihi.

Kwa sababu Wizara inapanga kuanza kutumia Mfumo wa ILMIS mikoa yote nchini, ninapendekeza uongozi kuanzisha utaratibu wa kudhibiti miamala inayofanyika nje ya mfumo kwenye MOLIS na MOLIS V3 hadi mfumo wa ILMIS utakapokuwa unatumika nchi nzima.

7.1.10 Kukosekana kwa mwingiliano kati ya ITAX na Mfumo wa RGS.

Tathmini ya ushuru hufanyika katika mfumo wa ITAX ambapo namba ya malipo huwekwa kwenye kila kiasi kilichotathminiwa. Kisha maelezo ya tathmini: nambari ya malipo na kiwango cha ushuru huingizwa kwa mkono katika Mfumo wa RGS kwa ajili ya ufuatiliaji wa malipo.

Nilikagua mchakato mzima unaofanyika kwenye mfumo wa ITAX na RGS ili kuhakiki ukamilifu wa habari kati ya mifumo hiyo miwili. Nilibaini miamala 341,200 na kiasi cha Sh. 2,880,517,770,581.24 zililipwa kwenye mfumo wa RGS bila kuwa na namba ya malipo inayolingana kwenye mfumo wa ITAX.

Nina wasiwasi kuwa, kasoro zilizoonekana husababisha kupatikana orodha ya mapato isiyo ya kweli, na kuathiri muonekano wa kweli na wa haki wa Taarifa za mapato.

Ninapendekeza uongozi wa TRA kuhakikisha kuwa ITAX na RGS zimeunganishwa ili kuondoa shughuli zinazofanywa nje ya mfumo ambapo nambari ya malipo huingizwa kwa mikono kwenye RGS.

7.1.11 Changamoto za ujumuishaji wa mifumo ya TEHAMA ya Serikali za Mitaa

Mamlaka za Serikali za Mitaa hutumia Mfumo wa Habari wa Ukusanyaji wa Mapato ya Serikali za Mitaa (LGRCIS) kukusanya mapato, IFMS- Epicor ya Uhasibu, Mfumo wa FFARS wa kusimamia vituo (shule za msingi, shule ya sekondari, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, na serikali za vijiji), mapato na matumizi, PlanRep kwa Upangaji wa Bajeti, na mfumo wa GoT-HoMIS kwa kusimamia shughuli za vituo vya afya ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa mapato.

Ukaguzi wangu wa mifumo hii umebaini kuwa kuna mjumuisho usio fanisi kati ya mfumo wa LGRCIS na IFMS-Epicor kitendo hiki kinapelekea kiasi cha mapato kilichopo kwenye mfumo wa LGRCIS kutolingana na kiasi cha mapato kilichopo kwenye mfumo wa IFMS-Epicor. Kwa mfano, nilikagua mapato ya Manispaa ya ilala kwenye mfumo wa IFMS-Epicor na mfumo wa LGRCIS kwa mwaka wa fedha 2017/18 na 2018/19 na kubaini tofauti ya taarifa zilizowasilishwa kwenye mifumo hiyo miwili (viambatisho Na. 1-3).

Hakuna mjumuisho kati ya mfumo wa FFARS na GoT-HoMIS jambo ambalo linapelekea afisa kuhamisha mapato yaliyokusanywa kwenye mfumo wa

GoT-HOMIS kupeleka kwenye mfumo wa FFARS kwa mkono. Kitendo cha kuhamisha kwa mkono taarifa za mapato kinakabiliwa na makosa ya kukusudia na yasiyo ya kukusudia. Kwa mfano, takwimu za mapato zilizoripotiwa katika mifumo kwa vituo sita vya afya kutoka Manispaa ya Ilala kwa mwaka wa fedha wa 2019/20, zinaonyesha kuwa, takwimu za mapato katika mfumo wa FFARS ni kubwa kuliko takwimu za mapato katika mfumo wa GoT-HOMIS kwa vituo vitano vya afya, na takwimu za mapato katika mfumo wa FFARS zipo chini ya takwimu za mapato katika mfumo wa GoT-HOMIS kwa kituo kimoja cha afya. (Kiambatisho Na. 4)

Nina wasiwasi kuwa: -

- (i) Tofauti ya takwimu za mapato kati ya mfumo wa mapato (LGRCIS) na mfumo wa uhasibu (IFMS-Epicor) una-athiri uwasilishaji wa kweli na wa haki wa mapato yaliyoripotiwa katika taarifa za kifedha.
- (ii) Tofauti ya takwimu za mapato kati ya mfumo wa FFARS na mfumo wa GoT-HOMIS unaathiri uwasilishaji wa kweli na wa haki wa mapato yaliyoripotiwa katika taarifa ya kifedha. Inaweza kusababisha ubadhirifu, hususan wakati takwimu za mapato katika mfumo wa FFARS ziko chini ya takwimu za mapato katika mfumo wa GoT-HOMIS.

Ninapendekeza uongozi wa Tamisemi kufanya kazi pamoja na Mamlaka za serikali za Mitaa ku:-

- (a) Pitia na kuboresha mjumuisho kati ya mfumo wa LGRCIS na mfumo wa Uhasibu ili kuhakikisha kuwa mapato yote yaliyokusanywa kutoka LGRCIS yanahamishiwa kwa usahihi kwenye mfumo wa uhasibu.
- (b) Ujumuisha mfumo wa FFARS na GoT-HOMIS ili taarifa ziwezinambazwa moja kwa moja kati ya mifumo hiyo miwili.

7.2 MATUMIZI DUNI YA MIFUMO YA TEHAMA

Tathmini yangu ya matumizi ya mifumo katika kujaribu kuangalia ufanisi wa utendaji na utambuzi wa thamani ya pesa kwa mifumo inayotumiwa serikalini ilibaini kwamba baadhi ya taasisi za serikali hazitumii kikamilifu mifumo kama ilivyoelezwa hapa chini:

7.2.1 Kuwapo kwa Moduli za mfumo zisizotumika

Katika ukaguzi wangu niliufanya mamlaka ya udhibiti wa manunuzi (PPRA), nilikagua hati ya Mahitaji ya Mfumo wa TANEPS na taarifa ya kuanzishwa kwa mfumo (inception report), nakubaini kuwa mfumo uliokamilika unapaswa kuwa na moduli kama vile uzabuni (e-tendering), Mikataba (e-contract management), e-catalogue, Mnada (e-auction). Kwa kuongezea, mkataba ulionyesha kuwa muuzaji alilipwa ili kupandisha, na kujaribu mfumo katika kipindi cha dhamana ambacho ni miaka minne.

Nilikagua hali ya utendaji kazi wa mfumo na kubaini kuwa moduli za mkataba na mnada zilijaribiwa lakini kwa sasa hazitumiki, na moduli ya E-catalogue ilijaribiwa lakini inasubiri kujumuishwa na MSD na Wakala wa Huduma za Ununuzi wa Serikali (GPSA) ili iweze kutumika.

Maoni yangu ni kuwa, miaka miwili ya kipindi cha udhamini kupita bila PPRA kutumia moduli muhimu za mfumo wa TANEPS. Hali hiyo inanyima mamlaka kupata thamani ya pesa na utumiaji wa moduli baada ya kumalizika kwa kipindi cha udhamini utasababisha mabadiliko makubwa kwenye mfumo na kusababisha kuingia gharama za ziada.

Vilevile, wakati wa ukaguzi wangu katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa mazingira (NEMC) nilibaini kuwa licha ya Baraza kununua programu ya uhasibu ya Microsoft Navision kwa takriban Sh. milioni 50 na kuendelea kulipa ada ya matengenezo kwa wastani wa Sh. milioni 102 kwa miaka mitatu ya fedha, 2017/18, 2018/19 na 2019/20, baraza lilitumia moduli moja tu ya ukusanyaji mapato kwenye mfumo wa Microsoft Navision. Hata hivyo, moduli zingine kama vile fedha (cash) na Benki (bank), Vifaa (equipment), madeni (receivables), makusanyo (revenue), manunuzi (purchase) na malipo mengine (other payment) hazikutumika. Jambo hili linapelekea kutokupatikana kwa thamani ya pesa ya mfumo ulionunuliwa.

Kwa kuongezea, wakati wa ukaguzi katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima niligundua kuwa walitumia programu ya SAGE Pastel kusimamia rekodi zake za kifedha. Katika ukaguzi wangu wa programu hiyo, nilibaini kuwa michakato yote ya usimamizi wa hesabu (inventory) ilikuwa ikifanywa kwa mikono wakati programu ina moduli ya kusimamia hisa (inventory). Ni maoni yangu kuwa usimamizi wa hisa (inventory) nje ya mfumo unaongeza hatari ya makosa katika rekodi za hisa (inventory). Jambo hili linafanya usimamizi

wa hisa kuwa mgumu na kuleta hatari ya kuripoti hesabuza za hisa zisizo sahihi.

Ninapendekeza

- (a) Uongozi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kuanza kutumia mfumo wa SAGE Pastel kwa usimamizi wa hisa (inventory). Ikiwa mfumo uliopo haukidhi mahitaji ya taasisi, uongozi unapaswa kuchunguza mfumo wenye sifa wanazozitaka ili waununue.
- (b) Uongozi wa PPRA kuanza kutumia moduli ya mkataba na mnada ili kuhakikisha kuwa maswala ya utendaji yanatambuliwa na kutatuliwa kabla ya kumalizika kwa kipindi cha dhamana. Pia, kufuatilia mchakato wa kujumuisha moduli ya e-catalogue haraka na kuhakikisha kuwa GPSA na MSD zinatimiza majukumu yao katika mchakato huo.
- (c) Uongozi wa NEMC kuhakikisha umahiri na utekelezaji sahihi wa programu ya sasa ya uhasibu na kuhakikisha kila moduli za mfumo zinatengenezwa vizuri na zinatumiwa kikamilifu.

7.2.2 Matumizi duni ya Mfumo wa Usimamizi wa Barabara za vijijini (DROMAS).

TARURA inatumia Mfumo wa Usimamizi wa Barabara za Wilaya (DROMAS) kusimamia hesabu (inventory) za barabara na huduma za matengenezo kama jukumu kuu la TARURA. Moja ya malengo ya msingi ya mfumo ni kufuatilia maendeleo ya mikataba ya ujenzi wa barabara. Kwa usanifu na ukamilifu wa usimamizi wa mikataba, mikataba yote ya kazi lazima irekodiwe katika mfumo wa DROMAS.

Hata hivyo, ukaguzi wangu wa mfumo huu wa DROMAS ulibaini kuwa maelezo ya mikataba hayajarekodiwa vyema katika mfumo. Ulinganisho wetu kati ya maelezo ya mikataba kutoka TANePS na maelezo kutoka DROMAS imebaini kutofanana kwa sampuli za mikoa saba kama jedwali linavyoonyesha hapa chini.

Jedwali Na. 8: Mikataba iliyosajiliwa kwenye TANePS vs DROMAS

		Idadi ya Mikataba	
S / N.	MKOA	VITUO	DROMAS
1	Iringa	40	31

2	Katavi	18	14
3	Lindi	9	31
4	Mara	14	32
5	Mwanza	11	54
6	Njombe	26	41
7	Songwe	9	21

Kwa kuongezea, nilibaini kuwa moduli ya kupanga (planning module) ya mfumo iliyoundwa kusaidia Waratibu wa Mikoa katika kusimamia mipango ya kazi kwa sasa haitumiki.

Ni maoni yangu kuwa, madhaifu niliyoyabaini yamesababishwa na Majaribio duni ya mfumo yanayofanywa na watumiaji (UAT) yaliyotokana na kushindwa kuratibu kwa ufanisi mabadiliko ya taasisi.

Ninaona kwamba TARURA haiwezi kutambua thamani ya pesa ya gharama ya ununuzi, matengenezo, na msaada wa mfumo huu.

Ninatoa mapendekezo kwa Uongozi wa TARURA:-

- (a) Kutathmini na kujua sababu zinazopelekea watumiaji wa mfumo kusita kumtumia mfumo na kuhakikisha kuwa mfumo unatumika vyema kama ilivyokusudiwa,
- (b) Kukamilisha mpangilio wa mfumo na kuhakikisha kuwa moduli zote zinatumika.

7.2.3 Usimamizi duni wa mabadiliko ya utendaji kuhakikisha matumizi fanisi ya mfumo

Ukaguzi wangu wa ripoti na uhibititi wa mfumo katika moduli ya mtazamo wa bandari (harbor view), mizigo na moduli za malipo ya mfumo wa TOS ambao unasimamia shughuli za bandari huko TPA ulibaini kuwa, mfumo huo hautumiwi vyema kusimamia shughuli za taasisi hiyo. Wafanyakazi hawasasishi taarifa kwa wakati katika mfumo, suala hili liligundulika kwa kuwapo kwa mizigo iliyotoka bandarini yenye hadhi ya "iliyosajiliwa" wakati shehena ikiwa imetoka inatakiwa kuwa na hali ya "kutekelezwa (excuted)".

Ushahidi mwingine ni kuwapo kwa meli zilizo na tarehe za kufanya kazi iliyo mbele zaidi ya muda wa kuondoka bandarini. Hali hii inaonyesha kuwa shughuli za meli zilifungwa baada ya tarehe ya kuondoka bandarini. Kwa

kuongezea, michakato mingine kama rekodi za mizigo iliyo pokelewa (receiving tally) na iliyo shuswa (discharging tally) katika mzunguko wa kuagiza na rekodi za mizigo iliyopokelewa (receiving tally) na kupakiwa (loading tally) katika mzunguko wa usafirishaji haukufanywa kwa wakati na kwa utaratibu sahihi, na hivyo kufungua mwanya wa udanganyifu.

Ukaguzi wangu pia uligundua kuwa, mfumo una huduma ambazo zinawezesha shughuli zingine kufanywa na wateja mtandaoni bila ya kutembelea ofisi za TPA, Hata hivyo, huduma hizo hazitumiwi na kusababisha foleni na ucheleweshaji wa kibali cha mizigo. Kwa mfano, Wakala wa usafirishaji/Mmiliki wa Chombo anaweza kuunda Transire kwa mfumo wa POAS kutoka eneo lolote. Hata hivyo, hii inafanywa na Mawakala wa usafirishaji katika ofisi za TPA/OSC. Pia, Utengenezaji wa ankara baada ya IOCD kupitishwa na TRA unaweza kufanywa na wafanyakazi wa TPA mara moja bila kusubiri wateja kupanga foleni ili kuomba huduma hii lakini Wateja lazima wapange foleni kwenye ofisi za TPA kuwasilisha IOCD TPA na kuomba Ankara (invoice).

Nina wasiwasi kuwa kuchelewa kusasisha taarifa katika mfumo, matumizi yasiyofaa na yasiyo sanifu ya mfumo na wateja kushindwa kutumia huduma za mtandaoni kunasababisha ukosefu wa ripoti za kweli kwa ajili ya kufanya maamuzi, ucheleweshaji wa usafirishaji wa mizigo, urasimu usiohitajika, na uzembe wa utendaji.

Ninapendekeza Uongozi wa mamlaka ya Bandari: -

- (a) Kutathmini matumizi yote yasiyokidhi mahitaji ya mfumo wa TOS kisha uanzishe mpango wa usimamizi wa mabadiliko ambao utahakikisha mfumo utakubaliwa na watumiaji na wamiliki wa mfumo, na**
- (b) Kuhakikisha wadau/wateja wa bandari wamepewa mafunzo juu ya matumizi ya huduma zinazopatikana mtandaoni na kuzuia huduma hizo kufanywa katika ofisi za TPA.**

7.2.4 Kushindwa Kutumia Mfumo wa Kompyuta wa Uhasibu

Ni namna bora ya uongozi wa taasisi kuanzisha mfumo mzuri wa udhibiti wa ndani ambao pamoja na mambo mengine, uwekaji wa mfumo wa kisasa wa uhasibu ambao utaimarisha udhibiti mzuri wa usimamizi wa kifedha kwa kutoa taarifa kwa wakati na kufanya maamuzi kwa wakati.

Wakati wa ukaguzi katika Chuo cha Wanyamapori Afrika (CAWM) niligundua kuwa chuo kilinunua kifurushi cha uhasibu cha pastel (pastel accounting package) mnamo 2010 kwa Sh. 32,500,000 kusaidia chuo katika kurekodi Taarifa za kifedha na ripoti za kifedha, hata hivyo kifurushi hicho hakikutumika kamwe. Chuo kinatumia excel kurekodi shughuli za kifedha za chuo hicho.

Nina wasiwasi kuwa, ukosefu wa kifurushi cha uhasibu umesababisha kurekodi taarifa za kiasibu kimakosa, kushindwa kuzuia makosa, na mapungufu ya ushahidi wa uhakiki na kutoa idhini ya taarifa iliyorekodiwa kwenye excel.

Vivyo hivyo, wakati wa ukaguzi wangu uliofanyika EWURA nilibaini kuwa maswala ya uhasibu bado yanafanywa katika ekseli ambapo inachukua muda mrefu kutoa au kupata ripoti zinazohitajika. Hii inapelekea udanganyifu na mabadiliko ya taarifa za kifedha. Wakati wa ukaguzi nilijulishwa na uongozi kwamba, Baraza lina mfumo wa uhasibu wa kompyuta unaoitwa Palladium ERP. Hapo zamani

Baraza lilikuwa likitumia mfumo wa Sage Pastel ERP. Matumizi ya mfumo uliotajwa wa uhasibu unahitaji seva na mtandao thabiti ambao kwa bahati mbaya haupo tangu Halmashauri kuhamia katika majengo ya ofisi ya sasa mnamo Desemba 2019. Hali hiyo ililazimisha Halmashauri kutumia njia zote mbili za mfumo wa uhasibu wa kompyuta na kutumia mikono. Hivi sasa Baraza linashughulikia suala hilo ili kuhakikisha upatikanaji wa mtandao wa kuwaminika na 'server'.

Napendekeza kuwa:

- (a) Uongozi wa CAWM kutumia programu kwa mahitaji yake ya kurekodi taarifa za kifedha za uhasibu, kuongeza usalama juu ya taarifa za kifedha, kupunguza na kugundua makosa yanayotekea wakati wa kutumia mikono, kurahisisha utoaji idhini na ukaguzi wa michakato na zaidi ya hapo kutoa ripoti ya kina ya kifedha kwa ajili ya kutoa maamuzi.**
- (b) Usimamizi wa EWURA CC kununua au kutengeneza na kutumia programu ya uhasibu ili kuboresha ufanisi wa utendaji na kuripoti kwa wakati wa shughuli zake.**

7.3 KUWAPO KWA MIFUMO MINGI INAYOFANYA KAZI ZINAZOFANANA

Kifungu cha 3.1.1 cha Mwongozo wa eGA kinataka taasisi za umma kuzingatia Miongozo ya Usanifu wa Kampuni (e-Government Enterprise Architecture guideline), ili Serikali iweze kupunguza hatari ya kutengeneza mifumo mingi yenye kufanya kazi moja.

Katika ukaguzi wangu, nilitathmini kuwapo kwa mifumo yenye kufanya kazi zinazofanana katika taasisi za serikali ili kupunguza gharama za kutengeneza na kukarabati mifumo. Katika tathmini yangu nilibaini kuwapo kwa mifumo inayofanya kazi zinazofanana kama zinavyoelezewa apa chinni:

Nilikagua mifumo inayotumika katika shughuli za Wizara ya Ardhi (MLHHS) na kubaini kuwapo kwa mifumo mitatu inayotumika kusimamia shughuli za ardhi: MOLIS ambayo inatumika Kigamboni, Temeke, na Manispaa za Ilala, MOLIS v3 ambayo inatumika katika mikoa mingine nje ya Dar es salaam, na ILMIS ambayo inatumika Kinondoni, Ilala, Ubungo, manisipaa ya Temeke na Halmashauri ya Wilaya ya Kigamboni. Wakati wa uchunguzi, niliarifiwa kuwa ILMIS ilinunuliwa kupitia pesa za wafadhili kushughulikia changamoto na udhaifu wa matoleo mawili ya MOLIS na kujaribiwa katika manispaa ya Kinondoni na Ubungo, hata hivyo, haikutolewa kwa matumizi nchini kote. Wakati wa uchunguzi tuliariifiwa na uongozi kwamba wizara inapanga kuzindua (ILMIS) na mifumo mingine iliyopo itaondolewa baada ya ILMIS kuanza kutumika nchini kote.

Pia ukaguzi wangu wa mifumo iliyopo Tamisemi ilibaini kuwa Wizara imetengeneza mifumo kadhaa ili kuboresha shughuli zinazofanya na wizara hiyo. Katika ukaguzi wangu nilibaini kuwapo kwa programu zaidi ya moja zinazofanya kazi sawa kama ilivyoelezwa hapo chini

Jedwali Na. 9: mifumo inayofanya kazi zinazofanana

S/N	Mfumo wa maombi	Kazi	maoni
1	Planrep TiMES (mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini wa Tanzania)	Mfumo unaotumika katika kupanga, kubajeti, kutoa taarifa katika Halmashauri Mfumo wa Ufuatiliaji na tathmini katika Halmashauri (LGAs)	Ufuatiliaji na tathmini ni sehemu ya mchakato wa Bajeti; kwa hivyo Planrep kama zana ya bajeti ilitakiwa kuwa na moduli ya ufuatiliaji na tathmini badala ya kuwa na mfumo tofauti ambao unaongeza shughuli usimamizi, na matengenezo.

S/N	Mfumo wa maombi	Kazi	maoni
2	SIS (mfumo wa shule)	unatumika kukusanya takwimu za shule kama vile mahudhurio ya wanafunzi na maendeleo, idadi ya wanafunzi, walimu, na vitabu	Mifumo hii miwili tofauti hukusanya takwimu za shule ambazo zinaweza kufanywa na mfumo mmoja.
	ASC (sensa ya kila mwaka ya shule)	hutumika kukusanya takwimu kutoka shule za msingi, sekondari, na elimu ya watu wazima kwa kutumia waulizaji maalum,	
3	IFT-MIS	Mfumo wa kusimamia uratibu na kuweka kumbukumbu za ufuatiliaji wa matumizi ya fedha katika Halmashauri. Mfumo pia unafuatilia utekelezaji wa mapendekezo na maagizo ya CAG, PPRA na LAAC.	Hii ni mifumo miwili tofauti ambayo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya CAG, PPRA, na LAAC katika Halmashauri.
	Mgumo unaofuatilia utekelezaji wa Mapendekezo ya kaguzi za serikali (GARI-ITS)	Mfumo unasimamiwa na Mkaguzi Mkuu wa ndani unatumika kufuatilia hali ya utekelezaji wa matokeo ya ukaguzi katika taasisi zote za serikali pamoja na Halmashauri	

Chanzo: Kifungu namba 14 cha mifumo ya PO-RALG

Ni maoni yangu kwamba udhaifu huu umesababishwa na ukosefu wa mipango madhubuti ya kutengeneza na kutumia mifumo ya TEHAMA.

Nina wasiwasi kuwa kuwapo kwa mifumo tofauti inayotumiwa kutimiza kusudio moja ni matumizi mabovu ya rasilimali, na huongeza ugumu wa usimamizi, matengenezo, na msaada kwa watumiaji.

Napendekeza

- (a) Uongozi wa MLHHS kuandaa mwongozo wa utekelezaji wa mfumo wa ILMIS nchini kote mfumo mmoja utumike nchi nzima kwa shughuli za usimamizi wa ardhi, na kupanga uhamishaji mzuri wa taarifa kutoka kwenye mifumo mingine kwenda ILMIS.
- (b) Uongozi wa TAMISEMI kukagua kazi za mifumo iliyopo na kuziunganisha ili kuepusha upatikanaji wa mifumo inayofanya kazi sawa.

7.4 SHUGHULI ZA MUHIMU ZA TAASISI KUTOFANYWA KUTUMIA MIFUMO YA TEHAMA

Matumizi ya teknolojia ni muhimu ili kufanya mchakato au michakato ya kutekeleza majukumu ya Taasisi kuwa myepesi na wenye ufanisi mzuri. Shughuli nyingi zinaweza kuwa otomatiki, pia kufanywa na binadamu katika maeneo ya kimkakati ndani. Utaratibu wa kiotomatiki hupunguza muda wa kukamilisha kazi, na gharama ya kuimaliza kwa mafanikio.

Mkakati wa serikali wa kielektroniki unaelezea maono ya serikali kuwa Serikali madhubuti inayotoa huduma za umma za ubunifu zinazoweza kwa TEHAMA. Miongoni mwa malengo makuu ya maono haya ni kutoa suluhisho jumuisi lililo salama na ubunifu kuwezesha utoaji wa huduma bora na uboreshaji wa michakato ya kazi.

Nilitathmini kitendo cha kubadilisha utendaji kazi wa shughuli muhimu za mashirika ya serikali zinazofanywa kwa mikono kwenda kwenye mifumo na kubaini upungufu ufuatao.

7.4.1 Ukosefu wa mifumo ya kusimamia shughuli za msingi za Taasisi

ETDCO ni kampuni tanzu ya Shirika la umeme Tanzania (TANESCO). ETDCO inahusika na usafirishaji na usambazaji wa umeme. Kulingana na mpango mkakati wa ETDCO 2018-2021, jukumu kuu la kampuni ni kutekeleza upembuzi yakinifu wa mradi, upangaji, kubuni na kutathmini, kuandaa na kufanya kazi ya ujenzi na matengenezo (shughuli za matengenezo ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja) ya mitandao ya Usambazaji.

Mapitio yangu ya taratibu za utendajikazi na mifumo yamebaini kuwa, ETDCO inasimamia rekodi za miradi ya ujenzi na matengenezo kwa njia isiyo na mpangilio, ambayo taarifa za miradi zinakaa katika kompyuta za wafanyakazi na kusababisha ungumu wa kufuatilia kwa ufanisi hali ya miradi, kuandaa bajeti, kufuatilia gharama, kufanya uhakiki wa ubora, na kutoa ripoti kwa ajili ya kufanya maamuzi.

Maoni yangu ni kwamba, TEHAMA inatoa fursa kwa ETDCO kufikia jukumu lake kwa ufanisi na kwa gharama nafuu kupitia njia ya kutengeneza utaratibu wa utendaji kazi unaojiendesha.

Maoni yangu ni kuwa, kushindwa kutengeneza mfumo wa usimamizi wa kumbukumbu za miradi ya usafirishaji na usambazaji kunaweza kusababisha ufanisi duni wa taasisi.

TGDC ni kampuni Tanzania TANESCO inayomilikiwa na serikali ya Tanzania. Ilianzishwa mnamo Desemba 2013 kwa madhumuni ya kuongoza maendeleo ya rasilimali ya jotoardhi nchini Tanzania. Ilianza shughuli zake mnamo Julai 2014 ikiwa na mamlaka ya kuchunguza, kuchimba na kutumia rasilimali za jotoardhi kwa uzalishaji wa umeme.

Ukaguzi wangu wa shughuli za TGDC na teknolojia iliyopo ya kusimamia taarifa za uchunguzi ulibaini kuwa kwa sasa taarifa kama hizo zimehifadhiwa kwenye kompyuta za wafanyakazi ambayo ni vingumu kujumuisha taarifa hizo na kutoa ripoti mara moja zitakazotumika kutolea maamuzi kwa ufanisi. Kwa kuongezea, kwa sababu ya unyeti wa taarifa hizo, utaratibu unaotumika sasa unaziweka taarifa hizo kwenye hatari ya kufikiwa na asieruhusiwa na uchakachujaji wa taarifa hizo.

Ninaamini TEHAMA inatoa fursa kwa TGDC kufikia majukumu yake vyema na kwa njia ya gharama nafuu kwa kupitia utengenezaji wa mfumo itakayosaidia kuhifadhi na kusimamia taarifa hizo. Kwa kuongezea, utengenezaji wa kanzi-data au mfumo wa tehama wa kusimamia uchunguzi uitapunguza hatari ya taarifa kufikiwa na mtu asiye ruhusuwa na kupunguza uchakachujaji wa taarifa.

Maoni yangu ni kuwa, kushindwa kusimamia rekodi za uchunguzi kiautomatiki kunaweza kusababisha ufanisi duni, kufikiwa taarifa na asiye na ruhusa uharibifu wa taarifa.

Ninapendekeza uongozi wa ETDCO na TGDC kwa kushauriana na Mamlaka ya e-GA kutengeneza au kununua mfumo wa kusimamia shughuli za msingi ili kuboresha ufanisi.

7.4.2 Ukosefu wa mfumo wa Uhasibu

Taratibu bora za kijasibu zinahitaji taasisi kuwa na mfumo rasmi wa kompyuta wa kuhifadhi miamala ya kijasibu ili kila muamala uhifadhiwe katika sehemu husika ambao utahakikisha unatoa taarifa za kifedha zenye kuaminika.

Tathmini yangu niliyoifanya katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Julius Nyerere (MJNUAT) ilibainisha kuwa Chuo Kikuu hicho hakina Mfumo wa Uhasibu kwa ajili ya kurekodi na kutunza vitabu vya mapato. Pia tathmini hiyo ilifanyika Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) nakubaini kuwa Taasisi haina mifumo ya kiasibu yenye kujiendesha na ripoti zao za fedha zinategemea Microsoft Excel ambayo inakabiliwa na udhaifu kadhaa kwenye taratibu mambo ya kiasibu.

Ninapendekeza uongozi wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Mwalimu Julius Nyerere (MJNUAT) na Taasisi ya Elimu Tanzania (TIE) kutengeneza/kununua mfumo wa uhasibu ili kuwezesha mchakato mzuri wa kuripoti taarifa za kifedha.

7.4.3 Kukosekana kwa mfumo wa TEHAMA wa usimamizi wa mauzo ya nyumba na ardhi (viwanja)

Mapitio yangu ya mchakato wa mauzo ya ardhi (viwanja) na nyumba katika Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) yalibainisha kuwa Shirika halijaanzisha mfumo wa kompyuta (Software) ambao utashughulikia shughuli za mauzo. Hivi sasa, afisa mauzo hutumia programu ya excel katika kurekodi mauzo. Kwa kuwa mauzo hufanywa kwa mikono, nina maoni kuwa bidhaa inaweza kugawanywa kwa mtu zaidi ya mmoja na hati zinaweza kupotea kwa sababu ya idadi kubwa ya taarifa ndani ya mchakato wa mauzo.

Ninapendekeza uongozi wa NHC kuanzisha mfumo wa kompyuta (Software) ambao utatumika kurekodi mauzo ya nyumba na viwanja

7.4.4 Ukosefu wa Mfumo wa Utafiti na Ushauri

Kifungu cha 4.2 (b) cha Mwongozo wa Sera ya Utafiti wa mwaka 2011 ya MUHAS kinahitaji Chuo Kikuu kuanzisha, kudumisha na kuendelea kusasisha kanzi-data ya shughuli za utafiti. Kutokana na mwongozo huu, taarifa zitakuwa zinachapishwa mara kwa mara kwenye Ukurasa wa Mtandao wa Utafiti wa MUHAS, kuanzisha na kudumisha kanzi-data yenye kufikika inayohifadhi utafiti wa elektroniki ambayo itakuwa na vifupisho na maandishi kamili ya ripoti za utafiti na machapisho mengine yanayohusiana.

Ukaguzi wangu wa mchakato wa biashara wenye kujiendesha huko MUHAS ulibaini kuwa, hakuna kanzi-data wala Mfumo wa Usimamizi wa utafiti na ushauri uliotengenezwa na Chuo Kikuu.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa mfumo wa kuratibu shughuli za utafiti na ushauri unaweza kusababisha ugumu katika ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Utafiti na Ushauri.

Napendekeza kuwa uongozi wa MUHAS kuanzisha mfumo wa TEHAMA wa usimamizi, na kanzi-data kwa shughuli zote za Utafiti na Shughuli za Ushauri.

SURA YA NANE

8.0 UDHIBITI WA JUMLA WA TEKNOLOJIA YA HABARI

8.1 USIMAMIZI HAFIFU WA IDARA YA TEHAMA

Mfumo wa utawala wa TEHAMA ni muundo wa uongozi, mpangilio, na utendaji kazi wa TEHAMA. Kwa kuzingatia mifumo ya utawala taasisi huweza kufanikiwa kutimiza malengo yake kwa ujumla.

Ajenda ya tano ya Serikali ni kuongeza matumizi ya TEHAMA nchini kuwanufaisha wananchi. Wananchi watanufaika endapo taasisi za serikali vinazotumia TEHAMA vitafuata mfumo na miogozo ya TEHAMA kikamilifu. Katika ukaguzi wangu, nilitathmini utoshelevu wa utawala kwenye ya TEHAMA na kubaini udhaifu katika maeneo ya mikakati na sera za TEHAMA, muundo wa kiutawala, utendaji wa kamati za uendeshaji, namna bora ya utendaji na usimamizi wa tathimini ya athari zinawoweza kusababishwa na matumizi ya TEHAMA (TEHAMA RISK).

8.1.1 MAPUNGUFU YA MPANGO MKAKATI NA SERA ZA TEHAMA

(a) Kukosekana kwa mpango mkakati wa TEHAMA

kwa mujibu wa miongozo ya Mtandao wa Serikali ya 2017 kifungu 2.3.1 kinazitaka taasisi zote za umma kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa TEHAMA na kuweka mtazamo bayana juu ya matumizi ya TEHAMA kwa utoaji bora wa huduma na kufikia thamani ya uwekezaji wa TEHAMA. Mpango mkakati wa TEHAMA unatakiwa kulandana na malengo ya taasisi hivyo kusaidia kutimiza malengo ya taasisi.

Nilikagua utoshelevu wa mpango mkakati wa TEHAMA katika Wizara ya maliasili na utalii, kituo cha uhusiano wa kigeni (Center for Foreign Relations), tume ya haki na ushindani (FCC), shirika la utangazazi Tanzania (TBC), wakala wa usajili wa biashara na Leseni (BRELA), kampuni ya uendelezaji wa jotoardhi Tanzania (TGDC), kampuni ya ujenzi na usambazaji wa umeme (ETDCO) na chuo kikuu cha ushirika cha Moshi (MoCU) ili kuangalia uwiano kati ya mipango ya TEHAMA na mipango mkakati ya taasisi, nimebaini kuwa taasisi hazina mpango mkakati wa TEHAMA. Pia nilipitia mipango ya kimkakati ya taasisi hizi ili kuangalia kama zinaonyesha utegemezi wa TEHAMA katika kufikia malengo ya taasisi. Nilibaini kuwa mchango wa TEHAMA haujazingatiwa vya kutosha katika kufanikisha malengo. Kadhalika, kwa mwaka huu wa ukaguzi, taasisi zilichukuwa hatua

mbalimbali kwenye masuala ya TEHAMA hivyo basi mpango mkakati wa TEHAMA ulitakiwa kuwapo kwa ajili ya kuongoza shughuli za TEHAMA.

Maoni yangu ni kwamba kukosekana kwa mpango mkakati wa TEHAMA kuna rudisha nyuma usimamizi wa mfumo unaolenga kuleta tija na ufanisi katika utekelezaji wa mipango ya TEHAMA.

Ninapendekeza uongozi wa wizara ya maliasili na utalii, kituo cha uhusiano wa kigeni (Center for Foreign Relations), tume ya haki na ushindani (FCC), shirika la utangazaji Tanzania (TBC), wakala wa usajili wa biashara na leseni (BRELA), kampuni ya uendelezaji wa jotoardhi Tanzania (TGDC), kampuni ya ujenzi na usambazaji wa umeme (ETDCO) na chuo kikuu cha ushirika cha Moshi (MoCU) kuendeleza mpango mkakati wa TEHAMA ambao unawiana na malengo ya kimkakati ya taasisi kuendana na thamani ya pesa ya huduma zinazotolewa na TEHAMA .

(b) Kukosekana kwa uwiano bayana kati ya mpango mkakati wa TEHAMA na mpango mkakati wa tasisi

Mapitio yangu ya mpango mkakati wa TEHAMA wa TARURA na wizara ya fedha mipango yalibaini kuwa mpango mkakati wa TEHAMA hauna uhusiano wa moja kwa moja na mpango mkakati wa taasisi. Kadhalika, nilibaini kuwa hakuna mpango kazi wa kila mwaka juu ya utekelezaji wa mkakati wa TEHAMA.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa uwiano wa moja kwa moja kati ya mpango mkakati wa TEHAMA na mpango mkakati wa taasisi kunasababisha TEHAMA kushindwa kutoa mchango unaokusudiwa hivyo kushindwa kuonesha thamani ya uwekezaji uliofanywa kwenye TEHAMA na kusababisha taasisi kutotimiza malengo malengo ya kimkakati.

Ninapendekeza yafuatayo kwa uongozi wa TARURA na wizara ya fedha na mipango (a) kupitia mpango mkakati wa TEHAMA na kuhakikisha unawiana na mpango mkakati wa taasisi (b) Kuhakikisha kuwapo kwa mpango kazi wa kila mwaka wa TEHAMA unaotokana na mpango mkakati wa TEHAMA.

(c) Kutofanyika kwa ufuatiliaji na tathimini ya mpango mkakati wa TEHAMA

Kufanya tathimini ni dhana muhimu ya katika kufuatilia utendaji kazi wa

taasisi kulingana na malengo yake. Ni njia muhimu ya kutafakari mafanikio na mapungufu, na pia ni muhimu kupitia tena malengo ya taasisi mara kwa mara ambayo yanaweza kuandaliwa katika nyakati au hali tofauti.

Pia nilikagua mfumo wa kiutawala wa TEHAMA katika bodi ya utalii Tanzania, TARURA, KADCO na wizara ya fedha na mipango na kubaini kuwa mikakati ya TEHAMA haielezi namna na kipindi kinachotakiwa kufanya mapitio ya mkakati na kuratibu ili kuhakihisha malengo yanatimizwa kwa wakati ikiwa ni pamoja kuonesha viashiria vya ufanisi. Hata hivyo hapakuwa na taarifa ya kufanyika kwa ufuatiliaji na tathmini.

Maoni yangu ni kuwa, kutokufanya ufuatiliaji na tathmini ya mpango mkakati wa TEHAMA kutasababisha taasisi kushindwa kufikia malengo yalikusudiwa.

Ninapendekeza uongozi wa bodi ya watalii ya Tanzania kufanya na kutoa taarifa ya ufuatiliaji na tathmini mara kwa mara kama ilivyoelezwa katika mpango mkakati wa TEHAMA.

(d) Kukosekana kwa sera ya TEHAMA na sera zilizopitwa na wakati

Kwa mujibu wa kifungu nambari 1.3 cha mwongozo wa Mtandao wa Serikali wa 2017 inazitaka taasisi za umma kutengeneza na kutekeleza sera ya TEHAMA ili kutoa uelekeo wa upangaji sahihi, maununuzi, usimikaji, utekelezaji, usimamizi na matumizi ya TEHAMA.

Nyaraka ya sera za TEHAMA huwa na taarifa rasmi zilizoratibiwa na kuungwa mkono na viongozi ili kuweka mwelekeo wa taasisi kulingana na mahitaji ya utendaji kazi, sheria na kanuni. Sera hiyo hutoa maagizo ya upangaji sahihi, ununuzi, kupitishwa na utekelezaji, usimamizi na utumiaji salama wa rasilimali za TEHAMA.

Mapitio yangu ya udhibiti wa ndani wa TEHAMA, kampuni ya uendelezaji wa jotoardhi Tanzania (TGDC), Kituo cha Mahusiano ya Kigeni (CFR), Baraza La Kiswahili Tanzania (BAKITA), ukaguzi wa ushirika na shirika la usimamizi (COASCO), Mamlaka ya Udhibiti wa ununuzi wa umma (PPRA) na mamlaka ya maji Singida (SUWASA) ilibaini kuwa TGDC, BAKITA na COASCO hazikuwa na sera ya TEHAMA, kituo cha mahusiano ya kigeni kilikuwa na sera ambayo haijapitishwa wakati PPRA na SUWASA sera zao zilikuwa zimepitwa na wakati. Sera ya TEHAMA ya PPRA haijakaguliwa tangu kuwanzishwa kwake Februari, 2016 ambayo ni kinyume na Kifungu cha 12 cha Sera ya TEHAMA

ya PPRA ambayo inahitaji sera hiyo kukaguliwa kila baada ya miezi kumi na mbili (12).

Maoni yangu ni kwamba taasisi zinaweza kushindwa kutambua athari na faida ya TEHAMA kwa sababu ya kukosekana kwa sera kamili na inayojitosheleza ya TEHAMA. Pia kutokaguliwa kwa sera ya TEHAMA kunasababisha taasisi kutoenda sambamba na mazingira ya sasa kwa sababu ya mabadiliko ya teknolojia, sheria na kanuni ambazo zimekuwa zikijitokeza katika taasisi na serikali kwa ujumla.

Napendekeza

- (a) Uongozi wa TDGC, Baraza La Kiswahili Tanzania (BAKITA) na COASCO kuandaa sera za TEHAMA**
- (b) Uongozi wa mamlaka ya udhibiti wa ununuzi wa umma (PPRA) na Mamlaka ya maji Singida(SUWASA) kukagua mara kwa mara sera ya TEHAMA kuendana na mabadiliko ya mazingira ya teknolojia.**
- (c) Uongozi wa kituo cha mahusiano ya kigeni (CFR) ili kukagua na kupitisha sera ya TEHAMA.**

8.1.2 MAPUNGUFU YA MUUNDO WA VITENGO VYA TEHAMA

Utaratibu thabiti na muundo wa utendaji wa kazi (reporting structure) wa kitengo cha TEHAMA ni muhimu katika utawala ili kuhakikisha mipango ya TEHAMA inafuatwa hivyo kutimiza malengo yaliyokusudiwa katika taasisi. TEHAMA inasaidia taasisi kufikia malengo ya kimkakati, kwa hivyo, ni muhimu kiongozi wa Kitengo cha TEHAMA kutoa taarifa kwa mhusika ambaye kipaumbele chake kikubwa ni utendaji wa kimkakati wa kitengo cha TEHAMA na pia kitengo cha TEHAMA kinapaswa kuwa na uwakilishi katika uongozi wa taasisi kwa ajili ya kufanya maamuzi.

Tathmini yangu ya uongozi na muundo wa utendaji wa kazi wa kitengo cha TEHAMA ilibaini kutokuwapo kwa idara / kitengo cha TEHAMA na muundo usiofaa wa utendaji kazi kwa taasisi za serikali kama ilivyoelezwa hapo chini:

(a) Kutokuwepo na kutorasimisha vitengo vya TEHAMA

Kifungu 21(1) cha sheria ya serkali mtandao, kinazitaka taasisi za umma kuanzisha kitengo cha TEHAMA chenye idadi ya wafanyakazi inayotosheleza

kufanya kazi kwa ufanisi. Pia kifungu nambari 5.3.2 cha miongozo ya Mtandao wa Serikali kinazitaka taasisi za umma kuanzisha kitengo cha TEHAMA ambacho kiongozi wake ataripoti moja kwa moja afisa masuuli.

Ukaguzi wangu wa muundo wa utendaji kazi kitengo cha TEHAMA wa COASCO na TGDC ulibaini kutokuwapo kwa idara / kitengo cha TEHAMA. Wakati ukaguzi wangu wa Kampuni ya Ujenzi na Usambazaji wa Umeme (ETDCO) ulibaini kuwa kampuni ina meneja wa TEHAMA, lakini nafasi hiyo ya meneja haukuwekwa rasmi katika muundo wa utendaji kazi wa kampuni na Mpango wa (scheme of service).

Muundo wa utendaji kazi unahitaji kuwapo kwa mtaalam wa TEHAMA, ambayo ni kinyume na matakwa ya sheria ya Mtandao wa Serikali ya 2019 na miongozo ya 2017. Vivyo hivyo, wakati wa ukaguzi wa Bodi ya Kahawa Tanzania (TCB), nilikagua muundo wa utendaji wa kazi (reporting structure) wa TEHAMA na kubaini kuwa muundo wa bodi ya kahawa hauonyeshi uhusiano wa kuripoti kati ya kitengo cha TEHAMA na uongozi wa bodi, hii inaonyesha kuwa uongozi unaona kitengo cha TEHAMA kama kiwezeshi lakini sio kitengo rasmi cha kimkakati.

Ni maoni yangu kuwa, kukosekana kwa kitengo cha TEHAMA kunapunguza majukumu ya TEHAMA kwenye mpango mkakati wa taasisi. Hii inaweza kusababisha taasisi kuanza mipango na shughuli za TEHAMA ambazo hazijapewa kipaumbele na kusimamiwa ipasavyo, na hivyo kusababisha TEHAMA kushindwa kutoa huduma ipasavyo.

Napendekeza uongozi wa COASCO na TGDC kuanzisha kitengo / idara ya TEHAMA na kiongozi wake anatakiwa kuripoti moja kwa moja kwa afisa masuuli.

Pia napendekeza uongozi wa Kampuni ya Ujenzi na Usambazaji wa Umeme (ETDCO) na bodi ya kahawa Tanzania (TCB) kupitia na kusasisha muundo wa utendaji kazi wa kitengo cha TEHAMA unayoongozwa na meneja anayeripoti kwa afisa wa masuuli na kuwainisha majukumu ya idara.

(b) Mapungufu ya muundo wa kuripoti wa vitengo vya TEHAMA

Nilikagua muundo wa TARURA na kubaini kuwa kitengo cha TEHAMA kinaongozwa na meneja anayeripoti kwa mkurugenzi wa huduma za usaidizi (Business Support Services) kinyume na matakwa ya sheria ya Mtandao wa

Serikali nambari 10 wa mwaka 2019.

Maoni yangu ni kwamba, upungufu uliobainika katika muundo wa kuripoti idara / kitengo cha TEHAMA unadhoofisha mchango wa TEHAMA katika kufanikisha malengo ya kimkakati ya taasisi.

Napendekeza uongozi wa TARURA kurekebisha Muundo wa taasisi na kuweka utaratibu wa Kitengo cha TEHAMA kuripoti moja kwa moja kwa Mkurugenzi Mkuu ili kuharakisha utekelezaji wa mikakati ya TEHAMA.

(c) Upungufu wa watumishi na muundo wa vitengo vya TEHAMA

kifungu cha 21 ya Sheria ya Mtandao wa Serikali ya 2019, kinazitaka taasisi za umma kuanzisha Kitengo cha TEHAMA chenye watumishi wa kutosha kufanya kazi kwa ufanisi.

Kulingana na makadirio ya Wafanyakazi ya Wizara ya Utalii na Maliasili kwa mwaka 2020/2021 kitengo cha TEHAMA kinahitaji jumla ya wafanyakazi 17 kwa utendaji wenye tija. Lakini, kitengo kwa sasa kina wafanyakazi saba kinyume na matakwa ya uanzishwaji kulingana na makadirio ya uhitaji za Wafanyakazi.

Maoni yangu ni kuwa, upungufu wa wafanyakazi wa unaweza kusababisha wizara kutoweza kutekeleza mgawanyo wa majukumu na kutotimiza majukumu mengine kwa wakati na ufanisi unaotakiwa, na kuwapo kwa mfumo wa MNRT kitengo cha TEHAMA kinatoa huduma kwa taasisi 16 na wadau wa nje, hivyo basi upungufu wa wafanyakazi unaweza kusababisha kitengo kutotekeleza shughuli zake ipasavyo.

Napendekeza Uongozi wa wizara ya maliasili na utalii kuhakikisha kitengo cha TEHAMA kinakuwa na watumishi wa kutosha wa kuweza kusimamia shughuli kwa ufanisi.

Vivyo hivyo, ukaguzi wangu wa muundo wa uongozi wa idara ya TEHAMA katika wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ulibaini mkurugenzi anaongoza idara yenye wafanyakazi 18 wa kada ya TEHAMA (Rejea Jedwali 2) kama inavyooneshwa mchanganuo wa mgawanyo wa wafanyakazi. Niligundua pia kwamba idara inashughulikia kazi zote za TEHAMA za kituo cha kitaifa cha taarifa za ardhi (National Land Information Centre), ofisi kuu ya wizara, ofisi za ardhi za mikoa 26 na 185 za halmashauri.

Idara ya TEHAMA pia haina wakurugenzi wasaidizi walioteuliwa kushughulikia usimamizi wa miundombinu ya TEHAMA, utengenezaji wa mifumo na kitengo cha kushughulikia changamoto za idara (support division) licha ya kazi nyingi zilizopo idarani. Timu ya ukaguzi pia ilipitia uboreshaji uliopendekezwa wa muundo wa idara ya TEHAMA ulioandaliwa Machi 2020 na kubaini kuwa haujatekelezwa hadi nilipofanya ukaguzi mnamo Novemba 2020. Hali hii inasababisha hitaji la mkurugenzi kusimamia na kufuatilia kila shughuli hata zile ambazo zingeweza kushughulikiwa na wasaidizi.

Jedwali Na. 10: Mchanganuo wa mgawanyo wa wafanyakazi

S/N	kundi	Idadi ya wafanyakazi
1	Wataalam wa kiufundi wa TEHAMA kwa ajili ya kuhudumia ofisi za mkoa 26	0
2	Usimamizi wa mifumo na seva	2
3	Usimamizi na usaidizi wa mtandao	3
4	Wasimamizi wa kanzidata	1
5	Utengenezaji wa mifumo	4
6	Utawala na usanifu ambapo mmoja wao anastaafu February 2021	2
7	Usimamizi na utoaji wa msaada wa mifumo	6
8	Usalama wa TEHAMA	0

Chanzo: Mgawanyo wa kazi na maboresho ya idara

Ni maoni yangu kwamba, kukosekana kwa wa wakuu wa vitengo /idara kunaweza kusababisha utendaji duni wa idara kwani mkurugenzi atazidiwa na shughuli za kila siku. Utendaji duni pia unaweza kusababisha wizara kutoweza kutekeleza mgawanyo wa majukumu na kushindwa kutimiza malengo kwa wakati na ubora unaotarajiwa.

Napendekeza uongozi wa wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kufuata mamlaka inayoidhinisha ili kuhakikisha kuwa muundo wa idara ya TEHAMA unapitiwa na mahitaji ya wafanyakazi yanaidhinishwa na kutekelezwa ipasavyo.

(d) Wakuu wa Idara/vitengo vya TEHAMA wasio na sifa stahiki

Kifungu cha 21 cha sheria ya Mtandao wa Serikali ya mwaka 2019, kinahitaji kitengo cha usimamizi wa TEHAMA kuongozwa na mtu aliye na sifa stahiki za kitaaluma na uzoefu wa kazi za TEHAMA.

Mapitio ya muundo wa idara ya TEHAMA wa taasisi ya elimu ya watu wazima (IAE) yalibaini kuwa idara ya TEHAMA inaongozwa na meneja ambaye hana

sifa za kitaaluma katika teknolojia ya habari na mawasiliano au taaluma unaohusiana.

Ni maoni kwamba idara kuongozwa na kiongozi asiye na sifa kunaweza kusababisha utendaji kazi duni na usio na kiwango kwa kitengo cha TEHAMA.

Napendekeza uongozi wa Taasisi ya Elimu ya watu wazima kuteua mkuu wa kitengo cha TEHAMA mwenye sifa na uzeofu stahiki

8.1.3 MAPUNGUFU YA KAMATI YA USIMAMIZI WA TEHAMA

Tathmini yangu ya muundo wa utawala wa TEHAMA ilibaini kuwa bodi ya tumbaku ya Tanzania, bodi ya usajili wa wakandarasi, TBC, kituo cha mahusiano ya kigeni (CFR) na ETDCO hazijaanzisha kamati ya uendeshaji wa TEHAMA au kamati ya TEHAMA kwa ajili ya kuhakikisha kazi za TEHAMA zinaleta tija yenye uwiano na uwekezaji uliofanyika.

Maoni yangu kwamba kukosekana kwa kamati ya uendeshaji wa TEHAMA kunasababisha taasisi kushindwa kusimamia vizuri uwekezaji wa shughuli za TEHAMA, kushindwa kutambua uwiano kati ya kazi za TEHAMA na mipango mkakakati ya taasisi ili kuleta tija.

Napendekeza uongozi wa bodi ya tumbaku Tanzania, bodi ya usajili wa wakandarasi, TBC, kituo cha uhusiano wa kigeni (CFR) na ETDCO kuanzisha kamati za uendeshaji wa TEHAMA zilizo na wajibu na majukumu yaliyo bayana.

(a) Kutokuwapo kwa kamati ya usimamizi wa TEHAMA

Tathmini yangu ya muundo wa utawala wa TEHAMA ilibaini kuwa bodi ya tumbaku ya Tanzania, bodi ya usajili wa wakandarasi, TBC, kituo cha mahusiano ya kigeni (CFR) na ETDCO hazijaanzisha kamati ya uendeshaji wa TEHAMA au kamati ya TEHAMA kwa ajili ya kuhakikisha kazi za TEHAMA zinaleta tija yenye uwiano na uwekezaji uliofanyika.

Maoni yangu kwamba kukosekana kwa kamati ya uendeshaji wa TEHAMA kunasababisha taasisi kushindwa kusimamia vizuri uwekezaji wa shughuli za TEHAMA, kushindwa kutambua uwiano kati ya kazi za TEHAMA na mipango mkakakati ya taasisi ili kuleta tija.

Napendekeza uongozi wa bodi ya tumbaku Tanzania, bodi ya usajili wa wakandarasi, TBC, kituo cha uhusiano wa kigeni (CFR) na ETDCO

kuanzisha kamati za uendeshaji wa TEHAMA zilizo na wajibu na majukumu yaliyo bayana.

(b) Kutofanya kazi kwa kamati ya usimamizi wa TEHAMA

Kwa mujibu wa mwongozo wa Mtandao wa Serikali wa 2017 kifungu 2.2.3 (I) hadi (VIII) juu ya mikutano ya kamati, inahitaji kamati ya uendeshaji wa TEHAMA kukutana mara moja kwa kila miezi (3) mitatu.

Katika ukaguzi wangu katika mamlaka ya maeneo maalum ya kuzalisha bidhaa za kuuza nje (Export Processing Zones Authority), niliona ratiba ya mikutano kama ilivyoainishwa katika kamati ya "TOR" ya TEHAMA, ratiba inahitaji mikutano usiyopungua minne kwa mwaka. Lakini, hakukuwa na kikao cha Kamati ya TEHAMA kilichoendeshwa na mamlaka katika mwaka huu wa ukaguzi.

Maoni yangu ni kwamba bila kupitia na kuidhinisha kamati ya uendeshaji wa TEHAMA, uwiano kati ya mipango ya TEHAMA na mpango mkakati hautafikiwa hivyo kusababisha kushindwa kuleta tija stahiki.

Ninapendekeza uongozi wa mamlaka ya maeneo maalum ya kuzalisha bidhaa za kuuza nje (Export Processing Zones Authority) kuhakikisha mikutano ya kamati ya uendeshaji wa TEHAMA unafanywa kulingana na miongozo na kuongeza uelewa kwa wajumbe wa kamati ya TEHAMA juu ya wajibu na majukumu ya kamati katika kufikia malengo ya kimkakati.

(c) Mapungufu ya uundaji wa kamati ya TEHAMA

Mapitio yangu ya miongozo na mikataba ya uendeshaji wa TEHAMA DAWASA nilibaini kuwa kamati ya uendeshaji imejumuisha wajumbe wafuatao: Mkuu wa Kitengo cha Usimamizi wa Mazingira (HEMU) ambaye ni Mwenyekiti, Meneja wa Off-grid & Comm - Sewer ambaye ni Makamu Mwenyekiti, Mkuu wa kitengo cha TEHAMA na Takwimu ambaye ni Katibu na wawakilishi kutoka Idara mbalimbali katika taasisi.

Vivyo hivyo, katika mapitio ya nyaraka ya TEHAMA inayoelezea malengo, wigo wa kazi, shughuli, majukumu ya kufanywa, majukumu husika ya idara ya TEHAMA, na matokeo yanayotarajiwa (terms of reference) katika taasisi ya KADCO nilibaini kuwa kamati hiyo inajumuisha wanachama mwisho watano (5) kutoka kwenye idara / kitengo chochote kile kulingana na muundo wa shirika la KADCO.

Hii ni kinyume na matakwa ya Kifungu cha 18 (1) cha sheria ya mamlaka ya Mtandao wa Serikali ya 2019 ambayo inahitaji kiwango cha chini cha washiriki kiwe sita na kiwango cha juu kuwa saba ikiwa ni pamoja na mjumbe mmoja kutoka katika wizara ambazo DAWASA na KADCO ni sehemu yao.

Maoni yangu ni kuwa, mapungufu katika uundaji wa kamati ya uendeshaji wa TEHAMA imesababishwa na kushindwa kwa kamati tendaji kutekeleza kwa vitendo majukumu yao.

Napendekeza uongozi wa DAWASA na KADCO kupitia upya na kuhuisha mwongozo wa uendeshaji wa TEHAMA (TEHAMA steering charter) ili kuendana na matakwa ya sheria ya mamlaka ya Mtandao wa Serikali ya 2019.

8.1.4 UDHAIFU WA USIMAMIZI WA HATARI ZITOKANAZO NA MATUMIZI YA TEHAMA

Usimamizi wa athari katika TEHAMA ni kitendo cha kutumia utaratibu utumikao katika kudhibiti athari zinginezo, katika mazingira ya TEHAMA ili kudhibiti madhara katika utendaji kazi yanayohusiana na matumizi, umiliki, operesheni, ushiriki na uanzilishaji wa TEHAMA ndani taasisi.

Udhibiti wa athari ni mchakato endelevu kwani mazingira ya biashara na teknolojia yanabadilika kila wakati na udhaifu mpya katika mifumo na teknolojia kwa ujumla huibuka kila siku.

Katika ukaguzi wangu wa namna ya usimamizi wa athari zinazoweza kutokea katika TEHAMA nilibaini mapungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutofanya tathmini ya athari zinazoweza kutokea katika TEHAMA, ukosefu wa rejista ya athari za TEHAMA na kutofuatilia utekelezaji wa mikakati ya kupunguza athari za TEHAMA kama ilivyoelezwa hapo chini:

(a) Ukosefu wa rejista ya hatari zitonazo na matumizi ya TEHAMA

Katika ukaguzi wangu wa mifumo ya Habari niliofanya Bodi ya Tumbaku, Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini (Tarura), Mamlaka ya Bandari Tanzania, Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi (MoCU), nilibaini kuwa hakukuwa na rejista ya athari za TEHAMA kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti athari, ambapo inamaanisha tathmini ya athari katika TEHAMA haijafanyika katika mwaka husika unaokaguliwa. Utaratibu unaopendekezwa ni kufanya

tathmini ya athari angalau mara moja kila mwaka na wakati wowote mabadiliko katika mazingira ya TEHAMA yafanyikapo kwasababu madhaifu mapya ya kiusalama katika mitandao yanagundulika kila mara. Kwa hivyo, tathmini ya athari zinazoweza kutokea yanatakiwa kufanywa ili kukabiliana na athari za TEHAMA zinazoweza kujitokeza.

Maoni yangu ni kuwa, ukosefu wa rejista ya athari za TEHAMA umetokana na kuwapo kwa udhaifu katika mchakato wa kutathmini, kutambua, kuweka kumbukumbu na ufuatiliaji wa athari za TEHAMA. Kwa hivyo, Bodi ya Tumbaku Tanzania, TARURA, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi (MoCU) hawawezi kubuni njia zinazofaa na za kutosha za kupunguza athari ili kuhakikisha usalama wa mali na mikakati ya TEHEMA vinafikiwa.

Napendekeza uongozi wa Bodi ya Tumbaku, TARURA, Mamlaka ya Bandari Tanzania, Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi (MoCU) kufanya tathmini ya athari za TEHAMA na kuanzisha rejista ya athari za ki-TEHAMA ili kugundua na kutafuta njia bora katika kupambana na athari zinazoweza kutokea katika TEHAMA.

(b) Kutofuatilia utekelezaji wa mikakati ya kupunguza athari katika TEHAMA

Wakati wa kukagua usimamizi wa athari za TEHAMA katika taasisi ya NACTE niliomba mpango mkakati wa kupambana na vihatarishi unaoonyesha vihatarishi vya TEHAMA vilivyogundulika NACTE. Kupitia ukaguzi wa nyaraka nilibaini kuwa, ripoti za utekelezaji wa mapambano dhidi ya vihatarishi za robo ya mwaka bado hazijaandaliwa, licha ya rejista ya vihatarishi kuidhinishwa tangu mwezi wa kumi 2019.

Katika ukaguzi mwingine kama huo katika Wizara ya Fedha na Mipango nilibaini kuwa Wizara haina utaratibu wa kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya kupambana na vihatarishi vilivyoainishwa katika rejista ya vihatarishi. Ni wasiwasi wangu kwamba shughuli nyingi katika taasisi za NACTE na Wizara ya Fedha na Mipango hutegemea TEHAMA. Hivyo, kushindwa kupambana na vihatarishi vya TEHAMA kunaweza kuwa na athari mbaya katika shughuli za kila siku.

Ni maoni yangu kwamba kutofuatilia na utekelezaji wa udhibiti wa vihatarishi kunaweza kusababisha madhara katika ufanyaji wa shughuli za kila siku zinazohitaji matumizi ya TEHAMA.

Napendekeza uongozi wa Baraza la taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) na MOFP kuanza utekelezaji wa udhibiti wa vihatarishi vya TEHAMA na kuripoti hali ya utekelezaji mara kwa mara.

8.2 UDHAIFU WA MPANGO WA KUHAKIKISHA HUDUMA ENDELEU NA KUKABILIANA NA MAJANGA

Nilikagua Mpango wa kuwa na huduma endelevu na Mpango wa Kukabiliana na majanga katika taasisi za serikali ili kuthibitisha yafuatayo: kuwapo kwa tathmini ya utoshelevu wa mipango hiyo katika kukabiliana na hitilafu inayoweza kujitokeza katika shughuli mbalimbali, kulinda huduma muhimu katika taasisi kuepokana na athari zinazoweza kujitokeza sababu ya majanga au hitilafu mbalimbali, pamoja na kuhakikisha huduma zinarudi kwa wakati inapotokea majanga. Katika kupitia nyaraka hizi niligundua mapungufu yafuatayo:

(a) Kukosekana kwa mpango wa kuhakikisha huduma endelevu (BCP) na kukabiliana na majanga (DRP)

Mpango wa huduma endelevu kwa taasisi na mpango wa namna ya Kurejesha huduma baada ya majanga kutokea huelezea mchakato na taratibu ambazo Taasisi ya Umma inazo kuhakikisha kwamba kazi/huduma muhimu katika taasisi na shughuli za TEHAMA zinaendelea wakati na baada ya janga

Wakati wa ukaguzi wangu niliona taasisi iitwayo Dar es salaam Maritime Institute (DMI), EPZA, Mamlaka ya Majisafi na usafi wa mazingira Kahama na Shinyanga (KASHWASA), Baraza la Taifa la Ujenzi (NCC), Baraza la Mitihani la taifa Tanzania (NECTA), Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (MUST), Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL), na Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) hazikuwa na BCP wala DRP. Vivyo hivyo, niligundua kuwa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili (MUHAS), Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Tiba (NIMR), na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI) hazikuwa na BCP; wakati Bodi ya Nafaka na mazao mchanganyiko Tanzania (CPB), Chuo Kikuu cha Ushirika moshi (MoCU), Baraza la Kitaifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (IAE) hawakuwa na DRP.

Maoni yangu ni kuwa, kukosekana kwa BCP na DRP kunaweka hatarini taasisi hizi katika kuweza kuhakikisha huduma za ki-TEHAMA na shughuli zinginezo zinazotumia TEHAMA zinaendelea baada ya kutokea kwa tukio lisilopangwa

au janga. Pia, taasisi zinakosa uhakika wa kurejea kwa huduma yanapo tokea majanga.

Napendekeza uongozi wa DMIEPZA, (KASHWASA), NCC, NEMC, MUST, MSCL, NACTE, NIMR na TAWIRI kufanya tathmini ya athari za kitehama zinazoweza kutokea katika taasisi na kutumia tathmini hiyo kutengeneza Mpango wa kuhakikisha kunakuwa na huduma endelevu (BCP) na Mpango wa namna ya kurejesha huduma (DRP) yanapotokea majanga ya ki-TEHAMA. Pia, Uongozi wa CPB, MoCU, NEMC na IAE kutengeneza DRP.

(b) Udhaifu wa mpango wa kuhakikisha huduma endelevu na kukabiliana na majanga

Nilikagua Mpango wa namna ya kurejesha huduma yatokeapo Majanga (DRP) katika Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi na Wizara ya Utalii na Maliasili (MNRT) na kubaini kuwa wahusika wanao takiwa kuhakikisha huduma za TEHAMA zinakuwa endelevu hawajui majukumu yao yaliyo elezwa katika mpango huo. Pia, nilibaini kuwa hakuna majaribio ya DRP yaliyofanyika katika mwaka husika unaofanyiwa ukaguzi. Kwa kuongezea, kiasi cha taarifa ambacho kinaweza kupotea huduma inaporejeshwa baada ya janga(RPO) , na mda ambao unaweza kutumika kurejesha huduma inapotokea janga havikubainishwa katika mipango yao.

Vivyo hivyo, katika ukaguzi wangu wa BCP na DRP nilibaini kuwa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha ya Tanzania ilikuwa na mpango wa kuwa na huduma endelevu (BCP) uliokwishwa mda wake wakutumika. mpango haujatengenezwa upya ili kujumisha mifumo mipya iliyotengenezwa kama mfumo wa leseni ya Michezo ya Kubahatisha, Ukaguzi na Utekelezaji wa Maombi (GLICA) na Mfumo wa Udhhibiti wa Umeme (GREMS) ambayo tayari imesambazwa na inatumika.

Kwa kuongezea, niliona kuwa katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Chuo Kikuu cha Mzumbe hakuna mapitio wala majaribio ya DRP yaliyofanyika. Chuo Kikuu cha Mzumbe hakijafanya mapitio ya BCP tangu Septemba 2014 wakati TBS tangu Juni 2016.

Upungufu uliojitokeza ni kwa sababu ya ukosefu wa ufahamu wa majukumu kwa wahusika walio katika mpango huo wakuhakikisha huduma zinarejea inapotokea majanga (DRP).

Maoni yangu ni kuwa, kutofanya mapitio na majaribio ya DRP kunaweza kusababisha kushindwa kurejesha huduma au kuchelewa kurejesha huduma, ukosefu wa RPO na RTO kwa kila mfumo wa habari inamaanisha kuwa vipindi vya kutengeza nakala haviakisi kiwango cha taarifa ambacho taasisi ipo tayari kupoteza wala mda ambao taasisi ipo tayari kutokuwa na huduma yatokeapo majanga.

Napendekeza uongozi wa MLHHS na MNRT kufanya mafunzo ya ufahamu kwa wahusika(DRP Members) wanao takiwa kuhakikisha huduma zinarejea itokeapo majanga,kufanya majaribio ya DRP mara kwa mara na kuhakikisha RPO na RTO zimeainishwa katika BCP. Pia, uongozi wa GBT, TBS na MU kufanya mapitio ya BCP kuhakikisha inaakisi mazingira ya sasa ya utendaji na matarajio ya uongozi.

(c) Taratibu dhaifu za kusimamia uchukuzi wa taarifa kwenye mifumo kwa ajili ya kihifadhi ili kutumika wakati wa majanga

Wakati wa ukaguzi wangu niligundua kuwa Taasisi ya Teknolojia ya Dar es salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Ushirika cha Moshi (MoCU), Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma Mjini, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, MUST, Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya walikuwa na mfumo dhaifu wa kuchukua taarifa mbadala , pia sera na taratibu yakuchukua taarifa mbadala ilikuwa dhaifu.

katika ukaguzi wangu wa mchakato wa uchukuaji wa taarifa mbadala DIT nilibaini kuwa RTO na RPO kwa kila mfumo hazijafanuliwa kwa hivyo nilishindwa kuthibitisha ikiwa uchukuaji wa nakala ya taarifa kila siku kunaendana na makubaliano ya uongozi juu ya uchukuaji taarifa na kurejeshwa kwa huduma wakati wa janga. Pia, katika mahojiano yangu na afisa wa kanzidata nilibaini kuwa nakala za taarifa hazijachukuliwa kwa mda wa wiki tatu kutoka 7 Novemba 2020 kwa sababu ya kuvurugika kwa mfumo unotumika kuchukua nakala uitwao webmin. Pia, sikuweza kupata ushahidi wowote kuhusu kufanyika kwa majaribio ya kutumia izo nakala au mwongozo uona elekeza namna yakufanya majaribio ya izo nakala.

Vivyo hivyo wakati wa ukaguzi wa sera yakuchukua nakala za kitehama ya Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira niligundua sera hiyo haijaidhinishwa kutumika, na pia haelezi yafuatayo: hatua kamili zitakazochukuliwa ili kufanikisha uchukuaji wa nakala, Wakati ambao nakala zinatakiwa kuchukuliwa, hatua zakuchukua endapo uchukuaji wa nakala umekuwa na

shida/hitilafu na wahusika wanao takiwa kupewa taarifa endapo kumetokea hitilafu katika uchukuaji wa nakala.

Maoni yangu ni kuwa, hii inaweza kusababisha Upotezaji wa habari na taarifa zingine ikiwa kuna janga kwa sababu ya ukosefu wa mfumo kamili na sera ya kuhifadhi nakala.

Napendekeza uongozi kuhakikisha kuwa kuna: -

(a) Ufafanuzi wa RTO na RPO (b) ufuatiliaji wa uchukuaji wa nakala (c) Utaratibu wa ufanyaji wa majaribio ya uchukuaji wa nakala kwa ajili ya kurejesha huduma inapotokea hitilafu katika mifumo (d) mapitio ya sera ya kuchukua nakala na kuhakikisha inaendana na matakwa ya sasa ya taasisi.

(d) Kukosekana kwa mahali maalumu kwa kuhifadhi taarifa mbadala

Wakati wa ukaguzi wangu nilibaini Kituo cha Mahusiano ya Kigeni (CFR), Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Tiba (NIMR), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi ya Watu (MLHHS), na Taasisi ya Teknolojia ya Dar es salaam (DIT) hazikuwa na eneo la nje za kuhifadhi taarifa mbadala. taarifa mbadala zinahifadhiwa katika eneo sawa na taarifa iliyo katika mazingira ya uzalishaji.

Ni maoni yangu kwamba, kutokuwapo kwa eneo la nje la kuhifadhi nakala (offsite backup location) huziweka taarifa zote zilizo mazingira ya uzalishaji na zile za mbadala kuwa katika hatari yakupotea endapo janga likitokea.

Napendekeza uongozi wa CFR, MLHHS na DIT kuanzisha utaratibu wa kuchukua nakala za taarifa na kuweka katika seva iliyo nje ya mtandao ambayo itahakikisha kurejeshwa kwa taarifa na programu ikiwa janga litaathiri taarifa iliyo katika mazingira ya uzalishaji.

(e) kukosekana kwa nyaraka za utaratibu wa kuchukua nakala na taratibu za urejesho

Katika kukagua Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Iringa Mjini (IRUWASA), na Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Tiba (NIMR) nilibaini ukosefu wa nyaraka zinazoonyesha kufanyika kwa majaribio ya kurejesha nakala(backup data restoration) kudhibitisha matokeo na kukubalika kwa

taarifa iliyorejeshwa ili kudhibitisha uwezekano wa kurejesha taarifa inapotokea janga. Vivyo hivyo, niligundua kuwa majaribio ya kurejesha taarifa DUWASA hufanywa na idara ya TEHAMA peke yake bila kuwapo kwa wamiliki wa taarifa ili kudhibitisha matokeo ya jaribio la urejesho lililofanywa.

Maoni yangu ni kuwa, kutofanya majaribio baada ya kurejesha huduma, kunaweza kusababisha athari kama vile nakala hizo kutokidhi mahitaji ya kuendelea kwa huduma. Kwa hivyo, shirika linakuwa haliwezi kurejesha huduma ndani ya mda mwafaka.

Napendekeza uongozi wa NIMR, IRUWASA na DUWASA kutengeneza utaratibu wa namna yafanya majaribio baada ya kurejesha huduma baada ya majanga na majibu ya majaribio yanapaswa kuandikwa.

8.3 UKIUKWAJI WA KANUNI ZA MGAWANYO WA MAJUKUMU

Mgawanyo kwa Majukumu (SOD) ni msingi wa usimamizi endelevu wa udhibiti wa hatari wa ndani ya biashara. Mgawanyo wa majukumu ni kanuni inayohitaji kutenganisha majukumu muhimu ambayo ni hatari kukaa Pamoja kwa kupewa mtu Zaidi ya mmoja.

Aya ya 2.2.9.1 ya usanifu wa usalama wa Mtandao wa Serikali inahitaji kwamba Taasisi zote za Umma kutekeleza muundo wa kazi na mazoea ya kufanya kazi ambayo huwapa wafanyakazi ufikiaji salama wa taarifa za Serikali na kutoa mgawanyo mzuri wa majukumu kama inavyoamuliwa na tathmini ya Maafa(Risk assessment). Kulingana na kanuni za mgawanyo wa majukumu, majukumu yafuatayo ya TEHAMA hayawezi kuunganishwa pamoja: Mzimamizi wa mifumo na msimamizi wa kanzi-data, Mtengeneza Mifumo na msimamizi wa kanzi-data, Msimamizi wa Usalama na msimamizi wa kanzi-data, msimamizi wa usalama na Msimamizi wa Mtandao na Msimamizi wa Mtandao na msimamizi wa kanzi-data.

Ukaguzi wangu wa mgawanyo wa majukumu kwa wafanyakazi wa TEHAMA uliofanyika Mamlaka ya majisafi na Maji taka Dar es Salaam (DAWASA) ulibaini kuwa, mpango wa huduma haujaelezea mgawanyo wa majukumu kwa kila kazi za TEHAMA. Wakati wa ukaguzi nilijulishwa kuwa, ingawa mpango wa huduma hautenganishi kazi za TEHAMA lakini kwenye utekelezaji wa majukumu, wafanyakazi wa TEHAMA, wamepewa majukumu

anuwai ya TEHAMA ambayo ni msimamizi wa mfumo, msanidi programu, msimamizi wa mtandao, msaada wa mfumo na msimamizi wa kanzi-data.

Mapitio yangu ya mgawanyo wa kazi kwa wafanyakazi wa TEHAMA kulingana na majukumu yaliyopo yaligundua ukiukwaji wa mgawanyo wa majukumu ambayo kazi zifuatazo zainafanywa na mfanyakazi mmoja : usimamizi wa kanzi-data na msaada wa mfumo, Msanidi Programu na Usaidizi wa Mfumo

Vivyo hivyo, katika kukagua iliyofanyika Chuo cha Teknolojia (DIT) ili kubaini ikiwa shughuli zinazopingana za kitengo cha TEHAMA zimetengwa, nilibaini mfanyakazi mmoja wa kitengo cha TEHAMA ni msimamizi wa kanzi-data, pia ni msimamizi wa mfumo wa usimamizi wa wanafunzi mtandaoni.

Vivyo hivyo, wakati wa ukaguzi wa utendaji wa moduli ya Udahili, moduli ya uteuzi, mifumo ya maombi ya SARIS, ARIS na SAGE katika Chuo Kikuu cha Mzumbe ulibaini kuwa, wasimamizi wa mfumo wa SARIS, ARIS na SAGE wanaweza kufikia kanzi-data ya mfumo wanaosimamia. Nilijifunza pia kwamba waandaji programu wanaweza kufikia kanzi-data moja kwa moja na kufanya mabadiliko kwenye sehemu ya mbele ya mfumo wa ARIS.

Pia nilifanya uhakiki kama huo katika Wizara ya Utalii na Maliasili na nikagundua wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA wanaweza kuingia kwenye kanzi-data kwa hiyo wanamajukumu ya usimamizi wa kanzi-data, pia wafanyakazi hao hao wana jukumu la Mchambuzi wa biashara(Business Analyst). Majukumu haya hayapaswi kupewa mtu mmoja kwa wakati mmoja, kwani inatoa fursa ya matumizi mabaya ya mfumo bila kugunduliwa.

Ninakubali kuwa changamoto hii inatokana na wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA kuwa wachache kulingana na majibu ya uongozi wa vyotaasisi hizi. Hata hivyo, njia mbadala ya udhibiti kama vile mapitio ya mara kwa mara wa shughuli zao lazima utekelezwe. Zaidi, nilibaini kuwa mapitio ya mara kwa mara ya shughuli hizo hayafanyiki.

Naamini kuwa, ukosefu wa magawanyo wa majukumu yaliyofafanuliwa wazi kwa kila kazi ya kitengo cha TEHAMA na kutotofautisha kazi zinazopingana za kitengo kunaweza kusababisha shughuli za kitengo zisizo salama kupewa mtumishi mmoja na uwajibikaji usiosanifu kati ya wafanyakazi wa kitengo cha TEHAMA.

Ninapendekeza uongozi wa DAWASA, Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam (DIT), Chuo Kikuu cha Mzumbe (MU), Wizara ya Utalii na Maliasili

(MNRT) kuhakikisha kuwa, majukumu yanayopingana yametengwa. Aidha, majukumu yanayopingana yanayofanywa na mtu mmoja yanakaguliwa mara kwa mara kama udhibiti mbadala.

8.4 MAPUNGUFU YA UDHIBITI WA MABADILIKO YA MIFUMO

Mchakato wa kudhibiti mabadiliko husaidia kuzuia mabadiliko yasiyofaa ambayo yanaweza kuvuruga huduma na kuhakikisha utumiaji mzuri wa rasilimali. Majukumu na taratibu rasmi za usimamizi zinapaswa kuwekwa ili kuhakikisha udhibiti wa kuridhisha wa mabadiliko hayo yote. Udhibiti duni ni sababu iliyozoeleka ya kufeli kwa mfumo. Mapitio yangu ya udhibiti wa mabadiliko ya mifumo yalibaini shida zifuatazo:

(a) Kokosekana kwa utaratibu wa kusimamia mabadaliko yanayofanywa kwenye mifumo

Wakati wa ukaguzi katika Chuo Kikuu cha Elimu cha Mkwawa (MUCE), BRELA, Bodi ya Kitaifa ya Wahasibu na Wakaguzi na Chuo kikuu cha Mzumbe Niligundua ukosefu wa nyaraka za taratibu za usimamizi wa mabadiliko ya mifumo ili kutoa uthibitisho juu ya ufanisi wa udhibiti na usimamizi wa mabadiliko ya mifumo. Pia, nilibaini kuwa NECTA haikuwa na sera ya usimamizi wa kiraka (patch management policy) ambayo inatoa mwongozo wa jinsi viraka vinavyochaguliwa, kuthibitishwa, kutekelezwa na wakati viraka vinapaswa kutumika kwenye ofisi zote.

Kwa mwaka unaoangaziwa, kulikuwa na mabadiliko ya mfumo katika Taasisi hizi. MUCE ilitekeleza mabadiliko kadhaa ya mifumo ambayo ni pamoja na mabadiliko ya vifaa na utekelezaji wa huduma inayotolewa na Mikrosoft (Active Directory) kwa wafanyakazi wote, wanaohama kutoka kwenye mfumo wa uhasibu wa Votebook kwenda MUSE, usanidi wa Mtandao wa eneo (Local Area Network) (ukihama kutoka Firewall ya Mikrotik kwenda firewall ya Sophos), usanidi wa seva na wavuti.

BRELA pia ilikuwa ikitekeleza mabadiliko kwenye mfumo wake wa usajili mtandaoni (ORS). Vivyo hivyo, MU ilikuwa ikitekeleza uboreshaji kwa mifumo ya usimamizi wa mwanafunzi wake. Vivyo hivyo, huko NBAA nilibaini kuwa msimamizi wa mfumo alikuwa na haki za kuhariri matokeo ya wanafunzi kwenye mfumo na hakukuwa na mwongozo ulioandikwa juu ya jinsi mabadiliko yalipaswa kuanzishwa, msimamizi aliagizwa kwa barua pepe kutoka kwa afisa uchunguzi (examination officer). Hakuna tarifa ya

mabadiliko iliyotumwa kiatomati kwa msimamizi / afisa wa uchunguzi baada ya mabadiliko kufanywa.

Kwa hivyo ninaamini ni muhimu kwa mabadiliko haya kudhibitiwa na kusimamiwa vyema ili kuepuka usumbufu na kuanzisha ukiukaji wa usalama kwenye mazingira ya uzalishaji, ikizingatiwa kuwa mabadiliko haya yalitekelezwa kwa mifumo ambayo inafanya kazi.

Nina wasiwasi kwamba kukosekana kwa udhibiti katika kusimamia mabadiliko na viraka vinaweza kusababisha mabadiliko yasiyoruhusiwa ambayo yanaweza kuathiri utendaji na usalama wa mifumo jambo ambalo litasababisha usumbufu katika kutoa huduma na kusababisha udhaifu wa kiusalama wa mfumo.

Ninapendekeza uongozi wa MUCE, BRELA, NBAA, MU na NECTA kuandaa utaratibu wa mabadiliko ya mfumo na taratibu za usimamizi wa kiraka(patch Management) kudhibiti vyema mabadiliko yanayofanywa kwenye mifumo.

(b) Kutotenganishwa Kwa Mazingira ya Utengenezaji, Majaribio, na Uendeshaji

Aya ya 12.1.4 ya Shirika la Kimataifa la Viwango (ISO) 27002: 2013 inahitaji mazingira ya utengenezaji, majaribio na mazingira ya utendajikazi kutengwa ili kupunguza hatari za ufikiaji bila idhini au mabadiliko kwenye mazingira ya utendaji.

Wakati wa ukaguzi wangu wa usimamizi wa mabadiliko ya mifumo katika chuo cha Teknolojia Dar es salaam (DIT), niligundua kuwa licha ya uongozi kuwa na mifumo iliyotengenezwa ndani, haikuwa na mazingira ya upimaji na mazingira ya matengenezo bali walitumia kompyuta zao kibinafsi na mazingira ya uzalishaji. Ukaguzi wa vibali vilivyotolewa kwa wageni wa vivutio vya utalii katika mfumo wa MNRT portal katika Wizara ya Utalii na Maliasili umebaini kuwapo kwa vibali ambavyo viliundwa kwa lengo la majaribio, jambo hili nikinyume na namna bora(best practice) ambapo majaribio hayapaswi kufanywa katika mazingira ya utendaji(operational environment). Vivyo hivyo, ukaguzi wangu wa watumiaji wa mfumo wa uhasibu wa SAGE uliofanyika Kampuni ya viwanja vya ndege Kilimanjaro (KADCO) ulibaini akaunti za watumiaji zinazotumika kwenye mazingira ya majaribio zipo kwenye mazingira ya uzalishaji.

Nina wasiwasi kuwa kushindwa kutofautisha mazingira ya matengenezo, upimaji na utendajikazi kunaongeza hatari ya Wadukuzi kuingia kwenye mfumo bila ruhusa Maalumu na mabadiliko kwenye mazingira ya utendaji.

Ninapendekeza kwa Menejimenti za MNRT, DIT na KADCO kuhakikisha kwamba kuna mgawanyo wa mazingira ya matengenezo na majaribio na kuimarisha udhibiti ili kuhakikisha kuwa majaribio hayafanywi katika mazingira ya uzalishaji.

(c) Kutofuata utaratibu wa usimamizi wa mabadiliko ya mifumo

Ukaguzi wangu wa taratibu za usimamizi wa mabadiliko ya mifumo uliofanyika Mamlaka ya Bandari Tanzania(TPA) ulibaini kwamba Aya ya 3.1 ya sera ya usimamizi wa mabadiliko ya mifumo, taratibu na miongozo ya TPA inahitaji mchakato wa Usimamizi wa Mabadiliko uanzishwe kwa maombi ya Mabadiliko (change Request), maombi hayo yawasilishwe baada ya kujaza Fomu ya Ombi la Mabadiliko namba 2A. Pia inahitaji Maombi yote ya Mabadiliko kupitiwa na Timu ya Usimamizi wa Mabadiliko (CMT), na yakishaidhinishwa, yaruhusiwe na Mamlaka ya Mabadiliko (change Authority)

Sera inaelezea zaidi kuwa, Maombi yote ya Mabadiliko yanayopendekezwa lazima yajumuishe, mpango wa utekelezaji, mpango wa majaribio, tathmini ya hatari na Uhifadhi wa Mabadiliko utafanywa katika rejista ya Usimamizi wa Mabadiliko (change management register) ambayo inapaswa kupitiwa ili kuboresha mchakato na utambuzi wa sababu za msingi. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa mazoezi ya usimamizi wa mabadiliko ya mifumo ulibaini makosa yafuatayo: -

- (i) Mamlaka ya mabadiliko (Change Authority) ina mwanachama mmoja tu, Mkurugenzi wa TEHAMA ambaye huondoa majukumu na ufahamu wa utekelezaji wa mabadiliko kwa idara za watumiaji ambao ndio wamiliki wa mifumo. Miundombinu ya Teknolojia ya Habari (ITIL) na taratibu bora (best practice) zinahitaji mamlaka ya mabadiliko (change authority) au bodi kuwa na wanachama kutoka kwenye shirika lote, kila idara inatakiwa kutoa mwakilishi atakayekuwa kwenye bodi hiyo. Usanidi huu unahakikisha kuwa, mabadiliko ambayo yanaathiri mifumo mingi katika shirika inahusisha watumiaji kutoka idara husika.

- (ii) Kukosekana kwa rejista ya mabadiliko (change registry) ambao huweka kumbukumbu na nyaraka za mabadiliko kwa kumbukumbu na ufuatiliaji rahisi.
- (iii) Kutokufuata sera na miongozo ya mabadiliko o ambayo ilitekelezwa katika mwaka unaoangaziwa. Katika mwaka uliopitiwa kulikuwa na mabadiliko kwenye Mfumo wa (POAS) na Mfumo wa (POS) ambayo yalitekelezwa. Hata hivyo, ukaguzi wangu ulibaini kuwa, fomu ya ombi la mabadiliko haikujazwa, kukaguliwa na kupitishwa na timu ya usimamizi wa mabadiliko. Mamlaka ya mabadiliko haikuidhinisha mabadiliko haya. Kwa kuongezea, hakukuwa na mpango wa utekelezaji ulioandaliwa, mpango wa majaribio, na tathmini ya hatari, ambayo ni kinyume na sera ya usimamizi wa mabadiliko ya TPA.

Ukaguzi kama huo uliofanyika Mamlaka ya uhifadhi ya Ngorngoro (NCAA) ulibaini kwamba Aya ya 4.4.2.2 (i) ya sera ya TEHAMA ya NCAA inahitaji mchakato wa usimamizi wa mabadiliko kujumuisha hatua zifuatazo. Kila moja ya hatua hizi lazima zikamilishwe kwa kila mabadiliko yatakayofanywa, Mwombaji kujaza fomu ya usimamizi wa mabadiliko (Fomu Na. 4), bodi ya usimamizi wa mabadiliko kukagua na kuidhinisha mabadiliko, kisha Kitengo cha TEHAMA kinaweza kurudisha mombi hayaa kwa mwombaji ili kupata maelezo Zaidi kama yanahitajika.

NCAA ilitekeleza mabadiliko matano kwenye mfumo wa Safari portal na badiliko moja kwenye mfumo wa Rasilimali Watu. Mapitio ya utoaji, idhini na utekelezaji wa mabadiliko haya ulibaini yafuatayo:

- (i) Mapitio na idhini ya bodi ya usimamizi wa Mabadiliko haikuthibitishwa na ripoti iliyotolewa,
- (ii) Hakukuwa na nyaraka za kuhalalisha kuwa mabadiliko haya yalijaribiwa na kutiwa saini na idara ya watumiaji kabla ya kupelekwa kwenye mazingira ya uzalishaji, na
- (iii) Sera ya TEHAMA haijaainisha mambo muhimu yafuatayo ya udhibiti wa mabadiliko: majukumu na muundo wa kamati ya usimamizi wa mabadiliko, taratibu na mwongozo wa majaribio, tathmini ya athari, usimikaji na kupitisha ukaguzi wa mabadiliko.

Vivyo hivyo, mapitio ya mabadiliko yaliyofanyika Mfuko wa hifadhi ya jamii (PSSSF), yalibaini kuwa, mabadiliko yamewekwa katika fomu. Pia,

hakukuwa na utaratibu wa ufuatiliaji wa mabadiliko ambao unaweza kufuatilia mabadiliko yote ambayo yanatekelezwa katika mifumo yote, uongozi hauwezi kufuatilia mabadiliko ambayo hayajaruhusiwa katika mazingira ya uzalishaji, kwa hivyo sikuweza kubaini utimilifu wa mabadiliko yaliyofanywa katika mifumo ya Mfuko (Microsoft Navision na Mfumo wa Utawala wa Wanachama) katika mwaka unaoangaziwa.

Kwa kuongezea, nilibaini kuwa mabadiliko matatu yalifanyika wakati wa ukaguzi, mabadiliko mawili hayakufanyiwa majaribio yanayofanywa na watumiaji (UAT) jaribio moja lilikuwa na mipango iliyoambatanishwa lakini hakukuwa na matokeo ya majaribio ya mfumo yaliyofanywa na watumiaji. Hii ni kinyume na Sera ya TEHAMA ya PSSSF ambayo inahitaji matokeo ya majaribio yanayofanywa na watumiaji kusainiwa na kuwekwa pamoja na maelezo au mombi ya mabadiliko.

Nina wasiwasi kuwa, kutofuata taratibu za usimamizi wa mabadiliko ya mifumo kunaweza kusababisha mabadiliko yasiyodhibitiwa ambayo yanaweza kuathiri utendaji na usalama wa mifumo na kusababisha usumbufu kwa watumiaji na upotezaji wa data.

Napendekeza kuwa:

- (a) Uongozi wa TPA kuanzisha mamlaka ya mabadiliko(change Authority) ambayo ina wanachama katika idara zote za TPA, kuanzisha rejista ya mabadiliko ili kuweka kumbukumbu na nyaraka za mabadiliko yaliyoombwa na kuimarisha udhibiti wa mabadiliko yote kwenye mifumo ili yafuate sera, taratibu na miongozo ya usimamizi wa mabadiliko.
- (b) Uongozi wa NCAA kufafanua majukumu na muundo wa kamati ya usimamizi wa mabadiliko na uimarisha udhibiti ili kuhakikisha mabadiliko yote kwenye mifumo yanafanywa kulingana na miongozo ya usimamizi na taratibu zilizoainishwa katika sera ya TEHAMA.
- (c) Uongozi wa PSSSF kuhakikisha kuwa mfumo wa ufuatiliaji wa mabadiliko umesimikwa ili kufuatilia kila mabadiliko yanayofanyika kwenye mfumo wa Mfuko(Fund's systems) na taratibu za Majaribio na mchakato wa kukubalika pamoja na kuandaa kesi za majaribio inapaswa kuandikwa na kuambathishwa na rekodi ya mabadiliko.

8.5 USIMAMIZI USIOFANISI WA WATOA HUDUMA ZA TEHAMA

Katika ukaguzi wangu pia nilipitia tathmini ya udhibiti unaohusishwa na usimamizi wa wauzaji/wazabuni wa TEHAMA kuhakikisha kiwango sahihi cha utoaji wa huduma kinadumishwa. Madhaifu yafuatayo yalibainika katika ukaguzi wangu:

(a) Ukosefu wa makabaliano ya viwango vya huduma baina ya taasisi za umma na watoa huduma za TEHAMA

Mkataba wa kiwango cha huduma (SLA) ni makubaliano au mkataba kati ya shirika (mpewa huduma) na mtoa huduma ambao unaelezea majukumu na matarajio ya uhusiano kati ya shirika (mpewa huduma) na watoa huduma wake.

Katika ukaguzi wangu wa Mfuko wa Dhamana ya Maendeleo ya Pamba (CDTF), Mamlaka ya Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB), Ofisi ya Viwango Tanzania (TBS), Mashirika ya Usafirishaji Tanzania (TASAC), na PPRA, Nilibaini ukosefu wa mikataba ya kiwango cha huduma kati ya vyombo husika na watoa huduma wa TEHAMA.

Mapitio yangu ya PSPTB nilibaini kuwa mamlaka hiyo ina mfumo (ERMS) ambao umetengenezwa na kudumishwa na wakala wa Mtandao wa Serikali na kusimamiwa moja kwa moja na Idara ya TEHAMA. Hata hivyo, sikuweza kupata ushahidi wa mkataba wa kiwango cha huduma (SLA). Hii pia ilikuwa ni kesi inayofanana na CDTF ambapo bodi haikuwa na mkataba wa kiwango cha huduma (SLA) na muuzaji/mzabuni wa mfumo wao wa uhasibu.

Vivyo hivyo, wakati wa ukaguzi wa NCAA, TASAC na TBS, niligundua kuwa wakala wa Mtandao wa Serikali (EGA) imezipatia mamlaka husika msaada na udumishaji wa huduma ya barua pepe, huduma za kituo cha data kwa ajili ya kusimika (hosting) mifumo na kuhakikisha mwendelezo wa mradi (business continuity). Hata hivyo, taasisi hazikuwa na makubaliano ya kandarasi na kiwango cha huduma (SLA) na EGA ili kufafanua majukumu ya kila sehemu na kuelezea vigezo vya kuashiria kiwango kinachotarajiwa cha huduma iliyotolewa.

Kwa kuongezea, ukaguzi wangu wa usimamizi wa miundombinu na utendajikazi wa mfumo wa kielektroniki wa ununuzi (TANePS) kutoka PPRA nilibaini kuwa tarehe 12 Juni 2019 PPRA iliingia mkataba na Mamlaka ya

serikali matandao kwa kutoa huduma ya kituo cha data kwa ajili ya kusimika mfumo wa TANEPS, kiasi cha Sh. 150, 512,854.24 inayolipwa kila mwaka kutoka 1 Julai 2019 hadi 30 Juni 2020. Hata hivyo, ukaguzi wangu wa mkataba wao niligundua kuwa hauna makubaliano ya kiwango cha huduma na utaratibu wa kupima kiwango cha utoaji wa huduma.

Mwishowe, wakati wa ukaguzi wangu wa mfumo wa mapato TRIS toka TARURA nilibaini kuwa mfumo huo ni zao lililotokana baada ya kubadilisha na kuboresha baadhi ya vipengele vya mfumo wa LGRCIS kutoka OR-TAMISEMI. Pia nilibaini kuwa mfumo umesimikwa na unasimamiwa na OR-TAMISEMI. Hata hivyo, hakukuwa na makubaliano au mkataba wa makubaliano (MOU) kati ya TARURA na OR-TAMISEMI kufafanua majukumu na uwajibikaji wa pande zote mbili.

Kwa mfano, tulibaini kuwa tangu 30 Desemba 2020 mfumo ulikuwa na mapungufu katika kutoa ripoti, ikiwa ni pamoja na ripoti ya upatanisho wa fedha (Cashier reconciliation report), kitabu cha pesa cha ukusanyaji wa Mapato (Revenue collection cash book), ripoti ya makusanyo ya mapato (Miscellaneous Collections), na kitabu cha ukusanyaji (collection journal) hakitoi taarifa sahihi za ukusanyaji. Mapungfu haya yaliripotiwa kwa OR-TAMISEMI. Hata hivyo, yalibaki hayajasuluhishwa hadi wakati wa ukaguzi Januari 5, 2021. Zaidi ya hayo, wakati wa ukaguzi iligundulika kuwa Wakala iliripoti kwa OR-TAMISEMI kwamba, vifaa vingine vya POS havifanyi kazi kwa siku kadhaa haswa Jumatatu asubuhi, ingawa suala hilo lilisuluhishwa mara moja hitilafu bado imekuwa ikijirudia.

Maoni yangu ni kuwa, bila mkataba na SLA basi uwajibikaji na matarajio haswa kwa kiwango cha huduma hayawezi kupatikana kwa taasisi wakati inashindwa kumwajibisha muuzaji iwapo kukatika kwa huduma au utoaji wa msaada wa wakati usiofaa.

Ninapendekeza uongozi wa NCAA, PSPTB, TBS, TASAC, PPRA na CDTF kuhakikisha Mkataba na makubaliano ya kiwango cha huduma na muuzaji/mzabuni umeanzishwa. Pia, uongozi wa TARURA na OR-TAMISEMI kukubaliana juu ya utaratibu maalumu ili kuhakikisha utatuzi unaofaa kwa wakati wa maswala yanayohusiana na matumizi ya mfumo wa TRIS.

(b) Mapungufu ya mikataba kati ya Taasisi za umma na watoa huduma za TEHAMA

Wakati wa ukaguzi katika Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mbeya Mjini nilibaini kuwa makubaliano kati ya muuzaji/mzabuni na Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Mbeya yalikuwa na upungufu kama vile ukosefu wa kifungu cha faragha ya data, makubaliano ya SLA na viashiria vinavyohusu ubora wa huduma itakayotolewa, dhamana ya muda wa juu sio chini ya 98%, na kukosekana kwa taratibu zinazohitajika kurekebisha masharti na wigo wa mkataba.

Hii inamaanisha kuwa, maslahi ya Mamlaka katika usimamizi wa mikataba hayalindwi na hukalibisha hatari ya mashtaka yasiyo ya lazima

Ninapendekeza uongozi wa mamlaka ya usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira ya Mjini Mbeya kupitia upya mkataba na kuhakikisha kuwa vifungu vinavyohusika vipo ili kulinda maslahi ya taasisi na kuzuia mashtaka yasiyo ya lazima.

8.6 KUKOSEKANA KWA UFANISI WA HUDUMA ZA TEHAMA NA USIMAMIZI WA MATUKIO YA TEHAMA

Kwa mujibu wa aya ya 2.3.23 ya usanifu wa miundombinu, viwango na miongozo ya kiufundi ya Mtandao wa Serikali inahitaji Taasisi za Umma kuandaa Taratibu za Usimamizi wa Huduma za TEHAMA, huduma ambazo zinaweza kuzingatiwa kwa:

- (i) Usimamizi wa matukio - kurejesha huduma za kawaida za Taasisi za Umma kwa haraka iwezekanavyo, na kupunguza athari mbaya kwa shughuli zinazoendelea.
- (ii) Usimamizi wa ombi la huduma - kuwezesha watumiaji wa TEHAMA kuomba na kupokea huduma mapema ndani ya muda uliowekwa.
- (iii) Usimamizi wa Dawati la Msaada - kutoa mfumo ulio sanifu wa kusajili na kutatua maswala ya TEHAMA yaliyoripotiwa.

Katika ukaguzi wangu wa utoshelevu wa utoaji wa huduma za TEHAMA na usimamizi wa matukio ya TEHAMA nilibaini mapungufu yafuatayo:

(a) Kukosekana kwa utaratibu wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa baadhi ya taasisi hazikuwa na nyaraka za kumbukumbu za taratibu za usimamizi wa matukio ya TEHAMA ili

kuhakikisha utunzaji mzuri wa matukio yaliyoripotiwa ili kupunguza athari kwenye shughuli za Taasisi. Taasisi hizo ni Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC), Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Mbeya, Chuo Kikuu Mzumbe, Taasisi ya Kitaifa ya Utafiti wa Tiba (NIMR), BRELA, Mashirika ya Usafirishaji Tanzania, Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Dodoma, Wizara ya Ardhi, Nyumba na maendeleo na Makazi (MLHHS), Wizara ya Utalii na Maliasili (MNRT), na Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA).

Ni maoni yangu kwamba, ukosefu wa nyaraka za utaratibu wa usimamizi wa matukio ya TEHAMA unaweza kusababisha kushindikana kwa kutambuliwa na kusuluhisha visa au matukio kwa wakati na kulingana na vipaumbele vya huduma kupunguza usumbufu wa kiuendetaji. Matukio hupelekea shida ikiwa kama hayasimamiwi vyema.

Ninapendekeza uongozi wa AICC, Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Mbeya, Chuo Kikuu Mzumbe, NIMR, BRELA, TASAC, Mamlaka ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Dodoma, MLHHS, MNRT na PPRA kuandaa taratibu za usimamizi wa matukio ya TEHAMA.

(b) Udhaifu katika usimamizi wa Maombi ya huduma na dawati la msaada wa TEHAMA

Wakati wa ukaguzi wa PSSSF niligundua kuwa matukio yanayotokea yanaingizwa kwenye mfumo wa Dawati ya Msaada. Baada ya kupitia mfumo ilibainika kuwa matukio mengine hayakupewa mtu wa kuyashughulikia, na mwenendo wake haukuonyesha ikiwa yametatuliwa, yameshindikana au la. Kwa kuongezea, nilibaini kuwa hakukuwa na mapitio ya mara kwa mara ya matukio/visa vilivyoripotiwa ili kuchukua hatua stahiki kwa visa/matukio ambayo bado yako wazi hayajashughulikiwa na kutambua matukio yanayojirudia ambayo yanahitaji kupelekwa kwa uongozi ili yatafutiwe suluhisho la kudumu

Mapitio yangu juu ya usimamizi wa mombi ya huduma na dawati la msaada wa TEHAMA katika TASAC yalibaini ukosefu wa utaratibu wa kupokea na kurekodi maombi ya huduma na matukio ya TEHAMA yaliyoripotiwa na wafanyakazi kuhakikisha yanashughulikiwa kwa ufasaha na kwa wakati sahihi. TASAC inaanza utekelezaji wa uundaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuziendesha shughuli zake za kila siku. Mifumo hiyo itatumiwa na

wadau wa ndani na wa nje. Hivyo, kuweka utaratibu wa kupokea, kurekodi na kusimamia maombi ya huduma ya TEHAMA na matukio ya TEHAMA ambayo ni muhimu kuhakikisha kuwa yanatatuliwa kwa wakati ili kuzuia usumbufu na kuwaridhisha wadau .

Vilevile, ukaguzi wangu wa mamlaka ya maji na usafi wa mazingira mjini Dodoma ulibaini kuwa mamlaka haina mfumo wa dawati la msaada wa TEHAMA ili kusaidia kusimamia ipasavyo maombi ya huduma ya TEHAMA na ufuatiliaji wa mara kwa mara wa matukio ya TEHAMA. Kutokan na sababu hiyo, Mamlaka haidumishi yafuatayo: Nyaraka ya kumbukumbu za matukio kwa ajili ya kuhifadhi na kudumisha matukio yote yaliyoripotiwa, rekodi ya matukio yaliyoripotiwa na ikiwa yanashughulikiwa ndani ya muda sahihi. Vivyo hivyo, katika Baraza la Kitaifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) nilibaini kuwa hakukuwa na utaratibu wa kupokea, kurekodi na kufuatilia matukio na kusaidi maswali/shida mbalimbali kutoka kwa watumiaji wa ndani (wafanyakazi).

Nilifanya ukaguzi kama huo huko MLHHS na nikabaini kuwa Wizara inashughulikia maombi ya huduma na matukio ya TEHAMA kupitia baruapepe, kikundi cha *WhatsApp*, na kupiga simu na hakuna utaratibu wa kuchambua visa/matukio yanayojitokeza mara kwa mara ili kuhakikisha suluhisho linalofaa linatambuliwa ili kuzuia kuwa shida. Ni maoni yangu kuwa, utumiaji wa barua pepe, vikundi vya *WhatsApp* na simu sio mzuri katika kufuatilia mwenendo na kutunza kumbukumbu kwa ajili ya mapitio na hakiki za baadaye. Hii pia ilibainika katika MNRT ambapo Wizara haina mfumo wa dawati la msaada ya TEHAMA kwa madhumuni ya kudhibiti matukio yaliyoripotiwa na maombi ya huduma ya TEHAMA.

